KAMPUNI NI DHAHABU

(JINSI YA KUANZISHA

&

KUENDESHA KAMPUNI).

BY:

MR. GODFREY EDWARD.



©2020.

MAWASILIANO NA GFOX INVESTMENT

Website: www.gfoxinvestment.co.tz

Email: travesgodfrey@yahoo.com

Simu: 0656-058184

Instagram: official_mrgodfrey

© 2020 GODFREY EDWARD

I S B N 978-9976-5609-0-9.

© Copyright 2020.

Haki zote zimehifadhiwa: kitabu hiki hakiruhusiwi kunakiliwa au kubadilishwa kwa njia yoyote ile ya kielektroniki, kimekanikali au kifizikali. kitabu hiki cha **KAMPUNI NI DHAHABU** pia hauruhusiwi kukitoa nakala kivuli, kukiskani au kukibadilisha kwa njia yoyote ile bila ruhusa rasmi ya muandishi wa kitabu hiki **Mr. Godfrey Edward**. Kwa suala lolote kuhusu kitabu hiki wasiliana moja kwa moja na Ofisi ya **GFOX INVESTMENT.**

KAMPUNI NI DHAHABU.

KITABU CHA ELIMU YA BIASHARA.

Disclaimer: Elimu inayopatikana kwenye kitabu hiki ina malengo ya kukupa mafunzo ya awali ya biashara na uwekezaji kwenye Kampuni. Kitabu hiki siyo mbadala wa ushauri wowote wa mtaalamu mwingine wa biashara na uwekezaji. Kama una suala la biashara usisite kutafuta ushauri kutoka kwa mtaalamu wa masoko na fedha. Pia fahamu kwamba elimu kuhusu Kampuni inayotolewa kwenye hiki kitabu, inaweza kubadilika kadri muda unavyozidi kwenda mbele.

KUHUSU MWANDISHI.



MR. Godfrey Edward ana shahada ya kwanza ya usimamizi wa biashara na masoko **(Bachelor Degree of Business Administration in Marketing)** kutoka chuo cha **Mzumbe University** aliyohitimu mwaka **2016.**

Baada ya hapo mwandishi **Mr. Godfrey Edward** alianza kufanya kazi kama mwajiriwa kwenye kampuni ya simu kama afisa mauzo wa simu na vifaa vya simu **(Sales Representative).**

Mr. Godfrey alikuwa anafanya kazi ya kutafuta masoko mapya ya simu na vifaa vya simu Dar es salaam, Tanzania kwenye masoko kama **Kariakoo, Buguruni, Tandika** mpaka **Tegeta.**

Kutokana na kusambaza simu na vifaa vya simu kwenye masoko makubwa kama haya **Mr Godfrey Edward** alipata uzoefu mkubwa wa kuelewa wafanyabiashara pamoja na changamoto zao. Pia alipata ujuzi kwa vitendo wa **kutangaza bidhaa mpya, kushawishi wateja kununua bidhaa** pamoja na kumudu **mauzo na fedha** za mauzo pamoja na kujifunza mbinu za kisasa za **Kurekodi mauzo ya bidhaa** kwa kutumia simu janja **(Smartphone)** na **Computer.**

Kutokana na ujuzi aliopata sokoni kwa muda wa miaka miwili. Mwaka (**2018) Mr Godfrey Edward** alianza kuandika kitabu chake cha kwanza alichokiita **USHINDANI WA BIASHARA.** Kitabu hiki kinaelezea **vitu 10** ambavyo kila mfanyabiashara au mtu anaetaka kuingia kwenye biashara anatakiwa kuvifahamu ili aweze kuwa mshindani wa kweli sokoni.

Vitu hivyo kumi kwenye kitabu cha USHINDANI WA BIASHARA ni,

#1. Mbinu za kupata mtaji wa biashara

#2. Mbinu za kutengeneza Bidhaa bora

#3.Eneo bora la biashara

#4. Mbinu na vigezo vya kupanga bei za bidhaa

#5. Mbinu za kutangaza biashara na bidhaa

#6. Mbinu za kufahamu wateja halisi

#7. Mjue mshindani kwenye biashara

#8. Mbinu za usambazaji bidhaa na huduma

#9. Mbinu za kukokotoa mahesabu ya biashara

#10. Tofauti kati ya mfanyabiashara na mjasiriamali.

Kitabu hiki cha **USHINDANI WA BIASHARA** kilifanikiwa kuuza zaidi nakala (**500) Tanzania** nzima na kinaendelea kufanya vizuri sokoni hadi sasa. Kitabu hiki cha **USHINDANI WA BIASHARA** kimesambazwa kwenye maduka mbalimbali ya vitabu **Tanzania.**

Mwaka (**2019)** Mr. **Godfrey Edward** aliamua kuacha kazi na kuamua kufungua **kampuni binafsi yenye Ukomo wa hisa (A Private Company Limited by Shares)** akishirikiana na wanahisa wengine na kuanzisha kampuni inayoitwa **GEMIX COMPANY LIMITED** ambayo

inajihusisha na **uuzaji wa asali mbichi (GEMIX HONEY)** na uwekezaji kwenye **Majengo** na **Migahawa.**


Miezi **sita (6)** baadae **Mr. Godfrey Edward** aliandika kitabu chake cha pili kuhusu masuala ya kampuni kinachoitwa **KAMPUNI NI DHAHABU.**

Kitabu hiki cha **KAMPUNI NI DHAHABU** kinaelezea **aina mbalimbali za biashara, jinsi ya kusajili kampuni Tanzania, umuhimu wa kumiliki kampuni na masuala mengine ya kampuni kama hisa na hatifungani.**

Kitabu cha **KAMPUNI NI DHAHABU** nacho kimepokelewa vizuri sokoni na kufanikiwa kuuza zaidi ya **nakala 200 Tanzania** nzima.


Mpaka sasa **(2020) Mr. Godfrey Edward** ni **Mkurugenzi Mkuu Wa Kampuni ya GEMIX COMPANY LIMITED** na pia anatoa **Seminar Za Biashara** na uwekezaji kwa njia za video na mafunzo ya maandishi kwenye mitandao ya kijamii ya **Instagram (Mr godfrey business)** na **WhatsApp** kwa kufungua group la mafunzo ya biashara kwa jina la **(THE BILLIONAIRE MINDS**). Pia **Mr. Godfrey Edward** anatoa mafunzo kwa njia ya video kupitia **YouTube channel** yake ya **(Mr Godfrey Business).**

Hakikisha unamfuatilia **Mr Godfrey Edward** ili uweze kupata mafunzo mbalimbali ya biashara na uwekezaji kwa njia za kisasa zaidi.



KAMPUNI NI DHAHABU

(10,000/= TZS)



USHINDANI WA BIASHARA

(10,000/= TZS)

MOBILE: 0656 058184

EMAIL: travesgodfrey@yahoo.com

TABLE OF CONTENTS

KUHUSU MWANDISHI. 4

DIBAJI....16

SEHEMU YA KWANZA....18

1. MIUNDO YA BIASHARA....18

KUSAJILI JINA LA BIASHARA YA MTU MMOJA (SOLE-PROPRIETOR REGISTRATION 23

BIASHARA YA USHIRIKIANO (PARTNERSHIP).....26

UBIA (JOINT VENTURE) 28

FRANCHISE....30

MIUNDO YA BIASHARA TOFAUTI NA SIFA ZAKE.33

SEHEMU YA PILI....39

Kampuni ni nini? 39

AINA ZA KAMPUNI 40

KAMPUNI KUTOKANA NA UMILIKI.....41

KAMPUNI BINAFSI (PRIVATE COMPANY). 41

KAMPUNI YA UMMA (PUBLIC COMPANY) 42

KAMPUNI BINAFSI KUWA YA UMMA (I.P.O) 44

KAMPUNI YA KIGENI (FOREIGN COMPANY). 46

KAMPUNI YENYE UKOMO WA MADAI (A LIMITED COMPANY). 47

KAMPUNI YENYE UKOMO WA MADAI WA HISA (A COMPANY LIMITED BY SHARES).....48

KAMPUNI YENYE UKOMO WA DHAMANA....49

(A COMPANY LIMITED BY GUARANTEE). 49

KAMPUNI ISIYO NA UKOMO WA MADAI (UNLIMITED COMPANY). 50

SIFA ZA KAMPUNI TOFAUTI....51

JINSI YA KUSAJILI KAMPUNI. 54

VITU VYA KUWA NAVYO WAKATI UNATAKA KUANZISHA KAMPUNI. 55
- **kitambulisho cha taifa** 56
- **TIN** 56
- **Anuani ya makazi** 56
- **Barua ya utambulisho wa makazi** 56

KUKATA LESENI YA BIASHARA KWENYE TOVUTI (ONLINE BUSINESS LICENSE REGISTRATION). 63
SIFA ZA KAMPUNI. 65
1.KAMPUNI NI MTU WA KUFIKIRIKA KISHERIA (ARTIFICIAL PERSON). 65
2. MALI ZA KAMPUNI HAZI INGILIANI NA MALI BINAFSI ZA WANAHISA WA KAMPUNI HUSIKA (SEPARATE LEGAL ENTITY). 66
3. KAMPUNI INATAKIWA ISAJILIWE KISHERIA NA IPATE CHETI CHA KAMPUNI (CERTIFICATE OF INCORPORATION). 66
4. KAMPUNI INATAKIWA IWE NA MUHURI WAKE (COMPANY SEAL). 67

SEHEMU YA TATU 69
3. MTAJI WA KAMPUNI 69
KAMPUNI KUTUMIA MTAJI MBEGU (SEED CAPITAL RAISING). 70
MTAJI MBEGU WA JUMUIYA. 71
KAMPUNI KUUZA HISA 73
HISA NI NINI? 73
AINA ZA HISA 75
- **ORDINARY SHARES** 75
- **PREFERENCE SHARES** 75
- **CUMULATIVE PREFERENCE SHARES** 75
- **REDEEMABLE SHARES** 75
- **NON-REDEEMABLE SHARES** 75

ORDINARY SHARES. 76
PREFERENCE SHARES 77
CUMULATIVE PREFERENCE SHARES..... 78
REDEEMABLE SHARES..... 78
NON-REDEEMABLE SHARES..... 79
THAMANI YA KIPANDE CHA HISA (SHARE VALUE).
..... 80
ASILIMIA (%) ZA UMILIKI KWENYE KAMPUNI. 81
❖ **GAWIO (DIVIDEND) KWA WANAHISA. 87**
❖ **SERA YA GAWIO (DIVIDEND POLICY).** 88
GAWIO KWA HISA (DIVIDEND PER SHARE) 89
KAMPUNI KUKOPA BENKI 97
KAMPUNI KUUZA HATIFUNGANI 98
HATIFUNGANI 98
AINA ZA HATIFUNGANI. 99
- Hatifungani ya muda mfupi **(Treasury Bills).** 99
- Hatifungani ya kati **(Treasury Notes).**..... 99
- Hatifungani ya muda mrefu **(Treasury Bonds).** 99

****** 99**
****** 101**
****** 102**
❖ **HATIFUNGANI YA MUDA MREFU (TREASURY BOND)..... 103**
❖ **HATIFUNGANI KUTOKANA NA MTOAJI 104**
1. HATIFUNGANI YA SERIKALI (GOVERNMENT BOND) 104
5. HATIFUNGANI ZA BENKI 109
1. HATIFUNGANI YENYE DHAMANA (SECURED BOND). 111
2. HATIFUNGANI ISIYO NA DHAMANA (UNSECURED BOND). 112

DEBENTURE. **112**

1. HATIFUNGANI INAYOBADILIKA (CONVERTIBLE DEBENTURES). 113

2. HATIFUNGANI ISIYOBADILIKA (NON-CONVERTIBLE DEBENTURES). 114

3. HATIFUNGANI ZINAZOWEZA KUNUNULIWA MAPEMA (CALLABLE DEBENTURES). 114

3. HATIFUNGANI ISIYOWEZA KUNUNULIWA MAPEMA (NON-CALLABLE DEBENTURES). 115

SEHEMU YA NNE **119**

4. WANAHISA NA WAKURUGENZI KWENYE KAMPUNI. **119**

- **WANAHISA (SHAREHOLDERS).** 119
- **WAKURUGENZI (DIRECTORS).** 120
- **MAJUKUMU YA MKURUGENZI MKUU** 122
- **KUCHAGUA BODI YA WAKURUGENZI.** 123
- **KUCHAGULIWA KWA MKURUGENZI MKUU KWENYE KAMPUNI.** 125
- **UKOMO WA MKURUGENZI KWENYE KAMPUNI** **126**
- **MUUNDO WA UTAWALA KWENYE KAMPUNI.** **128**

I) WANAHISA/WAMILIKI WA KAMPUNI 129

II) BODI YA WAKURUGENZI 129

III) MAMENEJA/ MAAFISA KWENYE KAMPUNI. 129

IV) WAFANYAKAZI WENGINE 130

SEHEMU YA TANO **131**

#5. WARAKA NA KATIBA YA KAMPUNI (MEMORANDUM & ARTICLES OF ASSOCIATIONS **131**

- **WARAKA WA KAMPUNI (MEMORANDUM OF ASSOCIATIONS).** 131

Vipengele sita (6) kwenye memorandum **132**

1. JINA LA KAMPUNI 132
2. MAKAO MAKUU YA KAMPUNI. 134
3. SHUGHULI ZOTE ZA KAMPUNI. 134
4. AINA YA UKOMO UTAKAOTUMIWA NA KAMPUNI HUSIKA (Limited or Unlimited Company). 136
5. MTAJI WA JUMLA WA KAMPUNI (AUTHORIZED SHARE CAPITAL) 136
WAMILIKI WA KAMPUNI (SHAREHOLDERS). 138
ARTICLES OF ASSOCIATION YA KAMPUNI. 139
VIPENGELE VYA KWENYE ARTICLES OF ASSOCIATIONS YA KAMPUNI 140
1. KUTENGENEZA VIPANDE VYA HISA (SHARE ALLOTMENT). 140
2. KAMPUNI KUTOA HISA (ISSUE SHARES) NA KUZIUZA (SUBSCRIBED SHARES). 141
3. HAKI ZA HISA (SHARE RIGHTS). 142
4. CHETI CHA HISA (SHARE CERTIFICATE). 143
5. KUSHIKILIA HISA (LIEN ON SHARES) 144
6. KUKUMBUSHIA MADENI YA HISA (CALLS ON SHARES). 145
7. MWANAHISA KUHAMISHA UMILIKI WA HISA KWA KUUZA (TRANSFER OF SHARES). 146
8. KUHAMISHA UMILIKI WA HISA KWA KURITHI (TRANSMISSION OF SHARES). 147
9. IDADI YA WAJUMBE KWENYE MKUTANO WA KAMPUNI (QUORUM). 150
10. KUFILISI HISA (FORFEIT OF SHARES) 151
11. MIKUTANO YA KAMPUNI 152
❖ **MKUTANO MKUU WA MWAKA (ANNUAL GENERAL MEETING).** 153
❖ **MKUTANO WA DHARURA (EXTRA ORDINARY MEETING).** 155

❖ **MKUTANO WA BODI YA WAKURUGENZI** 157
❖ **KODI YA MISHAHARA KWA WAFANYAKAZI (INCOME TAX).** 159
❖ **KODI YA GAWIO KWA WANAHISA (DIVIDEND TAX) (10%).** 160
❖ **KODI YA FAIDA YA KAMPUNI (CORPORATE TAX) (30%).** 161

SEHEMU YA SABA 165

7. MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA ZA KAMPUNI. 165

❖ **MAPATO YA KAMPUNI 165**

- **MAUZO YA BIDHAA NA HUDUMA ZA KAMPUNI.** 166
- **UDHAMINI (SPONSORSHIP).** 166
- **KAMPUNI KUUZA HISA.** 166
- **KAMPUNI KUUZA HATI FUNGANI.** 166
- **UWEKEZAJI WA KAMPUNI** 166

❖ **MATUMIZI YA KAMPUNI. 176**

- **Gharama za Kununua bidhaa** 176
- **Mishahara kwa wafanyakazi.** 176
- **Gawio la faida kwa wanahisa.** 176
- **Kodi kwa serikali.** 176

RIPOTI YA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA KAMPUNI 180

VIPENGELE VYA MUHIMU KWENYE RIPOTI YA MAPATO NA MATUMIZI YA KAMPUNI (PROFIT AND LOSS ACCOUNT)..... 181

- **MAUZO (SALES)** 181
- **GHARAMA ZA BIDHAA ZILIZOUZWA (COST OF GOODS SOLD)** 181
- **FAIDA YA AWALI (GROSS PROFIT)** 182

- **GHARAMA ZA UENDESHAJI BIASHARA**..... 182
- **FAIDA KABLA YA KODI (PROFIT BEFORE TAX - P.B.T)**..... 183
- **KODI YA KAMPUNI (30%).**..... 183
- **FAIDA HALISI BAADA YA KODI (NET PROFIT).** 183
- **GAWIO LA FAIDA (DIVIDEND).**..... 184
- **FAIDA ILIYORUDI KWENYE KAMPUNI (RETAINED EARNINGS).**..... 184

VIPENGELE VYA (BALANCE SHEET) 188

MALI ZA KAMPUNI (COMPANY ASSETS)..... 188

- ❖ **Mali za Muda Mfupi kwenye kampuni (Current Assets).** 188
- ❖ **Mali za muda mrefu kwenye kampuni (Non-Current Assets).** 189

❖ **MADENI YA KAMPUNI (LIABILITIES). 190**

DIBAJI

Kumekuwa na tatizo kubwa sana la watu wengi kupata fedha nyingi, ila baada ya muda fulani fedha zile huisha ghafla bila muhusika kufanya jambo la msingi. Fedha huwa zinaisha ghafla kwasababu mtu husika anakuwa hajawekeza kipato chake.

Ili fedha iweze kudumu kwa muhusika na kuongezeka, fedha inatakiwa kuhifadhiwa na kuwekezwa kwenye miradi mbalimbali ambayo itamletea faida stahiki mwekezaji. Moja ya uwekezaji mzuri ni kwa mfanyabiashara yoyote yule kuwekeza kwenye Kampuni.

Kitabu hiki cha **KAMPUNI NI DHAHABU** kinafundisha hatua kwa hatua jinsi ya Kusajili, kuanzisha na kuendesha kampuni kwa faida. Ufunguaji wa kampuni ni moja ya njia salama za kuwekeza fedha. Kitabu hiki pia kitakufundisha njia za kuhifadhi fedha baada ya kupata faida kwenye Kampuni husika kwa kuwekeza faida ya kampuni kwenye miradi mingine mipya ambayo italeta faida endelevu kwenye kampuni husika.

Baada ya kusoma kitabu hiki cha **KAMPUNI NI DHAHABU** mhusika atakuwa amepata uelewa wa aina

mbalimbali za mifumo ya kuingia kwenye biashara pamoja na kujifunza njia tofauti za kuwekeza fedha, kama kununua **Hisa** na kuwekeza kwenye **Hatifungani.**

SEHEMU YA KWANZA

❖

1. MIUNDO YA BIASHARA

Kwasasa **Tanzania** kuna muamko mkubwa wa watu mbalimbali kuwa na matamanio ya kuanzisha biashara tofauti. Lakini changamoto kubwa huja kwenye kuchagua muundo sahihi wa kufanya biashara husika. Kwa mfano, biashara moja ya kuuza **chakula**, inaweza kufanywa katika miundo tofauti.

Kwanza, mtu anaweza kuanzisha biashara ya chakula kama mtu binafsi **(Sole-Proprietor).** Akafungua **Mgahawa wa Chakula** kwa kutumia fedha zake binafsi na mtu huyo mmoja tu akawa ndio mmiliki wa mgahawa husika. Au watu wawili au zaidi wanaweza kuamua kuungana na kuchanga mitaji kwa malengo ya kuanzisha kwa pamoja **Mgahawa wa chakula** kwa mfumo wa ushirikiano **(Partnership).** Au watu wawili na kuendelea wanaweza **Kusajili Kampuni** ambayo itakuwa inajihusisha na uzalishaji na uuzaji wa mazao mbalimbali.

Pia mfanyabiashara yoyote anaweza kutoa **kibali cha kibiashara** kwa watu wengine kufungua **migahawa mikubwa ya chakula** au biashara yoyote ile katika Nchi mbalimbali, kwa **Majina ya Kibiashara** ya mfanyabiashara husika na kuruhusu **Nembo/Logo** zake zitumike pia kibiashara kwa makubaliano ya Malipo fulani **(Royalty Fee).**

Miundo hii tofauti ya biashara, ina tofautiana kwenye **kiasi cha mtaji** kinachohitajika kuianzisha, **Ulipaji wa Kodi**, **Idadi ya Wamiliki** na **Ukomo wa Madai** endapo biashara husika itafilisika. Ni muhimu kila mfanyabiashara anaetaka kuingia kwenye biashara fulani, kwanza aelewe miundo mbalimbali ya biashara, kabla ya kuchagua muundo fulani wa biashara.

Mfanyabiashara makini anatakiwa kuelewa faida na hasara za kila muundo wa biashara kabla ya **kuwekeza fedha** zake kwenye biashara yoyote ile. Hii ni njia pekee ambayo itamhakikishia usalama wa fedha zake mfanyabiashara husika anaetaka kuwekeza fedha kwenye biashara.

Baadhi ya miundo ya biashara ni ifuatayo.

- **Biashara ya mtu mmoja (Sole-proprietor)**
- **Biashara ya ushirikiano (Partnership)**
- **Kampuni (Kampuni binafsi na kampuni ya Umma)**
- **Ubia (Joint venture)**
- **Franchise**

BIASHARA YA MTU MMOJA (SOLE-PROPRIETOR).

Hii ni biashara ambayo inaanzishwa na kumilikiwa na mtu mmoja tu. **Mtu mmoja** tu ndio anahusika kwenye **Kuwekeza Mtaji** wake kwa ajili ya kuanzisha biashara binafsi ya mtu mmoja. Faida ya biashara binafsi ni kwamba ni **rahisi kuanzisha**, **haihitaji mtaji mkubwa** kuanzisha biashara ya mtu mmoja, na hata maamuzi ya uwekezaji kwenye biashara hii huwa ni ya haraka maana anaeamua ni huyo huyo mtu mmoja pekee yake mwenye biashara.

Biashara ya Mtu Mmoja ina hasara zake pia. **Hasara za biashara ya mtu mmoja** ni, endapo biashara husika **itafilisika** na mwenye biashara alikuwa anadaiwa wakati biashara yake inafilisika, basi mpaka **Mali Binafsi** za mwenye biashara binafsi zitauzwa ili kufidia deni la kwenye biashara husika ya mtu mmoja.

Hasara nyingine ya biashara ya mtu mmoja ni **usimamizi mbovu wa fedha**. Kwakuwa mmiliki ndio huyo huyo, ni rahisi **mauzo ya biashara** kuyachukua bila kuandika kwenye daftari la mauzo na kutumia fedha hizo kwa matumizi binafsi. Ndio maana biashara nyingi zinazomilikiwa na mtu mmoja ni vigumu sana kukua na kutanuka na kuwa kubwa zaidi. Wafanyabiashara wachache

sana binafsi ambao wana **nidhamu ya fedha** ya biashara ndio huwa wananufaika kwenye huu mfumo wa biashara ya mtu mmoja.

Hasara nyingine ya biashara ya mtu mmoja ni, siyo rahisi **Kupata Mtaji** wa ziada wa fedha endapo mmiliki wa biashara husika atakwama kwenye fedha. Biashara ya mtu mmoja kukopeshwa fedha nyingi huwa ni vigumu sana. Mara nyingi biashara za mtu mmoja hukopeshwa kiasi kidogo sana cha fedha, ambacho muda mwingine hakitoshi kukuza biashara husika. Matokeo yake, baada ya muda fulani biashara husika ya mtu mmoja inaweza kufilisika kwa **kukosa mtaji imara** wa kuendesha biashara husika ya mtu mmoja.

Hasara nyingine ya biashara ya mtu mmoja ni, endapo mmiliki wa biashara ya **mtu mmoja akafariki** basi na biashara husika hufa. Kwakuwa biashara ilikuwa inamilikiwa na mtu mmoja tu, kuanzia kwenye usajili wake mpaka uendeshaji wake. Hivyo ni vigumu mtu mwingine kuendeleza biashara husika, kama alikuwa hafahamu namna biashara husika ya mtu mmoja ilivyokuwa inaendeshwa.

KUSAJILI JINA LA BIASHARA YA MTU MMOJA (SOLE-PROPRIETOR REGISTRATION).

Mtu mmoja anaemiliki biashara pekee yake anaweza kusajili jina la biashara husika kisheria. Mamlaka inayohusika na kusajili majina ya biashara Tanzania ni **BRELA (Business Registration and Licence Agency).** Mwenye biashara anatakiwa kutunga jina lenye utofauti na majina ya wafanyabiashara wengine ambao tayari wameshasajili majina ya biashara zao.

Mmiliki wa biashara haruhusiwi kusajili jina la biashara ambalo tayari limeshasajiliwa na mtu mwingine **BRELA**. Ili mtu husika ajihakikishie kwamba jina analotaka kulitumia kwenye biashara husika halijasajiliwa, anatakiwa kuingia kwenye tovuti ya **BRELA**, na kwenda eneo la **(free business name search),** kisha aandike jina la biashara husika ambayo anataka kuisajili.

Kama jina husika litakuwa tayari limeshasajiliwa, litatokea jina la biashara husika pamoja na majina ya mtu aliyesajili jina husika la biashara yataonekana kwenye tovuti ya BRELA. Kama jina husika la biashara halijasajiliwa, taarifa ya **(not found)** itatokea. Hii itamjulisha mtu husika

anaetaka kusajili jina la biashara kwamba, jina hilo halijasajiliwa hivyo anaweza kulisajili.

Huwa kuna ada ya kusajili jina la biashara. Kwenye tovuti ya **BRELA,** mtu husika anaetaka kusajili jina la biashara ataelekezwa namna ya kulisajili jina la biashara na ada ya kulipia ni kiasi gani. Ili mtu yoyote aweze kusajili jina la biashara **Tanzania** anatakiwa kuwa na vitu vifuatavyo,

- **TIN (Tax Identification Number) ya mmiliki wa biashara**
- **Kitambulisho cha Taifa cha mmiliki wa biashara husika**
- **Jina la biashara husika**
- **Shughuli kuu za biashara husika**
- **Anuani ya eneo la biashara na anuani ya makazi ya mwenye biashara husika.**

Baada ya mmiliki kuwa na vitu tajwa hapo juu, atafungua akaunti kwenye tovuti ya **BRELA**, na kufuata maelekezo ambayo ataambiwa kwenye tovuti. Baada ya kukamilisha taarifa zote muhimu mtu husika atapewa risiti ambayo ina namba za malipo ya ada ya kusajili jina la biashara.

Mfanyabiashara husika atalipia ada husika kupitia control number ambayo atatumiwa.

Baada ya kulipa ada husika, siku kadha mbele, mwenye biashara atapatiwa vyeti viwili ambavyo ni, **Certificate of Registration** pamoja na **Extract from the Register.** Vyeti hivi viwili ndio vinathibitisha kwamba jina husika la biashara limeshasajiliwa na **BRELA.**

Mfanyabiashara anaruhusiwa kusajili shughuli **nne (4)** tu za biashara tofauti kupitia jina moja la biashara ya mtu mmoja **(sole-proprietor).** Na mfanyabiashara husika atatakiwa kufanya zile biashara tu ambazo ameziorodhesha kwenye cheti chake cha usajili wa jina la biashara husika tu.

****

BIASHARA YA USHIRIKIANO (PARTNERSHIP).

Hii ni biashara ambayo inamilikiwa na zaidi ya mtu mmoja yani kuanzia watu wawili na mwisho ni watu **ishirini (20).** Watu kadhaa wanaweza kuunganisha mitaji yao ya **fedha, mawazo** na **ujuzi** mbalimbali na kuanzisha biashara moja ya ushirikiano **(Partnership).** Biashara ya ushirikiano inatakiwa kusajiliwa kisheria na wamiliki wake watatengeneza katiba ya ushirikiano (**Partnership Deed**), ambayo itaelezea kila kitu kuhusu biashara husika ya ushirikiano.

Katiba ya biashara ya ushirikiano **(Partnership Deed),** itaelezea majina ya wamiliki wa biashara husika ya ushirikiano, aina ya biashara watakayofanya, mgawanyo wa majukumu yao, mgawanyo wa faida endapo itatokea utakuaje, na pia katiba ya biashara ya ushirikiano itaelezea endapo hasara itatokea nini kitafanyika na endapo mmoja wa wanabiashara ya ushirikiano akiamua kujiondoa au akafariki taratibu zipi hufuatwa.

Katiba ya biashara ya ushirikiano **(Partnership deed)** ni ya muhimu sana. Maana migogoro mingi kwenye biashara za ushirikiano hutokea kwasababu kuna baadhi ya vipengele

kwenye katiba ya ushirikiano haviku jadiliwa kabla ya watu husika kuingia kwenye biashara ya ushirikiano.

Chanzo kingine cha migogoro kwenye biashara ya ushirikiano ni, baadhi ya wajumbe hawakuelewa vizuri baadhi ya vipengele kwenye katiba ya biashara ya ushirikiano. Ni vyema **Mwanasheria** au mtu mwenye uzoefu wa biashara za ushirikiano ndio awaelekeze vipengele vyote vya muhimu watu husika wanaotaka kufanya biashara ya ushirikiano kabla ya kuwekeza fedha pamoja kwenye biashara husika ya ushirikiano.

Faida za biashara ya ushirikiano ni, mtaji mkubwa zaidi unaweza kupatikana wa kuendesha biashara ya ushirikiano kuliko biashara ya mtu mmoja. Faida nyingine ni mawazo ya wamiliki tofauti ambao wamewekeza fedha zao kwenye biashara ya ushirikiano hutolewa, hivyo jambo moja huongelewa kwa upana zaidi na kwa mawazo ya wengi zaidi.

Hasara za biashara ya ushirikiano ni migogoro inaweza kutokea endapo wamiliki wakatofautiana kwenye masuala mbalimbali ya kuendesha biashara husika ya ushirikiano. Kadri wamiliki wa ushirikiano wanavyozidi kuwa wengi ndivyo mgawanyo wa faida unavyozidi kuwa mdogo.

Na cha mwisho endapo biashara ya ushirikiano ikafilisika na ikawa na madeni ya biashara husika, mali binafsi za wamiliki wa biashara ya ushirikiano nazo zitauzwa ili kufidia deni ambalo biashara ya Ushirikiano husika inadaiwa.

*****

UBIA (JOINT VENTURE)

Ubia ni mfumo wa kuendesha biashara ambao unaundwa na watu wenye biashara tofauti au kampuni tofauti kuungana na kufanya mradi fulani kwa pamoja kwa kipindi fulani. Kampuni hizi tofauti zinaunganisha **mitaji ya fedha**, **maliasili watu, teknolojia** na maliasili zingine kwa ajili ya kufanya mradi husika kwa pamoja.

Baada ya mradi husika kumalizika kampuni hizi zilizoungana kwa Pamoja kama wabia, zina maamuzi ya kuendelea kuunganisha mitaji yao baada ya mradi husika kukamilika au wanaweza kusitisha muungano huu pale tu mradi husika utakapokuwa umekamilika na kugawana stahiki zao.

Mfumo wa kibiashara wa kuunganisha kampuni zaidi ya moja **(Joint Venture)** kufanya mradi fulani kwa pamoja, unatumika sana kama mradi husika ni mkubwa sana na kampuni moja pekee yake haiwezi kuufanya huu mradi pekee yake. Miradi mikubwa kama ya, **ujenzi wa barabara** ndefu, **ujenzi wa viwanja vya michezo,** kama **viwanja vya mpira wa miguu.** Huwa inahitaji fedha nyingi sana kufanya miradi mikubwa namna hii.

Hivyo kampuni mbili au zaidi za ujenzi zinaweza kuungana kwa pamoja **kisheria** kwa ajili ya kufanya mradi husika wa ujenzi. Baada ya mradi husika kukamilika na kampuni zilizoungana kulipwa stahiki zao na mwenye tenda. Kampuni husika zilizoungana watagawana kutokana na asilimia za uwekezaji kila kampuni iliyoweka kwenye mradi husika.

Baada ya hapo muungano huo unaweza kuvunjika kisheria. Au kama kuna miradi mingine inaendelea baada ya ule mradi wa awali kukamilika. Kampuni husika, zinaweza kuendeleza muungano wao kisheria mpaka pale watakapo kubaliana kuusitisha muungano huo.

*****

FRANCHISE

Ni mfumo wa kibiashara ambao unahusisha kampuni moja kuipa ruhusa kimkataba kampuni au mtu mwingine kutumia **Majina, Nembo, Logo, Fomula, Bidhaa** au **Ujuzi** wa kutengeneza bidhaa za **Kampuni Mama** kwa makubaliano maalumu ya kibiashara.

Kampuni Mama (Franchisor) ambayo inatoa ruhusa kwa kampuni nyingine **(Franchisee)** kutumia **Bidhaa zake**, **Fomula zake** au **Logo zake** kibiashara itakuwa inalipwa fedha fulani **(Royalty Fee),** kutokana na muda maalumu ambao kampuni nyingine itakavyotumia jina au bidhaa za kampuni mama iliyotoa idhini kibiashara.

Malipo yatakayolipwa **(Royalty Fee)** na kampuni inayotaka kutumia **Majina, Bidhaa** au **Ujuzi** wa kutengeneza bidhaa husika au vyote kwa pamoja vya kampuni mama, yanaweza kupangwa kabisa na hayata badilika hata kama kampuni inayotaka kutumia hivyo vitu kibiashara haitakuwa na uhakika wa kutengeneza faida.

Au malipo yanaweza kuwa kwa mfumo wa makubaliano ya **Asilimia (%)** ya mauzo ya bidhaa zenye **Nembo** na **majina ya Kampuni Mama**.

Kadri kampuni iliyoomba kibali **(Franchisee)** inavyouza bidhaa za kampuni mama **(Franchisor),** ndivyo inavyozidi kulipia fedha nyingi zaidi.

Kampuni nyingi, huwa zinapenda zilipe kabisa ada ya mwaka mzima ya kutumia huduma kama **(Majina, Nembo au Bidhaa)** za **Kampuni Mama.** Alafu kampuni iliyopewa idhini na leseni kibiashara na kampuni mama, itaweka mipango dhabiti jinsi ya kunufaika na idhini ambayo wamepewa ya kutumia kibiashara **Majina, Nembo**, **Bidhaa** na **huduma** za kampuni mama.

Kampuni Mama huwa inatoa masharti ya jinsi ya kutumia **jina lake** au **mbinu zake** za uzalishaji bidhaa kwa uangalifu na kuhakikisha kampuni au mtu anaetaka kutumia majina ya kampuni mama, wanazalisha bidhaa au huduma katika ubora ule ule ambao kampuni mama inazalisha. Mfano wa kampuni ambazo zinatumia mfumo wa franchise ni kama **Coca Cola** kwa upande wa **Vinywaji** na **Mc-Donalds** na **Sub-Ways** kwa upande wa **Migahawa ya Chakula**.

Hizi ni kampuni kubwa za **Kimarekani** na makao yake makuu yapo **Marekani.** Lakini kampuni hizi zina matawi yake karibia duniani kote. Na hawatumi maliasili zao kuwekeza kwenye hizi nchi zingine.

Wanachofanya ni kutoa **leseni ya kibiashara** ambayo inaruhusu kampuni nyingine kuzalisha bidhaa kama zao na kuita majina ya kampuni mama iliyotoa **leseni ya biashara** kutumia majina ya **Kampuni Mama.**

Kampuni Mama huwa inalipwa kiasi fulani cha ada **(Royalty fee),** kila mwaka. Baada ya hapo ikijiridhisha na mkataba na vipengele vyake huruhusu kimkataba kampuni nyingine kutumia **Majina** na **Fomula** zake za uzalishaji wa bidhaa na huduma zake.

Faida ya mfumo wa **Franchise** kibiashara ni kwamba, **Kampuni Mama** haihitaji kuingia gharama za **kufungua matawi mapya** kila nchi ili kuendesha shughuli zake. Hiyo ingemaanisha, wangeingia kwenye gharama kubwa za uendeshaji biashara kama, **kulipa mishahara wafanyakazi** kwenye kila nchi ambayo **wangefungua matawi** wenyewe, **kulipa kodi za serikali**, **kukata vibali** vya kufungua kampuni kwenye kila nchi ya kigeni na gharama zingine nyingi za kuendesha biashara kwenye nchi nyingine zingetokea.

Kuepuka gharama hizo zote kampuni nyingi kubwa, huwa zinatoa leseni kwa watu wengine wenye uwezo au

kampuni zingine zenye uwezo kwenye nchi husika kutumia majina ya kampuni mama kibiashara na kwa malipo fulani.

***

MIUNDO YA BIASHARA TOFAUTI NA SIFA ZAKE.

AINA YA BIASHARA	SIFA ZAKE	IDADI YA WAANZILISH
BIASHARA YA MTU MMOJA (SOLE PROPRIETOR)	• Inamilikiwa na mtu mmoja tu. • Mwenye biashara akifariki na biashara husika inakufa. • Biashara ya mtu mmoja ikifilisika mpaka mali binafsi za mwenye biashara zitahusishwa kwenye kulipa madeni.	Inaanzishwa na kumilikiwa na mtu mmoja tu.

	• Mwenye biashara anaweza kusajili jina la biashara ya mtu mmoja **(business name Registration)** husika kupitia mamlaka za **BRELA** na kupatiwa **Certificate Of Registration** pamoja na **Extract From The Register.**	
BIASHARA YA USHIRIKIANO (PARTNERSHIP)	• Watu wawili na zaidi, wanaunganisha mitaji yao kufanya biashara pamoja.	Wamiliki ni kuanzia watu wawili mwisho watu ishirini tu.

	• Wamiliki wa biashara ya ushirikiano Wataanda katiba ya ushirikiano inayoitwa **Partnership Deed.** • Mmoja wa wamiliki wa biashara ya ushirikiano akifilisika au akifariki biashara ya ushirikiano hufa pia.	**(wamiliki 2 – 20)**

	• Ikitokea biashara ya ushirikiano husika ikafilisika mpaka mali binafsi za wamiliki zitahisishwa kwenye kulipa madeni ya biashara husika ya ushirikiano. • Wamiliki wa biashara ya ushirikiano watagawana faida ya biashara husika kutokana na kiasi cha uwekezaji kila mmiliki alichowekeza.	

KAMPUNI BINAFSI	Hairuhusiwi kuuza hisa zake kwenye soko la hisa.	**Wamiliki 2 – 50**
KAMPUNI YA UMMA	Inaruhusiwa kuuza hisa zake kwenye soko la hisa.	**Wamiliki 2 – haina Ukomo wa umiliki wake.**
UBIA (JOINT VENTURE)	Watu au kampuni mbili na zaidi, zinaungana na kufanya mradi fulani kwa pamoja kwa makubaliano maalumu kwa kipindi fulani.	**Watu / kampuni mbili (2) na zaidi.**
FRANCHISE	Ni kitendo cha kutumia **Majina, Logo, Fomula za Uzalishaji au Bidhaa** za kampuni nyingine kwa makubaliano maalumu ya kibiashara kwa malipo **(Royalty Fee).**	**Franchisor na Franchisee**

"Mifumo ya kuendesha biashara ipo mingi,
Mtu Mmoja anaweza kufanya biashara pekee yake kama (Sole-proprietor)".
"Au watu kadhaa wanaweza kuungana na kufanya biashara ya ushirikiano kwa pamoja (Partnership")
.
"Au watu kuanzia wawili (2) na kuendelea wanaweza kuungana na kutengeneza kampuni moja (Private / Public Company)."
***"Au mfanyabiashara/ kampuni mama inaweza kutoa idhini ya* kutumia Majina, Logo, Fomula za Uzalishaji au Bidhaa zake kwa makubaliano ya kibiashara kwa kutumia mfumo wa (Franchisee)."**

"Mfanyabiashara anatakiwa kuwa makini kuchagua mfumo sahihi wa kuingia kwenye biashara.
Maana kila mfumo wa biashara una faida na hasara zake."

SEHEMU YA PILI

❖

2. JINSI YA KUANZISHA KAMPUNI.

Kampuni ni nini?

Kampuni ni muunganiko wa watu wawili au zaidi ambao wana lengo moja la kufanya shughuli fulani au mradi fulani wa pamoja ambao utasajiliwa kisheria. Ili kampuni yoyote iweze kufanya shughuli zake, ni lazima kwanza isajiliwe kisheria na mamlaka husika ya kusajili kampuni kwenye nchi husika.

Kwa **Tanzania,** mamlaka ya kusajili kampuni yapo chini ya **BRELA (Business Registration and Licence Agency).** Baada ya kampuni husika kusajiliwa itapewa cheti cha kampuni husika (**Certificate of Incorporation).**

Shughuli za kampuni zinaweza kusajiliwa kufanya shughuli za kibiashara, Kama kuzalisha bidhaa au huduma fulani na kuziuza kwa wateja. Au kampuni inaweza kusajiliwa kufanya shughuli zisizo za kibiashara ila shughuli za misaada tu.

Wamiliki wapya wa kampuni watatakiwa kuanda Waraka na katiba ya kampuni husika (**Memorandum and Articles of Association).**

Waraka na Katiba ya kampuni **(MEMARTS)** itaelezea, **jina la kampuni** mpya husika, **shughuli zote** ambazo kampuni husika itategemea kuzifanya, **Makao Makuu** ya kampuni husika, pamoja na **Mtaji Wa Jumla** ambao kampuni husika inategemea kuanza nao.

****

AINA ZA KAMPUNI

Kuna aina tofauti za kampuni ambazo mtu yoyote mwenye vigezo stahiki anaweza kuanzisha. Utofauti huo wa kampuni upo kwenye **kiwango cha chini** cha waanzilishi wa kampuni husika, **idadi ya wakurugenzi** wanaotakiwa kuwepo ili kuanzisha kampuni husika. Pamoja na **ukomo wa madai (Limited Or Unlimited Liability),** endapo kampuni husika itafilisika.

KAMPUNI KUTOKANA NA UMILIKI.

kampuni zinatofautiana kutokana na vitu tofauti tofauti. kuna kampuni zina tofautiana kutokana na aina ya umiliki wa kampuni husika. Hapo kuna kampuni zinasajiliwa kama **Kampuni Binafsi** na kuna kampuni zinasajiliwa kama **kampuni za Umma**.

KAMPUNI BINAFSI (PRIVATE COMPANY).

Kampuni binafsi, ni kampuni ambayo wamiliki wake wanaanzia **wawili (2)** na mwisho wa idadi ya wamiliki wa kampuni binafsi ni **Hamsini (50)** tu. Kampuni binafsi haiwezi kuuza hisa zake kwenye **soko la hisa.** Mtaji wa kuanzisha na kuendesha **kampuni binafsi** huwa unachangishwa na **wanahisa** tu ambao wanaunda kampuni binafsi husika. Kampuni nyingi binafsi huwa ni zile **kampuni za kifamilia** au zinaundwa na watu wanaofahamiana.

Kiwango cha chini cha **wakurugenzi** wanaotakiwa kuendesha shughuli mbalimbali za kampuni binafsi kinaanzia, mkurugenzi mmoja (1) na Kiwango cha mwisho cha wakurugenzi kwenye kampuni binafsi ni **wakurugenzi nane (8)** tu.

Siyo lazima wamiliki wa **kampuni binafsi** husika ndio wawe wakurugenzi wa kampuni hiyo. Wamiliki wa kampuni husika wanaweza kuajiri watu wenye taaluma husika wawe wakurugenzi kwenye kampuni. **Wakurugenzi** hao wa kuajiriwa watakuwa na majukumu ya kuendesha shughuli za kila siku kwenye kampuni husika na watakuwa wanalipwa mishahara na wamiliki wa kampuni husika.

Au wamiliki wa kampuni binafsi husika, wanaweza kuamua wao wenyewe ndio wawe wakurugenzi na wamiliki wa kampuni husika na watakuwa wanaendesha na kusimamia shughuli za kila siku kwenye kampuni husika.

***

KAMPUNI YA UMMA (PUBLIC COMPANY)

Kampuni ya Umma, ni kampuni ambayo inaweza kuwekwa kwenye **soko la hisa** kwa ajili ya kuuza hisa zake kwa jamii. **Kampuni ya Umma** inaruhusu jamii kununua hisa zake kutokana na uwezo wa mwanahisa na idadi ya hisa zitakazo ruhusiwa kuuzwa katika **soko la hisa** na kampuni husika ya **Umma.**

Kwa **Tanzania** soko la hisa lipo chini ya **Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA).**

Hii ni taasisi ya serikali chini ya **Wizara ya Fedha** ambayo imepewa mamlaka ya kusimamia na kuendeleza masoko ya mitaji Tanzania. Kwasasa Tanzania ina soko moja tu la hisa, ambalo lipo **Dar es salaam** na linatambulika kwa majina ya **Dar es salaam Stock Exchange Market (D.S.E).**

Kiwango cha chini cha wanahisa kuanzisha kampuni ya **Umma**, inaanzia wanahisa **wawili (2)** na hakuna kiwango cha kikomo kwa wanahisa kumiliki kampuni ya umma. Idadi ya chini ya wakurugenzi kwenye kampuni ya Umma ni kuanzia **wakurugenzi watatu (3).**

Hawa wakurugenzi kwa pamoja wanaunda **bodi ya wakurugenzi** wa kampuni ya umma. Bodi hii ya wakurugenzi ndio inawakilisha wanahisa wengine wa kampuni husika kwenye uendeshaji wa shughuli za kila siku kwenye kampuni husika.

KAMPUNI BINAFSI KUWA YA UMMA (I.P.O)

Kampuni binafsi inaweza kubadilika na kuwa kampuni ya umma kwa kubadilishwa katiba yake **(Amendment of The Memorandum & articles of associations)**. Kampuni inayotaka kuwa ya umma inatakiwa kupewa idhini na mamlaka ya usimamizi wa mitaji katika nchi husika kwanza. Baada ya mamlaka ya mitaji ya nchi husika kupitisha ombi la Kampuni husika binafsi au kampuni mpya kabisa inayotaka kuwa ya umma.

kampuni husika itatakiwa kutoa ofa ya awali **(Initial Public Offering – I.P.O)** ya kutangaza kuwa inadhamiria kuwa kampuni ya umma ambayo itaruhusu watu wa umma kununua hisa zake.

Hisa zitaanza kuuzwa kwenye soko la awali **(Primary market)** kwa kampuni mpya ya umma kuuza hisa zake kwa umma moja kwa moja.

Baada ya hapo kampuni husika ya umma hisa zake zitakuwa zinauzwa kwenye soko la pili la hisa **(secondary market)** kwa kutumia mawakala wa kuuza hisa **(brokers).** Hapo mtu au mwekezaji akihitaji kununua hisa atapitia kwa mawakala hao.

****

KAMPUNI KUTOKANA NA UTAIFA

Kampuni pia zimegawanywa kutokana na uraia wa wamiliki na nchi ambayo wamiliki watafungua kampuni husika. Kampuni kutokana na utaifa au uraia zimegawanyika katika makundi yafuatayo,

- **KAMPUNI YA SERIKALI**
- **KAMPUNI YA WAZAWA**
- **KAMPUNI YA KIGENI**

KAMPUNI YA SERIKALI (STATE/GOVERNMENT OWNED COMPANY).

Kampuni ya serikali, ni kampuni ambayo (**asilimia 51%)** ya hisa za kampuni husika zinamilikiwa na **Serikali. Kampuni za serikali** zinasajiliwa ndani ya nchi husika kwa malengo ya kufanya shughuli za kiserikali au za kibiashara.

lakini zikisimamiwa na serikali au watu wengine lakini serikali ndio inakuwa na umiliki mkubwa wa hisa za kampuni husika. Serikali inaweza kumiliki kampuni kadhaa kama njia ya kujiongezea kipato cha kuendesha bajeti yake ya kila mwaka kwenye nchi husika.

KAMPUNI YA KIGENI (FOREIGN COMPANY).

Kampuni ya kigeni, ni kampuni ambayo imesajiliwa nje ya nchi husika lakini inafanya shughuli zake ndani ya nchi nyingine. Mfano, kampuni itakuwa ni ya kigeni kama imesajiliwa nje ya **Tanzania** lakini inafanya shughuli zake ndani ya **Tanzania.**

Pia, Kampuni inakuwa ya kigeni kama asilimia zaidi ya **51%** ya hisa zitamilikiwa na **raia wa kigeni.** Mara nyingi **kampuni za kigeni** huwa ni **kampuni za kimataifa** ambazo zinawekeza kwenye nchi nyingi tofauti tofauti kwa kufungua matawi **(Branches)** kuziwakilisha kampuni mama. Mfano wa kampuni za kimataifa duniani ni kama kampuni za **Coca-Cola, Pepsi, Sony, Adidas.** Hizi ni kampuni ambazo zina matawi sehemu kubwa duniani.

KAMPUNI YA WAZAWA (LOCAL COMPANY).

Hizi ni kampuni ambazo zimesajiliwa ndani ya nchi husika kwa malengo ya kufanya shughuli zake ndani ya nchi hiyo hiyo. Mfano, kampuni isajiliwe ndani ya **Tanzania** na ifanye shughuli zake ndani ya **Tanzania.** Kampuni inakuwa ya wazawa kama asilimia zaidi ya **(51%)** ya hisa zake zinamilikiwa na wazawa.

KAMPUNI KUTOKANA NA UKOMO WA MADAI.

- KAMPUNI YENYE UKOMO WA MADAI **(LIMITED COMPANY).**
- KAMPUNI ISIYO NA UKOMO WA MADAI **(UNLIMITED COMPANY).**

KAMPUNI YENYE UKOMO WA MADAI (A LIMITED COMPANY).

Kampuni zenye ukomo wa madai **(limited Companies)**, ni zile kampuni ambazo madai yake yanaishia kwenye mali za kampuni tu. Endapo kampuni husika yenye ukomo wa madai itafilisika.

Mali binafsi za wanahisa haziwezi kuguswa. Mali za kampuni tu yenye ukomo wa madai ndio zitafilisiwa.

Hii inatoa ulinzi wa mali binafsi za wanahisa wanaomiliki kampuni yenye ukomo wa madai.

Kuna aina kuu mbili za kampuni zenye ukomo wa madai.

- **UKOMO WA HISA (LIMITED BY SHARES)**
- **UKOMO WA DHAMANA (LIMITED BY GUARANTEE)**

KAMPUNI YENYE UKOMO WA MADAI WA HISA (A COMPANY LIMITED BY SHARES).

Kampuni yenye ukomo wa madai wa hisa **(Company limited by shares),** ni ile kampuni ambayo katiba yake imeeleza kuwa kampuni husika itakuwa yenye ukomo wa madai ya hisa zake. Maana yake ni kwamba, endapo kampuni yenye ukomo wa hisa itakuwa na madeni, wanahisa watatakiwa kuchangia kile kiasi cha deni kinachodaiwa kutokana na idadi au ukomo wa hisa zao tu ndani ya kampuni husika. Ni fedha na mali ambazo zinamilikiwa na kampuni kwa mfumo wa hisa tu ndio zitahusika kulipia madeni yoyote ambayo kampuni husika yenye ukomo wa hisa itakuwa inadaiwa.

Kwa upande wa **faida ya kampuni**. Kama kampuni yenye **ukomo wa hisa** itatengeneza faida fulani. Wale wanaomiliki hisa za kampuni husika ndio watapata **gawio la faida.** Na **Mwanahisa** mwenye hisa nyingi zaidi ndiye atakaepata gawio kubwa kutokana na asilimia za umiliki wake wa hisa kwenye kampuni husika yenye **Ukomo wa Hisa.**

Kampuni yenye ukomo wa madai ya hisa zake, wanahisa wake huwa wanachangia fedha kwa mfumo wa **kununua hisa** za kampuni husika. Ili kampuni iendele kufanya shughuli zake. **Kampuni** inaweza kutangaza ofa ya kuuza hisa zake kwenye soko la hisa kama ni kampuni ya Umma. Watu mbalimbali wenye fedha na nia ya kuwekeza fedha zao wataenda **kununua hisa za kampuni** husika kwenye **soko la hisa** kutokana na thamani ya kila kipande kimoja cha hisa sokoni. Sehemu kubwa ya kuongeza mtaji kwenye kampuni yenye ukomo wa hisa, ni kwa wanahisa kununua hisa nyingi zaidi ambazo kampuni husika itakuwa imezitoa **(Issued shares).**

****

KAMPUNI YENYE UKOMO WA DHAMANA (A COMPANY LIMITED BY GUARANTEE).

Kampuni zenye ukomo wa dhamana, ni kampuni ambazo katiba yake inasema kwamba ni kampuni zenye ukomo wa dhamana. Kampuni zenye ukomo wa dhamana, zina sajiliwa na kuendeshwa kama taasisi zisizokuwa na umiliki wa hisa, ila mtaji wake ni dhamana tu kwa wamiliki wake. Kampuni zenye ukomo wa dhamana huwa

zinategemea **misaada** na **wafadhali** kama njia ya kuendesha shughuli zake za kampuni.

Mara nyingi **kampuni zenye ukomo wa dhamana** huwa hazianzishwi kwa malengo ya kibiashara. Kampuni zenye ukomo wa dhamana, huwa zinaanzishwa kwa malengo ya **kusaidia jamii** na kutoa **misaada kwa jamii**. Mfano wa kamapuni zenye ukomo wa dhamana ni kama mashirika yasiyo ya kiserikali ya kutoa misaada **(NGO'S) NON-GOVERNMENT ORGANIZATIONS.**

***

KAMPUNI ISIYO NA UKOMO WA MADAI (UNLIMITED COMPANY).

Hizi ni kampuni ambazo wanahisa wake hawana ukomo wa madai endapo kampuni husika itakuwa imekumbwa na madeni. Maana yake ni kwamba, Kampuni **isiyo na ukomo wa madai (UNLIMITED COMPANY)** ikikumbwa na **madeni,** mpaka mali binafsi za wanahisa na wamiliki wa kampuni husika huwa zinaguswa na kujumuishwa kwenye kulipa madeni ya kampuni husika.

Mfumo huu wa umiliki haushauriwi kwa mtu yoyote anaetaka kufungua kampuni kuutumia. Kwasababu kuna hatari ya wamiliki wa kampuni husika kufilisiwa hadi mali zao binafsi endapo itatokea kampuni husika ikafilisika.

***

SIFA ZA KAMPUNI TOFAUTI.

NO:	AINA YA KAMPUNI	SIFA ZAKE	IDADI YA WANAHISA
1.	Kampuni Binafsi **(Private Company)**	❖ Haiuzi hisa zake kwenye soko la hisa.	Wanahisa 2 - 50
2.	Kampuni ya Umma **(Public Company)**	❖ Inauza na kununua hisa kwenye soko la hisa.	Wanahisa 2 - hamna Ukomo.
3.	Kampuni ya Serikali. **(State-owned Company)**	❖ Serikali inamiliki hisa zaidi ya asilimia 51%	Asilimia 51% inamilikiwa na serikali.

4.	Kampuni ya Wazawa **(Local Company)**	❖ Imesajiliwa ndani ya nchi kufanya shuguli zake ndani ya nchi husika. • Asilimia zaidi ya **51%** ya hisa zake zinamilikiwa na wazawa.	**Asilimia 51% ya wamiliki ni wazawa.**
5.	Kampuni ya Kigeni **(Foreign Company)**	❖ Imesajiliwa nchi nyingine lakini inafanya shughuli zake ndani ya nchi nyingine. ❖ Asilimia zaidi ya 51% ya hisa zake zinamilikiwa na wageni.	**Asilimia 51% ya wamiliki ni wageni.**
6.	Kampuni yenye ukomo wa madai. **(Limited Company).**	❖ Endapo kampuni itafilisika ni mali za kampuni tu ndiyo zitafilisiwa kwa ajili ya kulipa madeni.	

7.	Kampuni isiyo na ukomo wa madai. **(Unlimited Company).**	❖ Endapo kampuni itafilisika. Mpaka mali binafsi za wamiliki zitafilisiwa ili kulipa madeni ya kampuni.	
8.	Kampuni yenye ukomo wa hisa (**Company Limited by Shares)**	❖ Inaendeshwa kwa mfumo wa hisa. ❖ Kampuni ikitaka kuongeza mtaji wake, itauza hisa mpya kwa wanahisa wa kampuni husika. ❖ Na kwa wawekezaji wa nje watakaotaka kumiliki hisa za kampuni husika.	
9.	Kampuni yenye ukomo wa Dhamana. **(A Company Limited by Guarantee).**	• Haziendeshwi kwa mfumo wa hisa. • Zinaendehswa kwa mfumo wa ufadhili na misaada. **(NGO'S).**	

****

JINSI YA KUSAJILI KAMPUNI.

kwasasa kuna muamko mkubwa wa watu kutaka kumiliki kampuni zao binafsi. Hili swala ni zuri sana, maana maendeleo ya nchi yoyote yanatokana na uzalishaji wa bidhaa na huduma katika mfumo rasmi ambao unatambulika kisheria. **Kampuni** ni mfumo mzuri zaidi wa kuendesha biashara kisasa zaidi. Na kama **Kampuni** husika itasimamiwa vizuri inaweza kukua na kutengeneza faida kubwa sana.

Kwa mujibu wa **katiba ya Tanzania**, kila Mtanzania ana haki ya kuanzisha kampuni. Iwe ni **Kampuni binafsi** au **kampuni ya Umma**. Anachotakiwa mtu husika ni kukidhi vigezo na masharti ambayo yamewekwa kwa mtu anaetaka kufungua kampuni ndani ya **Tanzania.**

VITU VYA KUWA NAVYO WAKATI UNATAKA KUANZISHA KAMPUNI.

1. Kitambulisho cha Taifa kwa kila mmiliki.

2. Wamiliki wawe na umri kuanzia **miaka 18** na kuendelea.

3. Wamiliki wa kampuni wanatakiwa **kuanzia wawili (2)** na kuendelea.

4. TIN namba ya kila mmiliki.

5. Anuani ya makazi ya kila mmiliki.

6. Mchanganuo wa biashara unayotaka kufanya.

7. Eneo la biashara.

8. **Jina la biashara** lililosajiliwa Brela.

9. Memorandum & Articles of Associations.
iliyothibitishwa na Mwanasheria.

USAJILI WA KAMPUNI.

Hatua ya kwanza, wanaohitaji kuanzisha kampuni Tanzania wanatakiwa kuwa na,

- **kitambulisho cha taifa kila mmiliki mpya**
- **TIN namba binafsi kila mmiliki mpya**
- **Anuani ya makazi ya kila mmiliki mpya**
- **Barua ya utambulisho wa makazi ya kila mmiliki mpya kutoka serikali za mtaa**

Hivi vitu vyote wanatakiwa kuwa navyo kuanzia wamiliki wawili na kuendelea wa kampuni husika inayotaka kufunguliwa.

Baada ya wamiliki wote wapya kuwa na **TIN binafsi, vitambulisho vya taifa** kwa kila mmiliki na barua ya utambulisho kutoka serikali za mtaa wanapoishi. Watatafuta mwanasheria ambae amethibitishwa na mwenyewe muhuri wa mwanasheria. **Mwanasheria** husika awandalie **Memorandum na Articles of Association** kisha agonge muhuri wa mwanasheria kwenye Memorandum baada ya taarifa zote muhimu kukamilika.

Memorandum & Articles of Association, ni dokumenti ambayo inaelezea muundo wa kampuni husika utakavyokuwa, shughuli zote za kampuni zitakuwa ni zipi, idadi ya wanahisa watakuwa wangapi? Kiwango cha mtaji ambacho kitawekezwa na kila mwanahisa, haki za kila mwanahisa na mgawanyo wa faida na hasara utakuaje kwenye kampuni husika endapo itatokea hivo.

Baada ya hapo, waanzilishi wa kampuni mpya watapeleka kwenye ofisi za Brela, **Memorandum na Articles of Association** iliyogongwa muhuri wa mwanasheria. **Memorandum** husika iwe imeorodhesha na majina ya wamiliki wote wapya pamoja na idadi ya hisa ambazo watamiliki kwenye kampuni husika pamoja na saini za wamiliki wa kampuni mpya husika.

****

BRELA ONLINE REGISTRATION

Siku hizi kuna maboresho ya teknolojia, unaweza kutuma taarifa za kampuni mpya inayotaka kufunguliwa online kupitia mtandao wa BRELA unaoitwa **ONLINE REGISTRATION SYSTEM (O.R.S).** Mmiliki mpya wa kampuni utaingia kwenye tovuti rasmi ya **BRELA,** kisha utapata maelekezo yote ya jinsi ya kuingiza taarifa za

kampuni mpya kwenye tovuti ya **BRELA** kupitia mfumo wa **(O.R.S)**.

Baada ya kuingiza taarifa zote muhimu kwenye tovuti ya **BRELA** ikiwemo na kutuma nakala kivuli ya **Memorandum na Articles of Association** husika. **BRELA** watapitia vielelezo vyenu vyote ili kuona kama havitakuwa na mapungufu yoyote.

Kama taarifa zote zitakuwa zipo sahihi. **BRELA** watawapa fomu yenye maelekezo ya kulipia gharama za kufungua kampuni kutokana na mtaji ambao wamiliki husika wataanza nao kwenye kampuni husika. Baada ya kulipia gharama zote stahiki, **BRELA** watatoa cheti cha **CERTIFICATE OF INCORPORATION** kwa wamiliki wapya wa kampuni husika. Cheti hiki ndiyo kitakuwa ni uthibitisho kwamba kampuni husika imesajiliwa kisheria.

Baada ya hapo utatafuta mtaalamu wa biashara na masoko au mhasibu ili akuandalie **Mchanganuo Wa Biashara** wenye makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka husika wa fedha.

MCHANGANUO WA BIASHARA

Mchanganuo wa biashara, ni dokumenti ambayo inaelezea kwa upana na kitaalamu zaidi, kampuni husika inategemea kufanya biashara gani? Kampuni husika inategemea kuzalisha bidhaa au huduma zipi? Kampuni husika inategemea kupata mapato kiasi gani kwa mwezi na kwa mwaka? kutokana na mauzo ya bidhaa au huduma inazotegemea kuuza kwa wateja.

Pia **Mchanganuo wa biashara** utaelezea gharama zote ambazo kampuni husika itakuwa inaingia kila mwezi wakati inafanaya shughuli zake za biashara. Mwisho **Mchanganuo wa biashara** utaonyesha faida ambayo kampuni husika inategemea kupata kila mwezi na kila mwaka wakati inafanya shughuli zake.

****

TIN YA KAMPUNI.

Kupata **TIN YA KAMPUNI** mmiliki wa biashara anatakiwa kuwa na vitu vifuatatvyo,

- **Memorandum & Articles of Associations,**
- **Certificate of Incorporation**
- **TIN** binafsi ya kila mmiliki mpya,

- **barua za utambulisho** kutoka serikali za mtaa kila mmiliki
- **Vitambulisho vya taifa** vya kila mmiliki mpya,
- **Mkataba wa jengo** ambalo mtalitumia kama ofisi ya kampuni husika,

Hivo vitu vyote wamiliki wapya wa kampuni wataenda navyo mamlaka ya mapato Tanzania **(T.R.A),** ili wakakadiriwe kodi stahiki kwa kampuni husika. Baada ya kukadiriwa kodi inayoendana na kampuni mnayotaka kuifungua. **T.R.A** itawapatiwa **TIN ya kampuni** ambayo ni bure. Baada ya kukabidhiwa **TIN ya kampuni** na **T.R.A,** kuna baadhi ya kodi mtazilipa. Kodi za awali mtakazotakiwa kuzilipa ni **withholding tax** pamoja na **stamp duty**.

KODI YA JENGO (WITHHOLDING TAX (10%)).

Withholding tax, ni kodi ambayo mmiliki wa jengo anailipa kwa serikali baada ya mpangaji kulipa fedha za kupanga kwenye jengo la mmiliki husika. Mmiliki wa jengo atalipa **asilimia kumi (10%)** ya kodi ambayo

mfanyabiashara anaetaka kukodi jengo kwa ajili ya kulifanya ofisi ya kampuni yake, kwenye mamlaka ya mapato **T.R.A.**

Kwa mfano, Kama mpangaji au mfanyabiashara husika, kodi yake ya jengo ni **300,000/= T.SHS** kwa mwezi na anailipa kwa **miezi 12** jumla inakuwa **3,600,000/= T.SHS**. Asilimia **10%** ya kodi ya hilo jengo atailipa **T.R.A** kama **withholding tax,** ambayo itakuwa **360,000/= T.SHS** na kiasi cha fedha kinachobaki **(3,240,000/= T.SHS)** ndio atamlipa mwenye jengo analotaka kupanga mfanyabiashara husika.

STAMP DUTY

Stamp duty ni **Asilimia 1%** ya kodi ya jengo. Hivyo kwenye mfano husika hapo **Stamp Duty** itakuwa ni shillingi **36,000/= t.shs** ambayo ni **asilimia 1%** ya **3,600,000/= t.shs.** Kwahiyo kwa ujumla mmiliki husika wa biashara atalipa jumla **396,000/= t.shs TRA.**

Baada ya mmiliki wa biashara mpya kulipia fedha hizo za **Stamp Duty** na **Withholding Tax** atapatiwa cheti cha **TAX CLEARANCE**.

****

LESENI YA BIASHARA YA KAMPUNI.

Kupata leseni ya biashara ya kampuni unatakiwa kuwa na vitu vifuatavyo,

- **T.I.N ya kampuni** uliyopewa na **T.R.A**
- Cheti cha **TAX CLEARANCE**
- **Certificate of incorporation**
- **Mkataba wa jengo la ofisi** uliogongwa muhuri wa Mwanasheria na Mwanasheria akupe na risisti ya **EFD Machine.**
- Nakala kivuli ya **kitambulisho cha taifa** cha mmiliki wa biashara.
- Nakala kivuli ya **Memorandum & Articles of associations.**

Hivo vitu vyote utaenda navyo kwenye halmashauri unayoishi, ili uweze kukata **leseni ya biashara** unayotaka kuifanya kwenye **kampuni** husika.

****

KUKATA LESENI YA BIASHARA KWENYE TOVUTI (ONLINE BUSINESS LICENSE REGISTRATION).

Kwasasa Kuna maboresho ya mfumo wa ukataji **leseni za biashara Tanzania**. Mfanyabiashara anaweza kukata leseni ya biashara yake au kuomba upya **(Renew)** leseni yake kupitia tovuti rasmi ambayo ni, (**www.business.go.tz).** Tovuti hii itakupeleka moja kwa moja kwenye mfumo wa kuomba leseni. Na Mfanyabiashara husika atafuata maelekezo kwenye tovuti hiyo.

Kama kampuni husika itakuwa inajishughulisha na mradi zaidi ya mmoja, kampuni husika itatakiwa kukata leseni tofauti kwa kila mradi au biashara tofauti ambazo itafanya chini ya kampuni husika.

Kama kampuni husika itakuwa inahusika na utengenezaji wa bidhaa mbalimbali. Wamiliki wapya wa kampuni husika wataende mamlaka za kudhibiti ubora wa bidhaa Tanzania, ili kuthibitisha ubora wa bidhaa husika.

Mamlaka ya kudhibiti ubora wa bidhaa kwa **Tanzania** ni **TBS (TANZANIA BUREAU OF STANDARDS).**

Kama wamiliki wanasajili kampuni ya michezo watatakiwa kwenda **Tanzania Games Board.** Kama wamiliki wanasajili kampuni ya ujenzi wataenda kukata na leseni **CRB (CONTRACTORS REGISTRATION BOARD).**

Baada ya kupata leseni zote halali za kuanzisha kampuni husika, wamiliki wa kampuni husika watakuwa wameruhusiwa kufanya shughuli zote za kampuni kisheria Tanzania.

*****

SIFA ZA KAMPUNI.

1.KAMPUNI NI MTU WA KUFIKIRIKA KISHERIA (ARTIFICIAL PERSON).

Kampuni ni mtu wa kufikirika **(Artificial person)** kisheria. Ingawa kampuni ni mtu wa kufikirika ila kampuni kama kampuni yenyewe haiwezi kujisimamia. Ni lazima mtu achaguliwe Kusimamia shughuli za kampuni kwa niaba ya kampuni. Mtu wa Kusimamia shughuli za kampuni anaweza kuwa mmoja wa wamiliki wa kampuni husika au wamiliki wa kampuni husika wanaweza **kuajiri mtu** mwenye taaluma husika kuendesha kampuni yao na ataitwa **Mkurugenzi wa Kampuni (Director)** husika.

Kwasababu kampuni ni **Mtu wa Kufikirika Kisheria**, kampuni inaweza **kushtaki** na **kushtakiwa** kwa kutumia jina la kampuni husika. Kampuni pia, inaweza **kuingia mikataba** kwa majina ya kampuni na mikataba hiyo itaibana kampuni tu na mali zake.

2. MALI ZA KAMPUNI HAZI INGILIANI NA MALI BINAFSI ZA WANAHISA WA KAMPUNI HUSIKA (SEPARATE LEGAL ENTITY).

Mwanahisa yoyote haruhusiwi kuchukua mali yoyote ya kampuni kwa ajili ya matumizi binafsi ambayo hayana manufaa kwa kampuni. **Mali za kampuni** zinajitegemea na huwa kuna **ripoti ya fedha** za kampuni ambayo itaelezea jinsi mali za kampuni zinavyotumika.

3. KAMPUNI INATAKIWA ISAJILIWE KISHERIA NA IPATE CHETI CHA KAMPUNI (CERTIFICATE OF INCORPORATION).

Ili kampuni iweze kufanya shughuli zake inatakiwa kwanza isajiliwe kisheria na kampuni husika ipate cheti cha kampuni **(Certificate Of Incorporation).** Cheti hicho ndiyo kitathibitisha kwamba kampuni husika imesajiliwa kisheria. Kwa Tanzania cheti cha kampuni kinatolewa na **BRELA Tanzania.**

4. KAMPUNI INATAKIWA IWE NA MUHURI WAKE (COMPANY SEAL).

Nyaraka zote ambazo zitakuwa na **muhuri wa kampuni** ndiyo nyaraka pekee ambazo zitathibitishwa kama nyaraka halali za kampuni husika kisheria. Mkurugenzi wa kampuni au sekretari wa kampuni au mtu aliyeidhinishwa na **bodi ya wakurugenzi** wa kampuni husika, ndio anaruhusiwa **kugonga muhuri** nyaraka zozote za kampuni.

5. KUNA KAMPUNI ZINA UKOMO WA MADAI (LIMITED LIABILITY).

Endapo kampuni yenye ukomo wa madai itafilisika, ni mali za kampuni tu ndiyo zitafilisiwa na siyo mali binafsi za wanahisa.

6. KAMPUNI ITAENDELEA KUISHI HATA BAADA YA MMILKI KUFARIKI. (CONTINUITY OF EXISTENCE).

Ikitokea wamiliki wa kampuni husika **wakafariki,** kampuni itaendelea kuishi. Watu wengine wanaweza kuja **Kurithi kampuni** ile ile kisheria na kuendeleza shughuli za kampuni iliyoachwa na wamiliki ambao wamefariki.

Kampuni huwa **inazaliwa kisheria** na huwa **inavunjwa kisheria.**

7. KAMPUNI INARUHUSIWA KUUZA NA KUNUNUA HISA (TRANSFER OF SHARES).

Kampuni zinaweza **kuuza hisa zake** kwa **wanahisa wapya** hivyo kukuza mtaji wa kampuni husika. Ila **kampuni binafsi** hairuhusiwi kuuza hisa zake kwenye **soko la hisa**. Mauziano ya hisa za kampuni binafsi, yanafanyika ndani kwa ndani kwa wanahisa wenyewe au kwa mtu wa karibu wa wanahisa bila kutangaza nia ya kuuza hisa za kampuni husika kwa Umma.

****

SEHEMU YA TATU

❖

3. MTAJI WA KAMPUNI

Kuanzisha **kampuni mpya** huwa kuna gharama kadhaa zinahitajika. Kama **Mfanyabiashara** hana fedha kwa wakati huo anahitaji kuanzisha kampuni mpya anaweza kukwama kufungua kampuni husika. Lakini kuna njia kadhaa ambazo kitaalamu zinaweza kutumika kukusanya **mtaji wa awali (Start up capital raising)**. Ambao unaweza kutumika kusajili **kampuni mpya** na kuanza shughuli za kampuni mpaka pale **Kampuni** itakapokuwa na uwezo wa kujiendesha yenyewe kupitia miradi mbalimbali ya kampuni husika.

Njia ambazo kampuni mpya inaweza kuzitumia kupata mtaji wa kuanzisha na kuendesha kampuni mpya ni kupitia,

- **KAMPUNI MPYA KUTUMIA MTAJI MBEGU**
- **KAMPUNI MPYA KUUZA HISA**
- **KAMPUNI KUKOPO KUTOKA TAASISI YA KIFEDHA.**
- **KAMPUNI KUUZA HATIFUNGANI.**

KAMPUNI KUTUMIA MTAJI MBEGU (SEED CAPITAL RAISING).

Fedha mbegu au **Mtaji Mbegu,** ni zile fedha za kwanza kabisa ambazo huwa zinawekezwa kwenye biashara mpya au kampuni mpya. Mara nyingi kampuni inapoanzishwa kwa mara ya kwanza huwa inakutana na gharama mbalimbali ambazo zinahitaji fedha nyingi kuzimudu. Gharama hizo ni kama, gharama za **kusajili kampuni** na kupata **Certificate of Incorporation**, gharama za **kulipia kodi za serikali**, gharama za **kukata leseni ya kampuni,** gharama za **kukodi jengo** ambalo litatumika kama **ofisi ya kampuni,** gharama za **kununua samani** za kuweka ofisini na gharama zingine za awali.

Kiuhalisia si kila mtu anaweza kuzimudu hizi gharama zote pale anapoanzisha **Kampuni Mpya**. Ukizingatia kama kampuni ambayo inategemewa kuanzishwa ni **kampuni binafsi** haitaruhusiwa kuuza hisa kwenye **soko la hisa** kama njia ya kupata mtaji wa kuanzisha na kuendesha kampuni husika. Je, mtu anaetaka kuanzisha kampuni binafsi anapata wapi fedha za kusajili kampuni hii binafsi kama hana fedha kwa muda huo?

Kuna njia mbalimbali ambazo mtu anaetaka kufungua kampuni mpya anaweza kuzitumia ili kupata mtaji wa awali (**Mtaji Mbegu**), utakaomwezesha mfanyabiashara husika kufungua kampuni kwa mara ya kwanza.

MTAJI MBEGU WA JUMUIYA.

Huu ni aina ya mtaji ambao, wawekezaji tofauti wa awali **(Angel Investors)** wanawekeza mtaji wa fedha kwa ajili ya **usajili wa kampuni mpya** kabisa inayotegemewa kuanzishwa. **Mtaji Mbegu** huwa unawekezwa na wawekezaji kwa makubaliano rasmi ya kuuziwa sehemu ya umiliki wa kampuni hii mpya itakayoanzishwa kwa mfumo wa kumiliki hisa kwenye kampuni hii mpya baada ya kampuni husika **kusajiliwa kisheria.** Ili na wao **Wawekezaji** wawe wamiliki wa hii kampuni mpya ikisha sajiliwa na kuanza shughuli zake.

Mtaji huu unaitwa **Fedha Mbegu** au **Mtaji Mbegu** kwasababu ndio msingi wa kampuni mpya inayotegemewa kuanzishwa. Yani ndio fedha ya kwanza kabisa ambayo inapandwa kama mbegu kwenye bustani ndani ya kampuni mpya au biashara mpya. Na unaitwa **Mtaji Mbegu wa Jumuiya** kwasababu, kila mtu anaruhusiwa kuwekeza fedha

zake kama jiwe la msingi la kusajili na kuanzisha kampuni hii mpya.

Mara nyingi fedha za **mtaji mbegu za jumuiya** huwa zina changamoto ya kustawi au kuto kustawi. Inategemea na aina ya kampuni ambayo mfanyabiashara husika anataka kuanzisha kwa mara ya kwanza. Hivyo, kutokana na kampuni hii inayoanzishwa kwa mara ya kwanza kutokuwa na uhakika mkubwa wa kufanikiwa, huwa kuna michango midogo midogo ya kuanzia **Elfu Ishirini (20,000/=)** mapaka **Elfu Hamsini (50,000/=).** Ndio huchangishwa, Kama njia ya kupata mtaji wa awali wa kuwekezwa kama **fedha mbegu** yani mtaji wa asili kwenye kampuni mpya.

Mategemeo ya wawekezaji wa awali **(Angel Investors)** ambao wanatoa fedha zao kwa mara ya kwanza ni kuhakikisha kampuni hii mpya **inasajiliwa kisheria**. Kisha mchakato wa **kununua hisa** unafuata ili na wao wawekezaji wapya wawe wamiliki wa kampuni hii mpya kwa mfumo wa hisa. Malengo huwa ni kuwekeza kwenye miradi yenye uhitaji mkubwa ili kampuni husika iweze kutengeneza faida kubwa na ya uhakika na hatimae hisa ambazo walinunua wawekezaji hawa ziweze kupanda thamani zaidi.

KAMPUNI KUUZA HISA

HISA NI NINI?

Hisa ni kipande cha sehemu ya umiliki kwenye kampuni. Hisa ni vipande vidogo dogo vyenye thamani fulani, ambavyo vikiunganishwa kwa pamoja vinatengeneza kampuni iliyo kamili.

Hisa hutolewa na kuuzwa kwa watu kwa ajili ya kupata **mtaji wa kuanzisha kampuni** kama ni kampuni mpya. Pia kwa kampuni ambayo tayari imesajiliwa na inaendesha shughuli zake, inaweza kutoa na kuuza hisa za kampuni husika kwa wanahisa ambao wapo ndani ya kampuni au kwa watu wa nje ya kampuni husika.

Kama **kampuni** husika ni ya **Umma** na ipo kwenye **soko la hisa** huwa hisa zake zinauzwa kwenye soko la hisa kama njia ya kuongeza mtaji wa kampuni husika. Hisa hutolewa na kampuni kwa ajili ya kupata mtaji wa fedha ambao utatumika kuendesha miradi mbalimbali ya kampuni au kwa maneno mengine hisa hutolewa kwa ajili ya kuongeza mtaji mkubwa zaidi wa kutanua kampuni husika kwa ajili ya kuendesha shughuli zake.

Watu ambao wanawekeza fedha zao kwenye kampuni husika kwa **kununua hisa za kampuni** husika huitwa **Wanahisa.**

Wanahisa hununua hisa kwenye kampuni kwa ajili ya kuwa sehemu ya wamiliki wa kampuni husika. Kisheria watu kuanzia **wawili (2)** na kuendelea ndiyo wanaweza kuanzisha kampuni na wakaimiliki kwa **mfumo wa hisa** au kwa mfumo rasmi ambao unatambulika kisheria.

Baada ya kuanzisha kampuni husika **wanahisa** waliopo wanaweza kualika **wawekezaji wapya** kwenye kampuni husika kama njia ya kuongeza mtaji wa kampuni husika.

Kama mtu anataka kukuza biashara, ni vyema akaisajili biashara husika kwa mfumo wa **kampuni ya Umma** yenye **ukomo wa hisa (A Public Company Limited by Shares)**. Kampuni ya umma yenye ukomo wa hisa ni rahisi zaidi kupata mtaji mkubwa wa kuendesha kampuni husika. Kampuni zenye mitaji mikubwa ni rahisi kufanya miradi mikubwa hivyo kujiingizia kipato kikubwa zaidi.

Kama mtu ana ndoto za siku moja kuja kuwa tajiri mkubwa sana, ni vyema afikirie kuendesha biashara kwa mfumo wa **Kampuni yenye Ukomo wa Hisa** na kuisajili

kampuni husika kwenye soko la hisa ili iwe kampuni ya Umma yenye uwezo wa **kuuza hisa** zake kwa jamii.

***

AINA ZA HISA

Kuna aina tofauti za hisa. Na kila aina ya hisa ina utofauti kwenye **nguvu ya kupiga kura**, **mgawanyo wa faida** pale itakapotokea, na ikitokea kampuni ikafilisika kuna wanahisa wenye aina fulani ya hisa ndiyo wataanza **kulipwa kwanza.**

Hisa zimegawanyika katika makundi yafuatayo,

- **ORDINARY SHARES**
- **PREFERENCE SHARES**
- **CUMULATIVE PREFERENCE SHARES**
- **REDEEMABLE SHARES**
- **NON-REDEEMABLE SHARES**

ORDINARY SHARES.

Hizi ni hisa zenye nguvu zaidi kwenye kampuni. **Mwanahisa** mwenye **Ordinary Shares** ana husika moja kwa moja kwenye maamuzi ya kila siku ya maendeleo ya kampuni. Maamuzi hayo ni pamoja na, kuamua miradi ipi kampuni iwekeze, na miradi ipi kampuni isiwekeze fedha.

Mwanahisa mwenye **Ordinary Shares,** ana **haki ya kupiga kura** kwenye **mikutano ya kampuni** ili kupitisha au kukata ajenda mbalimbali ambazo zitakuwa zinajadiliwa kwenye vikao tofauti vya kampuni husika.

Mwanahisa mwenye **Ordinary Shares,** hisa zake huwa **zinaongezeka thamani** kadri kampuni inavyongezeka thamani. Pia, kadri kampuni inavyozidi kupata faida zaidi, wanahisa wenye **ordinary shares** watakuwa wanapata **gawio kubwa zaidi** kutokana na idadi ya hisa kila mwanahisa mwenye ordinary shares atakazokuwa anamiliki kwenye kampuni husika.

Ila ikitokea kampuni husika **ikafilisika**, wanahisa wenye **Ordinary Shares** kwenye kampuni husika iliyofilisika. Huwa wanalipwa wa mwisho kabisa, kama kuna

fedha au mali za kampuni husika iliyofilisiwa zitabaki baada ya kulipa madeni yote ya kampuni husika.

****

PREFERENCE SHARES

Mwanahisa mwenye **Preference Shares,** hausiki moja kwa moja kwenye maamuzi mbalimbali ya kampuni. Hana haki ya kupiga kura kwenye baadhi ya mikutano ya kampuni, ila anaruhusiwa kuchangia hoja kwenye vikao vya kampuni husika.

Hisa za Preference huwa haziongezeki thamani kadri kampuni inavyo ongezeka thamani, na wanahisa wenye **Preference Shares** hawahusiki moja kwa moja kwenye maamuzi ya kila siku ya kuendesha miradi mbalimbali ya kampuni husika. Wao huwa wanawekeza fedha kwenye kampuni husika na **kusubiri Gawio** pale kampuni itakapo tengeneza faida.

Gawio la wanahisa wenye **Preference Shares** huwa halibadiliki, hata kama kampuni itatengeneza faida kubwa kiasi gani wataendelea kulipwa gawio lile lile. Ila, ikitokea kampuni husika imefilisika watu wenye **Preference Shares** hulipwa kwanza wao, ndipo wanahisa wenye

Ordinary Shares hufuata. Mwanahisa mwenye **Preference Shares** ana uhuru wa kuuza hisa zake pale atakapoamua kuachana na kampuni husika.

****

CUMULATIVE PREFERENCE SHARES

Hawa ni wanahisa ambao hisa zao haziongezeki thamani kadri kampuni inavyopata faida. Lakini endapo mwaka husika hakutakuwa na **gawio**, fedha yao ya gawio inajumlishwa kwenye mwaka unaofuata wa gawio. Faida kubwa ya wanahisa wenye **Cumulative Preference Shares** ni kwamba, endapo mwaka huu kampuni haikutengeneza faida, wao hawana wasiwasi maana mwaka unaofuata watapata gawio la mwaka jana jumlisha na **gawio la mwaka** huo husika.

****

REDEEMABLE SHARES

Hizi ni hisa ambazo kampuni baada ya kuziuza kwa wanahisa, ina uwezo wa **kuzinunua tena** siku za mbeleni pale kampuni itakapoona hivyo. **Tarehe** ya kuzinunua tena hizi **Hisa.** Mara nyingi huwa inapangwa kabisa na **mwanahisa** husika huwa anapewa taarifa kabla hajazinunua aina hizi za hisa.

Kuna wanahisa baadhi huwa wanataka faida ya haraka. Hivyo wanapenda aina hizi za hisa za **Redeemable Shares.** Maana yake atawekeza fedha zake, baada ya muda fulani kampuni itazinunua tena hizi **hisa,** kwa bei ya juu kuliko bei aliyonunua mwanzo mwanahisa husika. Hivyo mwanahisa husika kutengeneza faida kwa njia hiyo.

Kampuni hutoa **Redeemable Shares**, pale inapokuwa na uhitaji wa haraka wa fedha kwa ajili ya kuwekeza kwenye mradi fulani ya muda mfupi. Lakini kwa muda huo kampuni inakuwa haina kiasi hicho cha fedha kwenye akaunti ya kampuni. Hivyo **kampuni** itatoa hisa za **Redeemable Shares** ili kupata mtaji wa mara moja. Baada ya mradi husika kutekelezwa, kampuni husika itazinunua tena zile hisa ambazo iliziuza mwanzo kwa wanahisa husika.

****

NON-REDEEMABLE SHARES

Hizi ni **hisa** ambazo kampuni baada ya kuziuza kwa **wanahisa,** haitakuwa na uwezo wa kuzinunua tena, vile inavyotaka kampuni. Mpaka mwanahisa husika ndio aamue kuziuza kwa kampuni au kwa mtu wa nje ya kampuni.

Non-redeemable shares zinamfaa mwanahisa ambae anapenda kuwekeza kwa **muda mrefu (long term investors)**

kwenye kampuni husika. Kuna **wanahisa** wana malengo ya muda mrefu **(long term plans). N**a wanahisa husika wanaelewa kwamba kadri anavyozidi kushikilia hisa **(holding shares)** kwenye kampuni, kuna uwezekano miaka ya baadae hisa zake zikapanda sana thamani **(increase in share value)** hivyo kuja kujitengenezea faida kubwa zaidi huko mbeleni kupitia **(capital gains).**

****

THAMANI YA KIPANDE CHA HISA (SHARE VALUE).

Kila **kipande cha hisa** huwa kina thamani fulani **(Share value).** Thamani ya kila **kipande cha hisa** hupatikana kutokana na mtaji wa jumla ambao umewekezwa kwenye kampuni husika **(Total share capital)** gawanya kwa jumla ya vipande ambavyo vimetengenezwa kwenye kampuni husika **(Alloted shares).**

Kwa mfano, kampuni ambayo imeanza na mtaji wa jumla wa million mia mbili **(200,000,000/= t.shs).** Na mtaji husika wa jumla kugawanya katika vipande **200,000** maana yake kila hisa moja itakuwa na thamani ya shillingi **1,000/= T Shs.**

(Mtaji wa jumla) 200,000,000/= = BEI YA HISA (1,000/= T.SHS)
(VIPANDE VYA HISA) 200,000/= T.shs

Wanahisa wanzilishi wa kampuni **(Founders),** wanaweza kumiliki **vipande** vyote vya hisa. Au wanaweza kumiliki **asilimia (%)** fulani ya vipande vya hisa kwenye kampuni na vipande vingine wakaviacha kwa ajili ya kuviuza kwa watu wengine wa nje ya kampuni ambao wangependaa kuingia kwenye kampuni husika hapo mbeleni.

ASILIMIA (%) ZA UMILIKI KWENYE KAMPUNI.

Umiliki wa kampuni wa jumla huwa ni wa **asilimia 100%.** Asilimia hizi za umiliki wa kampuni hugawanwya kutokana na **idadi ya hisa** ambazo kila **mwanahisa** anamiliki kwenye kampuni husika.

Kwa mfano, **kampuni xy Ltd** inaweza kuanzishwa na **wanahisa wanne (4).** Kila **Mwanahisa** akawekeza mtaji tofauti wa fedha kutokana na uwezo wake. Mtiririko wa umiliki wao kwenye **kampuni xy Ltd** ukawa kama ifuatavyo.

Mwanahisa wa kwanza (1) akamiliki **kampuni ya xy Ltd** kwa **asilimia 10%. Mwanahisa wa pili (2)** akamiliki **kampuni ya xy Ltd** kwa **Asilimia 20%. Mwanahisa wa tatu (3)** akamiliki **Kampuni ya Xy** Ltd kwa **Asilimia 5%.**

Na **mwanahisa wa nne (4)** akamiliki **kampuni ya xy Ltd** kwa **Asilimia 15%.**

Jumla wanahisa wote **wanne (4)** wakawa wanamiliki kampuni kwa **Asilimia 50%** na **Asilimia 50%** zingine zikawa zimebaki kwa ajili ya **wanahisa wengine wapya** ambao wangependa kununua hisa hapo baadae.

ASILIMIA ZA UMILIKI KWENYE KAMPUNI YA XY COMPANY LTD.

NO:	JINA LA MWANAHISA	ASILIMIA ZA UMILIKI WA HISA
1.	MWANAHISA J	10%
2.	MWANAHISA L	20%
3.	MWANAHISA Q	5%
4.	MWANAHISA E	15%
	JUMLA YA ASILIMIA ZA UMILIKI WA WANAHISA	**50%**
	ASILIMIA ZA HISA ZILIZOBAKI XY COM LTD.	50%
	ASILIMIA ZA MTAJI WA JUMLA XY COM LTD.	**100%**

Asilimia (%) hizi za umiliki wa hisa kwenye kampuni huwa zinapatikana kutokana na **kiasi cha fedha** ambacho kila mwanahisa husika amewekeza kwenye kampuni **gawanya** kwa **mtaji wa jumla wa kampuni** husika zidisha kwa **100%.** Hivi ndivyo asilimia za umiliki kwenye kampuni zinavyopatikana. Wanahisa huwa hawajipi wenyewe kienyeji **asilimia (%)** fulani za umiliki kwenye kampuni.

Kwa mfano, **kampuni xy Ltd** ilianzishwa kwa mtaji wa jumla wa million mia mbili fedha za kitanzania **(200,000,000 T.SHS).** Thamani ya kipande kimoja cha hisa kikawa kinauzwa kwa sh **1,000/= T.SHS,** hivyo **vipande 200,000** vya hisa ya **kampuni ya xy Ltd** vilitengenezwa.

Katika mtaji huu wa jumla wanahisa wake wanne (4) ambao ndio waanzilishi wa **kampuni xy Ltd,** wakanunua hisa za million mia moja fedha za kitanzania **(100,000,000/= T.SHS)** za **kampuni ya xy.** Na hisa zinazobaki za million mia moja **(100,000,000/= T.SHS)** zikaachwa kwa ajili ya wanahisa wa baadae ambao watapenda kujuinga na **Kampuni ya Xy Limited.**

Wanahisa wa **kampuni ya XY LIMITED** walinunua hisa kwa mtiririko ufuatao,

Mwanahisa J – 20,000,000/= T.SHS

Mwanahisa L – 40,000,000/= T.SHS

Mwanahisa Q – 10,000,000/= T.SHS

Mwanahisa E – 30,000,000/= T.SHS

Kujua kila mwanahisa anamiliki **kampuni xy LTD** kwa hisa asilimia ngapi, utachukua mtaji wa jumla wa kampuni kisha utagawanya na kiasi cha fedha alichowekeza mwanahisa alafu utazidisha kwa **100%.**

Mwanahisa J – $\frac{20,000,000/=}{200,000,000/=}$ X 100% = 10%

Mwanahisa L - $\frac{40,000,000/=}{200,000,000/=}$ X 100% = 20%

Mwanahisa Q - 10,000,000/= X 100% = 5%
200,000,000/=

Mwanahisa E - 30,000,000/= X 100% = 15%
200,000,000/=

Hivyo basi **Mwanahisa J** atamiliki **kampuni xy Ltd** kwa **asilimia kumi (10%), Mwanahisa L** atamiliki kampuni ya xy kwa **asilimia 20%, Mwanahisa Q** atamiliki kampuni ya xy kwa **asilimia 5%** na **Mwanahisa E** atamiliki kampuni ya xy Ltd kwa **asilimia 15%.**

Jumla ya umiliki wao wote kwenye **kampuni ya xy Ltd** ni **asilimia 50%. Asilimia 50%** za hisa zilizobaki zitahifadhiwa kwa ajili ya wanahisa wengine ambao watapenda kumiliki hisa kwenye **kampuni ya xy Ltd.**

Hivi ndivyo umiliki kwa asilimia unavyokuwa. Vitu viwili vya kuzingatia ni **mtaji wa jumla wa kampuni** husika ambao umeandikwa kwenye katiba ya kampuni husika na **kiasi cha fedha** ambacho kila mwanahisa anawekeza kwenye kampuni husika. Ukigawanya hivyo vitu viwili kisha ukazidisha kwa **100%** utapata **asilimia (%)** za umiliki kwa kila **Mwanahisa.**

❖ GAWIO (DIVIDEND) KWA WANAHISA.

Gawio ni malipo ambayo mwanahisa anapata baada ya kampuni aliyowekeza fedha zake kwa **mfumo wa hisa** kupata **faida** fulani. **Gawio** linaweza kuwa kwa **mfumo wa fedha** kwa mwanahisa husika kuingiziwa **fedha taslimu** kwenye akaunti yake ya benki. Au kwa **mwanahisa** husika kupewa **cheki** yenye thamani ya fedha za gawio na kampuni husika. Au **mwanahisa** husika anaweza **kupewa gawio** lake kwa mfumo wa mwanahisa husika **kuongezewa hisa** za ziada kutoka kwenye hisa za awali anazomiliki kwenye kampuni husika.

Mwanahisa anapolipwa **gawio** huwa analipa na **kodi ya gawio kwa serikali** ambayo huwa ni **asilimia 10%** ya **gawio la jumla** la **mwanahisa** husika. Mara nyingi kampuni hukata kodi ya gawio la kila mwanahisa husika na kuilipa kwa serikali na kiasi cha **gawio** kinachobaki ndio hulipwa mwanahisa kwenye akaunti yake ya benki au kwa kupewa fedha taslimu mkononi.

Kampuni nyingi huwa na utaratibu wa kuwa na **tarehe** maalumu ya kutoa **gawio** lake. Mara nyingi kampuni hutoa **gawio** kila baada ya miezi mitatu (3), au kila baada ya

miezi sita (6) au kila **mwisho wa mwaka** wa fedha wa kampuni husika ndio **gawio** hutolewa. **Wanahisa** huwa wanajulishwa **ratiba ya utoaji wa gawio** hivyo huwa wanaifahamu kabisa. Ingawa kabla ya **tarehe** maalumu ya utoaji wa gawio kufika, **kampuni** inaweza kutoa **gawio maalumu (special dividend)** kwa wanahisa wake kutokana na faida ambayo kampuni itakuwa imepata kwa kipindi husika.

Mfumo wa malipo wa gawio kwa mwanahisa

- Fedha taslimu
- Cheki
- Mwanahisa Kuongezewa hisa za ziada

***

❖ **SERA YA GAWIO (DIVIDEND POLICY).**

Hii ni **sera** ambayo inawekwa kwenye katiba ya kampuni ikielezea ni **asilimia (%)** ngapi ya faida itatolewa kama gawio kwa wanahisa wa kampuni husika. Sera ya gawio inaweza kuwa ni **asilimia arobaini ya faida (40%),** au **asilimia hamsini (50%)** ya faida ndio itatolewa kama gawio kwa wanahisa au hata **asilimia sitini (60%)** ya faida ndio inaweza kutolewa kama gawio kwa wanahisa.

Asilimia za gawio huwa inawekwa kwenye katiba ya kampuni na kila **Mwanahisa** anafahamu ni **asilimia (%)** ngapi ya faida hutolewa kama gawio pale **tarehe ya gawio** inapofika.

Baada ya wanahisa kulipwa **Gawio, Asilimia (%)** nyingine ya faida ya kampuni huwa inarudishwa kwenye akaunti ya kampuni kama **(Retained earnings)** ili kukuza **Mtaji wa Kampuni** husika.

*****

GAWIO KWA HISA (DIVIDEND PER SHARE)

Baada ya kampuni kufanya biashara zake na kupata faida, **sehemu ya faida** huwa inatolewa kwa wanahisa kama **Gawio.** Kila **Mwanahisa** atapata gawio fulani kutokana na **kiasi cha fedha** alichowekeza kwenye kampuni, na **idadi ya hisa** ambazo anamiliki kwenye kampuni husika.

Ili kujua kampuni itamgawia kiasi gani kila **Mwanahisa** kwenye sehemu ya faida ya kampuni kutokana na sera ya kampuni husika. Utachukua **faida ya kampuni** kisha utagawanya kwa idadi ya **hisa** zote ambazo zinamilikiwa na wanahisa.

Mfano **kampuni xy Ltd** ilitangza faida ya **Million Mia Mbili (200,000,000/= T.Shs). Sera ya kampuni** ya gawio ni kutoa gawio la faida la **Asilimia Arobaini 40%**

- **Asilimia arobaini (40%) ya 200,000,000/= t.shs ni 80,000,000/= T.SHS**

Hiyo ndio fedha ya jumla ambayo itagaiwa kama gawio kwa wanahisa wote kwenye kampuni husika.

Kujua kila mwanahisa atapata **gawio la shilling ngapi** kwenye **80,000,000/= T.SHS**.

Itabidi ufahamu idadi ya hisa za jumla kwenye kampuni ambazo zinamilikiwa na wanahisa wote. Kufahamu **idadi ya hisa** anazomiliki kila mwanahisa utachukua kiasi cha fedha alichowekeza mwanahisa kwenye kampuni, alafu utagawanya na thamani ya kipande kimoja cha hisa.

Mfano **kampuni ya XY Ltd** thamani ya kipande chake kimoja cha hisa ni **shilling elfu kumi (10,000/= t.shs).**

Idadi ya hisa anazomiliki kila mwanahisa kwenye kampuni ya XY COMPANY upo kwenye mtiririko ufuatao.

Mwanahisa J – aliwekeza 20,000,000/= T.SHS gawanya kwa 10,000/= t.shs = anamiliki HISA 2,000.

Mwanahisa L – aliwekeza 40,000,000/= T.SHS gawanya kwa 10,000/= t.shs = anamiliki HISA 4,000.

Mwanahisa Q – aliwekeza 10,000,000/= T.SHS gawanya kwa 10,000/= t.shs = anamiliki HISA 1,000.

Mwanahisa E – aliwekeza 30,000,000/= T.SHS gawanya kwa 10,000/= t.shs = HISA 3,000.

Jumla ya hisa elfu kumi **(Hisa 10,000)** zenye thamani ya **10,000/= T.Shs** kwa hisa moja zilinunuliwa na wanahisa wanne. Hivyo kufanya mtaji wa jumla wa wanahisa hao kuwa **100,000,000/= T.Shs.**

Kujua kila hisa moja italipwa shilling ngapi kwenye gawio utachukua,

Gawio ambalo linategemewa kutolewa **(80,000,000/= t.shs)** utagawanya na jumla ya hisa zote zilizonunuliwa na wanahisa **(Hisa 10,000).**

Faida 80,000,000/= t.shs = 8,000/= t.shs

Vipande vya Hisa 10,000

Kwahiyo kila hisa moja italipwa **8,000/= T.Shs.**

Mtiriko wa gawio kwa kila mwanahisa utakuwa kama ifuatavyo,

Mwanahisa J – HISA 2,000 X 8,000/= T.SHS = 16,000,000/= T.SHS

Mwanahisa L – HISA 4,000 X 8,000/= T.SHS = 32,000,000/= T.SHS

Mwanahisa Q – HISA 1,000 X 8,000/= T.SHS = 8,000,000/= T.SHS

Mwanahisa E – HISA 3,000 X 8,000/= T.SHS = 24,000,000/= T.SHS

****

SEHEMU YA FAIDA YA MIRADI YA KAMPUNI HURUDI KWENYE AKAUNTI YA KAMPUNI KAMA (RETAINED EARNINGS).

Baada ya kampuni yoyote kutengeneza faida kutokana na miradi yake. Kuna fedha kampuni itawalipa wanahisa wake kama **Gawio** na kuna fedha Kampuni itazirudisha kwenye biashara ili iweze kukua zaidi. Zile fedha ambazo kampuni huwa inazirudisha kwenye miradi yake kitaalamu huitwa (**Retained Earnings)**. Kampuni huwa inaweka **sera ya kampuni** ya asilimia ya faida ambayo irudi kwenye biashara na asilimia ya fedha ambayo itagaiwa kwa wanahisa.

Kujua asilimia za fedha ambazo zitarudi kwenye kampuni baada ya kutengeneza faida. Utachukua Faida ya kampuni kisha utatoa na asilimia ya fedha ambazo zitatolewa kama gawio kwa wanahisa.

FORMULA,

FAIDA YA KAMPUNI - ASILIMIA YA GAWIO

=

ASILIMIA YA FEDHA ZITAKAZORUDI KWENYE KAMPUNI

Kwenye mfano wetu wa mwanzo. **Kampuni ya XY COMPANY** ilitengeneza faida ya million mia mbili **(200,000,000/= T.SHS).** Sera yake ya gawio ni **asilimia 40%** ya faida. Hivyo sera yake ya kurudisha fedha kwenye kampuni ni **asilimia 60% ya faida.**

(FAIDA) 200,000,000 – (GAWIO) 80,000,000 = 120,000,000/= T.SHS (RETAINED EARNINGS).

Kwahiyo million mia moja na ishirini **(120,000,000/= T.SHS),** ndio fedha ambazo zitarudishwa kwenye akaunti ya kampuni ili kukuza mtaji wa **kampuni ya XY COMPANY LTD.**

Wamiliki wa kampuni wanatakiwa kuwa na sera endelevu na imara ya kiasi cha faida cha kugawana kama gawio na kiasi cha fedha cha kukirudisha kwenye akaunti ya kampuni, ili kampuni husika iweze kukua kimtaji.

Kampuni inapokuwa inarudisha sehemu kubwa ya faida kwenye kampuni kama (Retained earnings) inakuwa na faida nyingi za kibiashara.

1. Kampuni inapokuwa inarudisha sehemu ya faida kwenye kampuni**, inaongeza mtaji wake** na kuwa mkubwa zaidi. Hivyo kampuni husika inaweza kufanya miradi mikubwa zaidi.
2. Kampuni ikirudisha sehemu ya faida kwenye biashara, **inajipunguzia mikopo**. Badala ya kampuni kukopa fedha za kufanya miradi mingine, inatumia fedha zake za faida ya biashara kujiendesha yenyewe.
3. Kampuni inaweza **kuzalisha bidhaa mpya** au **kuingia soko jipya** kwa kutumia fedha ilizo zirudisha kwenye kampuni baada ya kutengeneza faida.

4. Pia kampuni kama ilikuwa na madeni makubwa inaweza kutumia sehemu ya fedha ilizozirudihsa kwenye kampuni **kupunguza madeni** hayo.

****

KAMPUNI KUKOPA BENKI

Mkopo wa benki ni njia nyingine ambayo kampuni inaweza kuitumia kupata fedha za kuendesha shughuli mbalimbali za kampuni husika. **Mkopo** kutoka benki unaweza kutumika kwenye kampuni husika kuongezea mtaji. Kampuni inapoongeza mtaji wake kupitia mkopo, inaweza kufanya uwekezaji kwenye miradi mikubwa zaidi.

Kampuni inaweza kutumia fedha za mkopo kutengeneza **bidhaa mpya** ambazo zikiuzwa zitaleta faida kubwa zaidi kwenye kampuni kuliko kiasi cha fedha kilichokopwa. Au kampuni inaweza kukopa fedha kwa ajili ya **kuongeza tawi jipya** la kampuni katika mkoa mwingine au katika nchi nyingine ili kuweza kuwafikia wengi zaidi na kuwa hudumia kiurahisi zaidi sehemu kubwa ya wateja wake hivyo kuzidi kuongeza faida kwenye kampuni.

Kampuni inaweza kuweka baadhi ya **mali za kampuni** kama **dhamana ya kupata mkopo** kutoka benki au taasisi yoyote ya kifedha ambayo inatoa **mikopo.**

Au **kampuni** inaweza kukopa fedha kutoka kwa **wawekezaji** au **watu binafsi** kwa mfumo wa kuuza **Hatifungani za Muda Mfupi** au **Hatifungani za Muda Mrefu** za kampuni husika.

****

KAMPUNI KUUZA HATIFUNGANI

HATIFUNGANI

Hatifungani ni mkopo ambao **Mwananchi, Mwekezaji** au kampuni inaikopesha **Serikali** au **kampuni** nyingine fedha kwa makubaliano maalumu ya malipo. **Serikali** au **kampuni ya (Umma au binafsi)** inaweza kukopa fedha kutoka kwa **Mwekezaji** au **Mwananchi** yoyote kwa mfumo wa **Hatifungani.** Kampuni inapokopa fedha kwa mfumo wa hatifungani inaweza kutoa **(Riba inayobadilika** au **Riba isiyobadilika).**

Pia Kuna baadhi ya mikopo kwa mfumo wa hatifungani haina **Riba** ila **Mwekezaji** au **Mwananchi** ataikopesha serikali au kampuni husika fedha kwa bei ya punguzo **(Discount Price)** na mkopo ukipevuka **(Mature) Mwekezaji** au **Mwananchi** husika atalipwa kwa bei halisi ya mkopo **(Face value).**

AINA ZA HATIFUNGANI.

1. Hatifungani kutokana na muda wa mkopo kupevuka

- Hatifungani ya muda mfupi **(Treasury Bills).**
- Hatifungani ya kati **(Treasury Notes).**
- Hatifungani ya muda mrefu **(Treasury Bonds).**

2. HATIFUNGANI KUTOKANA NA DHAMANA.

- Hatifungani yenye dhamana **(Secured Bond/Debenture).**
- Hatifungani isiyo na dhamana **(Unsecured Bond/Debenture).**

3. HATIFUNGANI KUTOKANA NA MTOAJI.

- Hatifungani za serikali **(Government Bonds, Notes & Bills).**
- Hatifungani za manispaa **(Municipal Bonds & bills).**
- Hatifungani za kampuni **(Corporate Bonds & Bills).**
- Hatifungani za kibenki **(Bank bonds, Notes & Bills).**

****

❖ **HATIFUNGANI YA MUDA MFUPI (TREASURY BILLS).**

Ni mkopo ambao **Mwananchi, Mwekezaji au Kampuni** inaikopesha serikali au kampuni nyingine fedha ambapo marejesho yake yanapevuka **(Mature) chini ya mwaka mmoja** yani baada ya siku **91** au baada ya siku **182** au baada ya siku **273** au baada ya siku **361.**

Kwenye **Hatifungani ya Muda Mfupi** Mwananchi au Mwekezaji ataikopesha **Serikali** au **Kampuni** fedha kwa bei ya punguzo **(Discount Price)** alafu muda wa mkopo kupevuka ukifika **(Maturity date). Mwananchi** au **Mwekezaji** husika atarudishiwa fedha zake katika bei halisi **(Face value).**

Kiwango cha chini cha **Mwananchi**, au **Mwekezaji** kuikopesha **Serikali** au **Kampuni** fedha kwenye **hatifungani ya muda mfupi** huwa ni kuanzia shillingi **laki tano (500,000/= T.SHS)** kwa **Tanzania** na kuendelea.

Mfano, **Mwekezaji** au **Mwananchi** anaweza kuikopesha kampuni shillingi **laki nane (800,000/= T.SHS).** Baada ya miezi sita **(siku 182),** Mwananchi husika anaweza kurudishiwa shillingi millioni moja **(1,000,000/= T.SHS).**

Ile **Laki mbili (200,000/= T SHS)** ambayo imeongezeka hapo kutoka kwenye **(800,000/= T.shs)** iliowekezwa awali ndio malipo kwa **Mwananchi** au **Mwekezaji** husika ambaye aliikopesha fedha kampuni husika au **Serikali.**

****

❖ **HATIFUNGANI YA KATI (TREASURY NOTES)**

Ni mkopo ambao **Mwananchi** au **Mwekezaji** anaikopesha Kampuni au Serikali fedha na Malipo yake yanapevuka **(Mature)** kwa zaidi ya mwaka mmoja mpaka **Miaka Kumi (10).** Kwenye **hatifungani ya kati (Treasury Notes),** Mwekezaji atakuwa analipwa **riba ya mkopo** ambayo inaweza kuwa **inayobadikika** au **isiyobadilika.** Asilimia za riba ya mkopo inaweza kuwa ni **Asilimia 3%, 5%** au hata **Asilimia 10%** ya mkopo wote.

Kwenye hatifungani ya kati **(Treasury Notes),** kila baada ya muda fulani labda **miezi sita (6)** au kila baada ya **miezi (12),** Mwekezaji atakuwa analipwa **riba ya mkopo** tu.

Mwekezaji husika ataendelea kulipwa **riba ya mkopo** pekee yake mpaka pale muda wa deni kupevuka utakapofika

(Maturity date) na Mwekezaji husika atarudishiwa fedha zake zote alizowekeza hapo awali.

Mfano, **Mwekezaji** anaweza kuikopesha kampuni shillingi **Millioni Kumi (10,000,000/= T SHS**), kwa riba isiyobadilika ya **asilimia 5%,** kwa muda wa **miaka mitatu (3).** Kwa maana hiyo kila baada ya mwaka mmoja yani **(miezi 12),** kampuni husika itakuwa inamlipa mwekezaji husika shillingi **laki tano (500,000/= T.SHS)** ambayo ni **Asilimia Tano (5%)** ya millioni kumi **(10,000,000/= T.SHS)** ambayo **Mwekezaji** husika ameikopesha serikali au kampuni.

Au kila baada ya miezi sita (6), kampuni au serikali itakuwa inamlipa **Mwekezaji** husika **shillingi laki mbili na nusu (250,000/= T.SHS)** ambayo ni nusu ya **asilimia 5%. Malipo** yataendelea kwa utaratibu huu mpaka miaka **mitatu (3)** itakapofika na mwekezaji husika atarudishiwa fedha zake zote **Shillingi Millioni Kumi (10,000,000/= T.SHS).**

****

❖ **HATIFUNGANI YA MUDA MREFU (TREASURY BOND)**

Hatifungani ya Muda Mrefu, ni aina ya mkopo ambao Mwekezaji anaweza kuikopesha kampuni au Serikali fedha na mkopo husika utapevuka **(Mature)** baada ya miaka **kumi (10)** na kuendelea. Kwenye **Hatifungani ya muda mrefu** mtu binafsi au kampuni inaweza kuikopesha serikali au kampuni nyingine fedha kwa malipo ya **asilimia za riba** ya mkopo husika kila baada ya muda fulani na tarehe ya mkopo kupevuka **(Maturity date)** ikifika Mwekezaji husika atarudishiwa fedha zake alizowekeza awali.

Kwenye **Hatifungani ya muda mrefu** mwekezaji husika atakuwa analipwa **asilimia za riba** ya mkopo husika tu. Na muda wa mkopo husika kupevuka **(Maturity date),** ikifika **Serikali** au **kampuni** husika itamrudishia fedha zote mwekezaji husika.

*****

❖ HATIFUNGANI KUTOKANA NA MTOAJI

1. HATIFUNGANI YA SERIKALI (GOVERNMENT BOND)

Huu ni mkopo wa muda mrefu ambao serikali inakopa ili kuendesha bajeti yake. **Mwananchi, Mwekezaji** au **Kampuni** inaweza kuikopesha fedha serikali kwa makubaliano maalumu ya malipo ya **asilimia ya riba** kila baada ya muda fulani na tarehe ya mkopo kupevuka **(Maturity date)** ikifika, serikali itamrudishia mwananchi au kampuni husika fedha zake za taslimu za awali ambazo serikali ilikopa.

Riba ya mkopo kwenye **Hatifungani za Serikali** inaweza kuwa ni **asilimia 3% au 5%** ya mkopo wote kutokana na sera za serikali za mikopo za wakati muda huo serikali inaombamkopo husika.

Hatifungani za serikali zinahamishika **(Transferable),** hivyo **Mwekezaji** au **Kampuni** husika ambayo imeikopesha serikali fedha kwa mfumo wa **hatifungani ya muda mrefu** inaweza kuuza hatifungani zake kwa mtu mwingine kabla ya muda wa hatifungani husika kupevuka **(Mature).**

Mwekezaji au **kampuni** husika inaweza kuuza hatifungani zake kwa **bei ya juu** zaidi kuliko ambayo ilinunulia hatifungani husika hivyo kutengeneza faida kabla ya tarehe ya kupevuka mkopo **(Maturity date).**

Pia hatifungani za serikali zinaweza kutumika kama dhamana **(Collateral),** kwa ajili ya mwekezaji au kampuni kukopa fedha kwenye taasisi ya kifedha.

Hatifungani za serikali huwa zinauzwa kwenye soko la awali la hisa **(Primary stock market)**, kwa njia ya mnada wenye ushindani kwa kila wiki.

Hatifungani za serikali pia huuzwa kwenye soko la pili la hisa **(Secondary stock market)**, ambapo wale wawekezaji na kampuni ambazo zilinunua hatifungani za serikali kwenye **soko la mwanzo (Primary stock market)** wanaweza kuwauzia kwa bei ya faida wawekezaji au kampuni nyingine ambazo zitahitaji Kununua **Hatifungani za Serikali** kwenye soko la pili la hisa **(Secondary Stock Market).**

Kwenye **soko la pili la hisa,** hatifungani za serikali huuzwa na kununuliwa wakati wowote ambao mnada wa hatifungani za serikali unaendana na kalenda inayotengenezwa na serikali kila mwaka.

Kila **mwananchi wa Tanzania** pamoja na wananchi wa **Afrika mashariki** wana haki ya kushiriki kununua **hatifungani za serikali** ya Tanzania kipindi cha mnada kikifika.

Kwa Tanzania hatifungani ya muda mfupi kiwango cha chini cha Kununua ni shillingi **laki tano (500,000/= T.SHS)** na kwa hatifungani ya muda mrefu kiwango cha chini cha Kununua hatifungani zake ni shillingi **millioni moja (1,000,000/= T.SHS).**

Kwa Tanzania, **Benki Kuu ya Tanzania** ndio wakala wa serikali ambae amepewa wajibu wa kuuza **Dhamana za Serikali** za muda mfupi na za muda mrefu kwa Wananchi na kampuni zinazotaka kuikopesha Serikali fedha.

****

2. HATIFUNGANI YA MANISPAA (MUNICIPAL BONDS)

Huu ni mkopo wa muda mrefu ambao **Manispaa** inakopa fedha kutoka kwa **Wananchi** au kwa **Kampuni** kwa makubaliano ya kulipa **riba ya mkopo** kila baada ya muda fulani na muda wa mkopo kupevuka ukifika **(Maturity date),** manispaa husika itarudisha fedha ilizokopa kwa **Mwananchi** au **Kampuni** husika.

Manispaa inaweza kuuza **hatifungani** kama njia ya kujipatia fedha za kuendesha miradi mbalimbali ya manispaa husika kama **Ujenzi wa Barabara**, **Ujenzi wa Shule** katika manispaa husika na **ujenzi wa hospitali** na huduma zingine za kijamii.

Sehemu ya **Mapato** yatakayopatikana katika miradi ya manispaa itatumika kulipa madeni ya hatifungani na sehemu nyingine ya fedha itawasilishwa kwenye **Serikali Kuu** kama utaratibu wa kuwasilisha fedha za manispaa kwa serikali unavyoelekeza.

3. HATIFUNGANI YA KAMPUNI (CORPORATE BOND).

Mwananchi au **Mwekezaji** anaweza kuikopesha kampuni fedha kwa mfumo wa **Hatifungani ya muda mfupi** au **Hatifungani ya muda mrefu**. Kampuni ikichukua mkopo kwa njia ya hatifungani, itatoa cheti cha hatifungani **(Bond Certificate)** au **Karatasi ya Bondi**.

Bond Certificate itaonyesha kiasi cha Mkopo ambao kampuni husika imekopa na muda ambao mkopo huo utachukua kupevuka **(Maturity date).**

Cheti cha Hatifungani kitaonyesha pia na **asilimia (%) za riba** ambazo **kampuni** husika itamlipa **mwekeza**ji na kila baada ya muda gani malipo hayo yatafanyika.

Hatifungani ya kampuni ya muda mrefu huwa inapevuka baada ya miaka miwili na kuendelea. Katika kipindi hicho mwekezaji atakuwa analipwa riba ya mkopo kwa asilimia (%) ambazo kampuni husika itakuwa imeziweka.

****

5. HATIFUNGANI ZA BENKI

Mwananchi, Mwekezaji au **Kampuni** inaweza kuikopesha taasisi ya kifedha kama benki fedha kwa mfumo wa **hatifungani ya muda mfupi** au **Hatifungani ya muda mrefu.** Mkopo wa **hatifungani ya benki ya muda mrefu** utakuwa ni wa makubaliano rasmi ya kisheria kati ya benki husika kumlipa mwekezaji riba ya mkopo kila baada ya muda fulani. Riba inaweza kulipwa labda kila baada ya **miezi mitatu (3),** au kila baada ya **miezi sita (6)** au kila baada ya **miezi kumi na mbili (12).**

Riba ya mkopo (%) itaendelea kulipwa kwa mwekezaji mpaka pale tarehe ya mkopo kupevuka **(Maturity date)** itakapofika. Muda wa mkopo husika kupevuka ukifika, benki husika itamrudishia fedha za awali yule **Mwekezaji** husika ambae aliikopesha benki husika fedha.

Riba ya asilimia (%) za mkopo wa hatifungani za benki unaweza kuwa ni **asilimia tano (5%)** au **asilimia kumi (10%)**, kutokana na sera za benki husika.

Kima cha chini cha kuwekeza kwenye hatifungani ya benki ya muda mfupi kinaanzia shillingi laki tano **(500,000/= T SHS)** na kuendelea.

Kwa **Tanzania,** ruhusa ya taasisi ya kifedha kama benki kuuza hatifungani inatolewa kwa **Mamlaka ya Masoko na Mitaji ya Dhamana Tanzania (CMSA).**

Kwa kawaida taasisi za kifedha kama benki, huwa wanatoa muda maalumu wa kuruhusu wananchi na kampuni mbalimbali Kununua hatifungani za benki husika. Muda huo unaweza kuwa ni mwezi mmoja au miezi miwili kutokana na mipango ya benki husika.

Baada ya dirisha la kwanza la ununuaji hatifungani za benki kufungwa. **Hatifungani za benki** husika zinaweza kupatikana kwa mteja mmoja wa hatifungani za benki husika kumuuzia mtu mwingine hatifungani zake kwa bei ya faida, hivyo mwekezaji husika kupata fedha za faida kabla hata hatifungani zake za benki husika hazijakomaa **(Mature).**

Ili Mwananchi au Kampuni iweze kununua hatifungani za benki husika ambayo inauza hatifungani zake. Mteja anatakiwa kutembelea tawi lolote la benki husika au kununua hatifungani kwa wakala wa benki husika inayouza hatifungani zake, kisha kwenda kwenye tawi lolote la benki husika kufanya usajili rasmi.

****

❖ HATIFUNGANI KUTOKANA NA DHAMANA.

Kuna baadhi ya mikopo ina dhamana na kuna baadhi ya mikopo haina dhamana au hauweki dhamana **(Collateral)** ya mali yoyote ili kupata mkopo husika.

1. HATIFUNGANI YENYE DHAMANA (SECURED BOND).

Ni mkopo ambao mkopaji anatakiwa kuwa na dhamana **(Collateral/Security)** ili aweze kupata mkopo husika. Dhamana inaweza kuwa **gari ya kampuni**, **majengo ya kampuni, viwanja** vinavyo milikiwa na kampuni au vya taasisi husika au kitu chochote chenye thamani kinacho milikiwa na kampuni husika kinachoendana na thamani ya mkopo husika unaotaka kukopwa.

FAIDA ZA HATIFUNGANI YENYE DHAMANA.

- **Riba ndogo** kwa mkopaji, kwasababu MKOPO HUU UNA DHAMANA.
- Pia Mkopaji anaweza kupewa **fedha nyingi** kwasababu Kuna dhamana anaiweka Kama rehani ya kupata mkopo husika.

2. HATIFUNGANI ISIYO NA DHAMANA (UNSECURED BOND).

Ni mkopo ambao mkopaji haweki dhamana ya aina yoyote ili kupata mkopo kwa mkopeshaji. Bali historia njema ya mzunguko wa fedha wa kampuni husika au taasisi husika ndio hutumika kama kigezo kikuu cha mkopaji husika kupata mkopo.

HASARA ZA HATIFUNGANI ISIYO NA DHAMANA (UNSECURED BOND/ DEBENTURE).

1. Riba kubwa kwasababu huu mkopo hauna dhamana.
2. Fedha ndogo anakopeshwa mkopaji kwasababu huu mkopo hauna dhamana.

***

DEBENTURE.

Ni aina ya mkopo ambao hauna dhamana ambao kampuni inakopa kwa mtu binafsi au kwa kampuni nyingine. **Kampuni** inakopa hizi fedha kama njia ya kupata fedha za kuendesha shughuli zake au kutanua miradi yake. **Kampuni** inaweza kukopa fedha kwa mfumo wa debenture bila ya kuweka dhamana yoyote.

Kampuni inayokopa kwa mfumo wa **Debenture,** itatoa **kuponi**, ambayo ni karatasi inayothibitisha kampuni husika imekopa na itakuwa inalipa riba kwa asilimia fulani mpaka

pale mkopo utakapo pevuka na kampuni iliokopa itatakiwa kulipa fedha yote iliyokopa.

AINA ZA HATIFUNGANI ZA MUDA MFUPI (DEBENTURE).

1. HATIFUNGANI INAYOBADILIKA (CONVERTIBLE DEBENTURES).

Huu ni **mkopo wa muda mrefu usio na dhamana** ambao unaweza kubadilika na kuwa **hisa** hapo mbeleni. **Mwekezaji** anaweza kuikopesha kampuni fedha ila hapo mbeleni akabadili maamuzi na kuamua kuchukua **hisa** kwenye kampuni husika kupitia fedha alizoikopesha kampuni husika.

Baada ya mwekezaji husika kufanikiwa kubadili amana yake ya **Mkopo** kuwa **Hisa** moja kwa moja **Mwekezaji** husika atahesabiwa kama **Mwanahisa** na mmoja wa wamiliki wa kampuni husika. **Mwekezaji** huyu ambae amebadilika kuwa **Mwanahisa** atakuwa analipwa na **Gawio la faida** pale ambapo kampuni husika itaamua kulipa **Gawio la faida** kwa wanahisa wake.

2. HATIFUNGANI ISIYOBADILIKA (NON-CONVERTIBLE DEBENTURES).

Huu ni **mkopo wa muda mrefu usio na dhamana** ambao hauwezi kubadilishwa kuwa **hisa.** Mwekezaji mwenye hatifungani isiyobadilika atakuwa anapokea **riba ya mkopo** kwenye kampuni husika kama malipo ya kuikopesha kampuni husika fedha. Muda wa mkopo kupevuka **(Maturity date)** ukifika, **Mwekezaji** husika atarudishiwa fedha zake za awali alizoikopesha kampuni husika.

3. HATIFUNGANI ZINAZOWEZA KUNUNULIWA MAPEMA (CALLABLE DEBENTURES).

Huu ni mkopo wa muda mrefu usio na dhamana, ambao kampuni unaweza kuulipa mapema kabla ya tarehe ya kupevuka haijafika.

Mfano, kampuni imekopa **Millioni kumi (10,000,000/= T.shs)** kutoka kwa mwekezaji. Makubaliano ya marejesho ya mkopo huu ni kipindi cha **miaka kumi (10). Riba ya mkopo** husika ni **asilimia 10%** ya fedha zote za mkopo, ikiwa na maana kila mwishoni mwa mwaka kampuni

husika inatakiwa kulipa **Million Moja (1,000,000/= T.Shs)** Kama riba ya mkopo husika kwa Mwekezaji.

Ila kwakuwa hatifungani husika zinaweza kununuliwa mapema **(Callable)** kampuni inaweza kuamua kulipa deni lote mapema kwa mwekezaji husika kabla ya **miaka kumi (10)** kufika ila kupunguza gharama za riba ambazo ingetakiwa kuzilipa kila mwaka kama isingelipa deni hilo mapema.

3. HATIFUNGANI ISIYOWEZA KUNUNULIWA MAPEMA (NON-CALLABLE DEBENTURES).

Huu ni **Mkopo wa Muda Mrefu Usio na Dhamana**, ambao kampuni iliokopa haiwezi kuulipa mapema mkopo huu kabla ya muda wa kupevuka haujafika. Itabidi kampuni husika iendele kulipa riba za mkopo (%) husika mpaka tarehe ya kupevuka kwa deni **(Maturity Date)** itakapofika ndio kampuni husika ilipe deni lote kwa mwekezaji husika.

***

❖ MUUNDO WA DEBENTURE.

1. KARATASI YA MAKUBALIANO

Ni karatasi ambayo inaonyesha makubaliano kati ya kampuni inayokopa fedha na mwekezaji ambae anaikopesha fedha kampuni husika. Karatasi ya makubaliano itaonyesha ni **kiasi** gani cha fedha ambacho kampuni husika inakopa, **riba** itakuwa asilimia ngapi, italipwaje na baada ya **muda** gani deni lote litakuwa limepevuka.

2. RIBA

Ni asilimia za malipo ambazo mkopaji analipa kutokana na kiasi cha fedha **(Principal)** alichokopa. **Riba** huwa inatozwa kwa asilimia. **Riba** inaweza kuwa ni asilimia 3**%, 5%** au **10%** ya deni lote na muda ambao deni husika litalipwa. Kadri mkopaji anavyozidi kuchelewa kulipa mkopo ndivyo **riba ya deni** inavyozidi kuwa kubwa. Riba inaweza kuwa ambayo **inayobadilika** au **Riba isiyobadilika.**

3. TAREHE YA KULIPA RIBA.

Hii ni tarehe ambayo riba ya deni itakuwa inalipwa. Riba ya deni inaweza kulipwa kila baada ya **miezi sita (6)** au kila bada ya **miezi kumi na mbili (12)** mpaka pale tarehe ya deni kupevuka itakapofika.

4. MUDA WA DENI KUPEVUKA.

Hii ni tarehe ambayo kampuni inayodaiwa inatakiwa kulipa deni lote la awali **(Principal).** Muda wa Deni kupevuka kwa **hatifungani ya muda mfupi** huwa ni chini ya mwaka mmoja, yani kuanzia **siku 91, 181** mwisho ni siku **364.** Kwa **hatifungani ya muda mrefu** muda wa mkopo kupevuka huwa ni zaidi ya mwaka mmoja na kuendelea. **Miaka 5, 10** mpaka **Miaka 30.**

5. MFUMO WA MALIPO.

Kampuni husika iliokopa inaweza kulipa taratibu deni la mkopo au inaweza kulipa deni lote kwa mkupuo baada ya muda fulani.

FAIDA ZA KUWEKEZA KWENYE HATIFUNGANI

1. Mwekezaji atakuwa **analipwa riba** kila baada ya muda fulani huku fedha yake ya awali **(Principal**) ikisubiri tarehe ya kupevuka **(Maturity Date)** ili alipwe
2. Mwekezaji anaweza **kuuza kuponi** yake kwa **bei ya faida** kwenye soko la hisa.
3. Mwekezaji anaweza **kukopa** pia na akatumia Hatifungani zake kama dhamana ya kupata mkopo.
4. Mwekezaji anaweza **kubadilisha kuponi** yake ya mkopo **kuwa hisa** kwenye Kampuni au Taasisi ambayo mwekezaji husika aliikopesha fedha hapo awali.
5. Hatifungani ni moja ya **njia salama** ya kuhifadhi fedha **(SAVINGS).** Na hatifungani salama zaidi za kuwekeza fedha ni **Hatifungani za Serikali** maana huwa zina Malipo yasiotetereka sana.

*****

SEHEMU YA NNE

❖

4. WANAHISA NA WAKURUGENZI KWENYE KAMPUNI.

❖ WANAHISA (SHAREHOLDERS).

Wanahisa, ni wamiliki wa kampuni husika. **Wanahisa** ni sehemu ya umiliki wa kampuni baada ya kuwekeza fedha zao kwa njia ya **kununua hisa** kwenye kampuni husika ili kufanya miradi mbalimbali ya kampuni.

Wanahisa wanaweza kuwa ndio **wakurugenzi** kwenye kampuni husika hivyo wakawa ndio wanaendesha shughuli za kila siku za kwenye Kampuni husika. Au **Wanahisa** wanaweza kuchagua watu wa nje ya kampuni ambao siyo wanahisa kuwa **Wakurugenzi** kwenye kampuni husika. **Wanahisa** ndio wenye jukumu la kuchagua **wakurugenzi** ambao watakuja kuunda **Bodi ya Wakurugenzi** kwenye kampuni husika.

❖ WAKURUGENZI (DIRECTORS).

Mkurugenzi kwenye kampuni ni mtu ambae anaendesha na kusimamia shughuli za kila siku kwenye kampuni. Shughuli kuu za mkurugenzi kwenye kampuni ni **kusimamia uzalishaji** bidhaa au huduma za kampuni, **usimamizi wa fedha** za kampuni pamoja na **utawala** kwenye kampuni husika. **Mkurugenzi (Director)** anaweza kuchaguliwa kati ya wanahisa au Mkurugenzi anaweza kuajiriwa na wanahisa ambao wanamiliki kampuni.

Kwa kampuni binafsi **(Private Company),** Mkurugenzi anaweza kuwa mmoja tu ambae atasimamia shughuli zote za kampuni husika. Idadi ya wakurugenzi katika kampuni inategemea na ukubwa wa kampuni husika. Kama kampuni ni mpya inaweza kuchagua mkurugenzi mkuu mmoja tu ambae ndio atakuwa anasimamia shughuli za kila siku kwenye kampuni husika na Wanahisa wengine wakabaki kuwa Wanahisa wa kawaida ambao wanasubiri gawio.

Au wakurugenzi wanaweza kuwa **wawili (2)** hadi **nane (8)** kwenye kampuni binafsi. Itategemea na idadi ya miradi

ambayo kampuni husika inategemea kuifanya na idadi ya matawi ambayo kampuni husika itakuwa nayo.

Kwa **kampuni ya Umma (Public Company),** Wakurugenzi wanaanzia **wawili (2).** Wamiliki wengine wa kampuni husika ya Umma wanaweza kubaki kama wanahisa tu ambao watakuwa wanahudhuria vikao vya bodi pamoja na kusubiri gawio pale tarehe ya gawio itakapofika. **Kikomo cha wakurugenzi** kwenye **kampuni ya Umma** ni mpaka **wakurugenzi (24).**

Kama **Mkurugenzi** atakuwa ni mmoja maana yake yeye ndio atakuwa **Mkurugenzi Mkuu**. Kama kutakuwa na Mkurugenzi zaidi ya mmoja maana yake kutakuwa na **Mkurugenzi Mkuu, Mkurugenzi Msaidizi, Sekretari wa Kampuni, katibu wa kampuni** pamoja na wajumbe wengine wa bodi ambao kwa pamoja wanatengeneza **Bodi ya Wakurugenzi** wa **Kampuni** husika.

❖ **MAJUKUMU YA MKURUGENZI MKUU (C.E.O) NA BODI YA WAKURUGENZI (BOARD OF DIRECTORS).**

1. Usajili wa wanahisa wapya.

2. Kurekodi taarifa zote za wanahisa.

3. Kumsajili sekretari wa kampuni.

4. Kuanda ajenda za vikao.

5. Kuanda mahesabu ya ripoti ya benki.

6. Kuanda mikataba ya wafanyakazi kwenye kampuni.

7. Kutunza nyaraka zote za usajili wa kampuni **(CERTIFICATE OF INCORPORATION & BUSINESS LICENCE).**

8. Kuanda na Kutunza vyeti vyote vya hisa **(SHARE CERTIFICATES).**

9. Kuratibu na kusimamia shughuli za kampuni.

10. Mkurugenzi mkuu anaiwakilisha kampuni kama balozi sehemu yoyote ile rasmi.

11. Kuhakikisha kampuni inajiendesha kwa faida.

12. Kuhakikisha **thamani za hisa** za kampuni zinapanda kwa kuweka mikakati thabiti.

13. Kuhakikisha **Gawio** linatolewa kwa **Wanahisa** kila tarehe ya kutoa **Gawio** inapofika.

14. Kuhakikisha kampuni inamiliki mali zake na kampuni inajiendesha kwa mali za kampuni.

15. Kutengeneza **Budget ya Fedha** ya kampuni kwa ajili ya kuendesha shughuli mbalimbali za kampuni husika.

(Budget ya **mishahara ya wafanyakazi**, na **wajumbe wa bodi**, budget ya **uzalishaji wa bidhaa**, budget ya **matangazo** na budget ya kuendesha shughuli zingine za utawala kama vikao vya bodi).

***

❖ KUCHAGUA BODI YA WAKURUGENZI.

Katiba ya kampuni **(Memorandum and Articles of Associations**), itataja idadi ya wajumbe ambao wataunda bodi ya wakurugenzi. Katiba ya kampuni husika inaweza kueleza kwamba, wajumbe kuanzia **wawili (2)** hadi **nane (8)** tu ndio wanaweza kuunda bodi ya wakurugenzi.

Pia, **katiba ya kampuni** itaelezea wajumbe hawa watachaguliwa kwa vigezo vipi ili kuunda **Bodi ya Wakurugenzi.** Katiba ya kampuni pia, itaelezea wajumbe wanaounda bodi ya wakurugenzi watakuwa wanakutana mara ngapi na kujadili nini kwenye kila mkutano wa kampuni husika.

Wanaoruhusiwa kuchagua **bodi ya wakurugenzi** ni **Wanahisa** tu wa kampuni husika. Mtu wa nje ambae hamiliki hisa za kampuni husika haruhusiwi kuchagua wajumbe watakaounda bodi ya wakurugenzi. Ila mtu wa nje anaweza kumwakilisha **(Proxy), Mwanahisa** ambae anamiliki hisa kwenye kampuni husika, ambae hataweza kufika katika uchaguzi wa **Bodi ya Wakurugenzi.**

Mwanahisa ambae hataweza kufika kwenye mkutano wa kuchagua wajumbe watakaounda **bodi ya wakurugenzi** na angependa kura yake imchague mmoja wa wajumbe kuunda **bodi ya wakurugenzi,** anaweza kuchagua mwakilishi wa nje ya kampuni **(Proxy)** ili aje kupiga kura kwa niaba yake.

Ila **mwanahisa** husika ambae atashindwa kuhudhuria vikao kwa kampuni anatakiwa kumtaarifu mwenyekiti wa Kampuni husika siku zisizopungua **saba (7)** kabla ya mkutano husika kwa barua. Kwamba hataweza kushiriki mkutano husika na anamteua mwakilishi wake ili apige kura kwa niaba yake.

Baadhi ya **wanahisa** wanaweza kuchaguliwa kuwa sehemu ya **Bodi ya Wakurugenzi.** Au wanaweza kuajiriwa baadhi ya watu kutoka nje ya kampuni husika, ambao siyo

wanahisa kuwa sehemu ya **Bodi ya Wakurugenzi** na watakuwa wanalipwa mishahara.

Watu wa nje ya **kampuni** husika wanaweza kuajiriwa kuwa sehemu ya **Bodi ya Wakurugenzi** kwasababu ya uzoefu wao na elimu zao za kuendesha shughuli za **kampuni.**

***

❖ KUCHAGULIWA KWA MKURUGENZI MKUU KWENYE KAMPUNI.

Bodi ya Wakurugenzi ndio inamchagua mkurugenzi mkuu. **Mkurugenzi mkuu** ndio raisi wa kampuni na ndio msimamizi mkuu wa shughuli zote za kampuni. **Bodi ya wakurugenzi** pia, ndio inamchagua **mkurugenzi msaidizi**, **(Executive Vice President)** au kampuni zingine humuita **(C.F.O - CHIEF FINANCIAL OFFICER).** Huyu ni msaidizi wa shughuli za mkurugenzi mkuu.

Wajumbe wote kwenye bodi ya **wakurugenzi** wanahaki ya kupiga kura na kufanya maamuzi kwenye vikao vya bodi ya wakurugenzi. **Bodi ya wakurugenzi** kwa ujumla inaweza kuundwa na wajumbe **wawili (2) mpaka wajumbe (24),** kutokana na aina ya kampuni na ukubwa wa kampuni

husika. Masuala yote haya, huwa yanaandikwa kwenye katiba ya kampuni **(MEMORANDUM & ARTICLES OF ASSOCIATIONS).**

❖ UKOMO WA MKURUGENZI KWENYE KAMPUNI

Mkurugenzi yoyote anaeunda bodi ya wakurugenzi kwenye kampuni, anaweza kusitishiwa ukurugenzi wake endapo yafuatayo yatatokea,

- **Mkurugenzi akiamua kujiuzulu yeye mwenyewe.**
- **Mkurugenzi akipatwa na matatizo ya akili.**
- **Mkurugenzi akipatwa na ugonjwa wowote ambao utamfanya ashindwe kutekeleza majukumu ya ukurugenzi kwa ufasaha.**
- **Mkurugenzi akifariki.**
- **Mkurugenzi akitumia mali za kampuni kwa matumizi binafsi.**
- **Mkurugenzi akithibitishwa amechafua taswira ya kampuni kwa namna yoyote ile.**

Mkutano wa dharura huwa unaitishwa kama kuna mkurugenzi yoyote inabidi aondolewe. Mkurugenzi husika atapewa nafasi ya kujielezea na kujitetea kutokana na mashtaka yanayomkabili.

Baada ya hapo, Kura zitapigwa na wanahisa wenye **hisa zenye nguvu ya kupiga kura**. Kama kura nyingi zitasema **Mkurugenzi** husika aondolewe basi ataondolewa. Kama kura nyingi zitasema **Mkurugenzi** husika apewe nafasi nyingine basi itakuwa hivyo.

Kama **Mkurugenzi** husika ataondolewa kwenye nafasi yake, itabidi achaguliwe mkurugenzi mwingine wa dharura kushikilia madaraka ili kufidia idadi ya wakurugenzi wanaotakiwa kutengeneza bodi ya wakurugenzi kwa mujibu wa katiba ya kampuni husika.

Mkurugenzi huyu wa dharura atakaechaguliwa atakaimu cheo cha mkurugenzi husika mpaka kwenye mkutano wa mwisho wa mwaka utakapofika. Kwenye mkutano wa mwisho wa **mwaka wa fedha wa kampuni** husika, moja ya ajenda itakuwa ni kumteua mkurugenzi mwingine baada ya yule wa awali kuondolewa.

Wanahisa wote kwenye mkutano wa mwisho wa mwaka wa fedha wa kampuni husika watapata nafasi ya

kuchagua mkurugenzi mwingine mpya ili akajaze nafasi ya **Mkurugenzi** aliye ondolewa.

***

❖ **MUUNDO WA UTAWALA KWENYE KAMPUNI.**

Muundo wa utawala kwenye kampuni yoyote huwa unaelezewa kwenye katiba ya kampuni. **Katiba ya kampuni** husika itaelezea mwenyekiti wa kampuni atakuwa ni nani, Makamu mwenyekiti atakuwa ni nani, sekretari atakuwa ni nani na wajumbe wengine wa muhimu kwenye kampuni huwa majina yao yanaorodheshwa kwenye katiba ya kampuni husika. Pia majukumu ya kila mjumbe wa bodi ya wakurugenzi yataelezewa kwenye **Articles of associations** ya kampuni husika, ili kila mmoja afahamu majukumu yake na afahamu anaripoti kwa nani baada ya kutimiza majukumu husika.

Muundo wa utawala kwenye Kampuni ni ufuatao,

I) <u>WANAHISA/WAMILIKI WA KAMPUNI</u>

Hawa ndio waanzilishi wa kampuni **(Founders).** Hawa ndio wenye nguvu kubwa kwenye kampuni. **Wanahisa** ndio wanachagua **bodi ya wakurugenzi.**

II) <u>BODI YA WAKURUGENZI</u>


Kazi ya **Bodi ya wakurugenzi** ni kusimamia shughuli zote za kila siku kwenye kampuni kwa niaba ya **wanahisa** ambao ndio wamiliki wakuu wa kampuni husika. Baadhi ya **wanahisa** wanaweza pia kuwa sehemu ya **bodi ya wakurugenzi.**

III) <u>MAMENEJA/ MAAFISA KWENYE KAMPUNI.</u>

Hawa wana ajiriwa na bodi ya wakurugenzi. Kazi zao ni za kiutendaji. Wanatekeleza majukumu yote waliopewa na bodi ya wakurugenzi. Kazi ya mameneja ni kuwasimamia wafanyakazi wa chini kwenye kampuni. Baadhi ya mameneja kwenye kampuni ni **Meneja Masoko, Meneja Uajiri, Meneja Uzalishaji, Meneja Wa Fedha** n.k.

IV) WAFANYAKAZI WENGINE

Hawa ni waajiriwa kwenye kampuni. Wafanyakazi wanaajiriwa na mameneja ingawa kudhibitisha uajiri wa wafanyakazi unafanywa na **bodi ya wakurugenzi**. Hawa ndio wanaingia sokoni na kutekeleza shughuli za uzalishaji wa Bidhaa na Huduma za kampuni na kuhakikisha bidhaa na huduma za kampuni zinawafikia wateja.



SEHEMU YA TANO

❖

#5. WARAKA NA KATIBA YA KAMPUNI (MEMORANDUM & ARTICLES OF ASSOCIATIONS

Memorandum of Associations (MOA) na **Articles of Association (AOA)** kwa Pamoja zinatengeneza Waraka na katiba ya kampuni ambayo inaitwa **Memorandum and Articles of Associations (MEMARTS).** Hizi ni nyaraka mbili za muhimu sana zinazohitajika wakati wa kuanzisha kampuni mpya. Kila nyaraka inaelezea kitu tofauti na vya muhimu kuhusu kampuni husika.

❖ WARAKA WA KAMPUNI (MEMORANDUM OF ASSOCIATIONS).

Ni nyaraka ambayo inaelezea kwa upana muundo mzima wa kampuni, wamiliki wa kampuni husika pamoja na shughuli zote za kampuni. **Memorandum** ndio nyaraka ya muhimu zaidi inayohitaji kuandaliwa wakati wa kusajili kampuni mpya. **Memorandum** ina vipengele vikuu **sita (6)** ambavyo ni lazima vyote viwepo kwenye **Memorandum** ili iweze kupitishwa kwenye usajili wa kampuni mpya.

Vipengele sita (6) kwenye memorandumvya muhimu ambavyo vipo kwenye memorandum ni pamoja na,

1) Jina la kampuni
2) Makao makuu ya kampuni
3) Shughuli zote za kampuni
4) Mtaji wa jumla wa kampuni **(Authorised Share Capital).**
5) **Majina ya wamiliki** wote wa kampuni husika. Pamoja na idadi ya hisa watakazo miliki kwenye kampuni husika.
6) **Aina ya ukomo wa kampuni** (Itakuwa ni kampuni yenye ukomo wa madai au ni kampuni isiyo na ukomo wa madai **(Limited or Unlimited Company).**

****

1. <u>JINA LA KAMPUNI</u>

Kampuni zote kabla ya kuanzishwa, ni lazima waanzilishi wake kwanza waseme wataita jina gani kampuni mpya husika. Baada ya hapo itabidi hilo jina jipya la kampuni litafutwe **(search)** kwenye mtandao wa mamlaka ya kusajili kampuni kwenye nchi husika ili kujiridhisha kuwa hakuna jina kama hilo ambalo tayari limesajiliwa na **Kampuni** nyingine.

Kama jina husika halitakuwa linatumiwa na kampuni nyingine ndipo kampuni mpya itaruhusiwa kulitumia jina husika. Kwa Tanzania taasisi inayojihusisha na shughuli za kusajili majina ya kampuni na kampuni mpya kwa ujumla inaitwa **BRELA (BUSINESS REGISTRATION AND LICENCE AGENCY).** Taasisi ya **BRELA** ndiyo ina husika na kuhakiki majina ya makampuni yote mapya kabla hayaja sajiliwa **Tanzania.**

Kama ndio mara ya kwanza mtu anataka kufungua kampuni anatakiwa kwanza **kubuni jina la kampuni** husika ambalo ni la kipekee na lipo tofauti. Baada ya hapo mtu husika anatakiwa kwenda kwenye **Mamlaka Za Usajili Wa Kampuni** kuangalia kama jina ambalo amebuni halitumiwi na mtu mwingine.

Baada ya hapo ndipo anaruhusiwa kuanza **kulisajili** jina husika ili liwe jina la kampuni mpya husika. **Ni makosa kisheria** kutumia jina la biashara ambalo tayari limesajiliwa na mtu mwingine kwa ajili ya shughuli zozote zile bila ruhusa ya mtu husika.

Baada ya **jina jipya la kampuni** husika kuhakikiwa halitumiwi na mtu mwingine kibiashara ndipo unaweza kulisajili jina husika kwa ajili ya kampuni mpya na jina hilo

litatumika kwenye **Memorandum ya Kampuni Mpya** husika kama jina la kampuni husika.

2. MAKAO MAKUU YA KAMPUNI.

Kila mtu anaetaka kufungua kampuni mpya na kuisajili kisheria ni muhimu awe na ofisi rasmi ambayo itatumika kama makao makuu ya kampuni mpya ambayo inategemea kufunguliwa. Kwenye **Memorandum** makao makuu ya kampuni mpya yataandikwa kuanzia **Nchi** ambayo kampuni mpya inafunguliwa, ikifuatiwa na **Mkoa** ambapo kampuni husika inafunguliwa, na baada ya hapo ni **Wilaya** ikimalizia na **Kata** ambayo ofisi husika itakuepo.

3. SHUGHULI ZOTE ZA KAMPUNI.

Kampuni yoyote mpya inayotaka kusajiliwa, ni lazima ieleze kwenye **Memorandum** yake itakuwa inajihusisha na **shughuli zipi kuu** na shughuli nyingine zote za kibiashara ambazo inategemea kuzifanya kwenye kampuni husika.

Shughuli za kampuni zinaweza kuwa ni za **Kilimo** na **Ufugaji**, **Uhandisi**, **Ujenzi, Upishi, Ushauri Nasaha**,

Masuala ya Masoko na **Biashara** au shughuli yoyote halali ambayo kampuni husika imefikiria kuifanya. Hizi shughuli zote za kampuni mpya husika lazima zielezewe kwenye **Memorandum** ya kampuni husika.

Sheria ya Kampuni kwenye (**Company act 2002**), inaruhusu kampuni moja kuwa na shughuli mbalimbali hata hamsini na kuendelea ambazo ni halali kisheria. Kampuni haizuiliwi kufanya shughuli moja tu pekee yake au shughuli chache. Kampuni ina uhuru wa kufanya shughuli nyingi tofauti tofauti. Ila tu, shughuli zote ambazo zitafanywa na kampuni husika ni lazima ziwe halali kisheria na shughuli zote za kampuni ziandikwe kwenye **Memorandum** ya kampuni husika na kila biashara ikatiwe leseni yake. Kwasababu kampuni haitaruhusiwa kufanya shughuli zozote za kibiashara ambazo haziku orodheshwa kwenye **Memorandum** ya kampuni husika na pia hairuhusiwi kufanya shughuli ambazo hazijakatiwa leseni.

4. AINA YA UKOMO UTAKAOTUMIWA NA KAMPUNI HUSIKA (Limited or Unlimited Company).

Memorandum ya kampuni, inabidi ieleze itatumia mfumo upi wa kusajili kampuni husika? Je kampuni mpya itasajiliwa kwa ukomo wa madai au usiyo wa madai? **(Limited or Unlimited Liability?)** Na kama ni kwa ukomo wa madai **(Limited Liability).** Je madai hayo ni kwa ukomo wa hisa? **(A Company Limited by Shares)** au kwa ukomo wa dhamana? **(A Company Limited by Guarantee).**

Ni muhimu kuelezea kwenye **Memorandum** kampuni itakuwa ni ya ukomo upi. Kwasababu kila mfumo una sheria zake za usajili na namna tofauti za kuendesha kampuni husika. Pamoja na utaratibu wa madai endapo kampuni husika itafilisika.

5. MTAJI WA JUMLA WA KAMPUNI (AUTHORIZED SHARE CAPITAL)

Memorandum pia ni lazima ieleze ni kiasi gani cha mtaji ambacho kampuni husika inakadiria kuanza nacho. **Mtaji wa jumla wa kampuni,** ni kiwango cha juu zaidi cha Mtaji ambacho kampuni husika imeruhusiwa na katiba yake kukiuza kwa wanahisa. Kiwango cha juu cha kampuni husika

kinaweza kuwa ni **5 Million T.shs, 10 Million T.shs, 50 Million T.shs** au hata **1 Billion T.shs**. **Kampuni** haiwezi kuuza hisa juu ya mtaji wake wa jumla ambao umeandikwa kwenye katiba yake **(Memorandum & Articles of Associations).**

Kila kampuni inaruhusiwa kukadiria kiasi cha mtaji wa jumla ambao kampuni husika itaanza nao wakati inaanzishwa. Kampuni inaweza kuanza na mtaji wa jumla wa **million 100**, **million 500**, au hata **Billion moja**. Kiasi hicho cha mtaji ambacho kampuni itaanza nacho inatakiwa kiandikwe kwenye katiba ya kampuni **(Memorandum & Articles of Associations).**

Kampuni inaposema itaanza na **Mtaji wa Jumla** wa **Billion Moja**. Haimaniishi kwamba hizo fedha kwa wakati huo zipo kwenye akaunti ya kampuni. Ila ni makadirio tu ya wapi kampuni husika inalenga kukua kimtaji.

WAMILIKI WA KAMPUNI (SHAREHOLDERS).

Memorandum, pia inatakiwa ijumuishe na idadi ya wamiliki ambao wataanzisha kampuni husika. Kila mtu ambae atakuwa mmiliki au Mwanahisa **(Shareholder)** kwenye kampuni mpya anatakiwa kuandikwa kwenye **Memorandum ya kampuni** husika.

Kwenye **Memorandum,** yataandikwa **Majina yote matatu** ya kila mmiliki, **Anuani za Makazi** yao pamoja na **Idadi ya Hisa** ambazo kila **Mmiliki** au **Mwanahisa** atakuwa anazimiliki kwenye kampuni husika.

Majina haya yataambatana na **saini** ya kila mmiliki. kisha chini ya jedwali la majina ya wamiliki wa kampuni wataapishwa na **mwanasheria** kama taarifa walizoandika kwenye **memorandum** ni za kweli.

kisha **mwanasheria** husika atasaini pia kwa chini ya majina ya wamiliki Pamoja na kuandika majina yake kamili na atagonga **muhuri wa mwanasheria.**

ARTICLES OF ASSOCIATION YA KAMPUNI.

Hii ni nyaraka ambayo inaelezea sheria ndogo ndogo za kampuni **(By-Laws)** na taratibu mbalimbali za uendeshaji wa kampuni. **Articles of associations** inaelezea shughuli zote za uendeshaji wa kampuni husika ikiwepo, jinsi **Wakurugenzi watakavyo chaguliwa, Majukumu ya Wakurugenzi kwenye kampuni** husika, Pamoja na **Mishahara ya Wafanyakazi** wote itakuwa ni shilling ngapi na itakuwa inalipwa kila baada ya muda gani.

Articles of association, itaelezea pia, jinsi kampuni itakavyokuwa inatoa hisa zake ili zinunuliwe **(Allotment of shares)**, jinsi kampuni itakavyokuwa **inalipa gawio (Dividend)**, **tarehe za kulipa gawio** kwa **Wanahisa**, na **Nguvu ya Upigaji Kura (Voting powers and rights)** kutokana na aina za hisa kila mwanahisa husika anazomiliki kwenye kampuni husika itaelezewa kwenye **Articles of Associations** ya **Kampuni** husika.

Articles of association, itaelezea pia masuala yote kuhusu **Vikao vya Kampuni** husika. Nyaraka hii itaelezea kutakuwa na **vikao vingapi kwa mwaka**, **aina ya vikao** hivyo na washiriki au walengwa wa vikao hivyo watakuwa wakina nani.

Articles Of Associations pia itaelezea kila baada ya muda gani kutakuwa na vikao vya wanahisa na wajumbe wa **Bodi ya Wakurugenzi.**

VIPENGELE VYA KWENYE ARTICLES OF ASSOCIATIONS YA KAMPUNINI.

1. KUTENGENEZA VIPANDE VYA HISA (SHARE ALLOTMENT).

Ni kitendo cha kutengeneza Vipande vya hisa, pale kampuni mpya inapoanzishwa. Kwa mfano mtaji wa jumla wa kampuni **(Company share capital)** ni **1 billion (1,000,000,000,000/=),** na thamani ya kipande kimoja cha hisa ni **elfu moja (1,000/=).** Hivyo kutokana na mtaji huo wa kampuni vitatengenezwa vipande vya hisa **Millioni moja (1,000,000,000).**

2. KAMPUNI KUTOA HISA (ISSUE SHARES) NA KUZIUZA (SUBSCRIBED SHARES).

- **Hisa zinazouzwa (Issued Shares)**

Hizi ni zile hisa ambazo zimetolewa na kampuni kwa ajili ya kuuzwa kwa wanahisa au kwa watu wapya wanaotaka kumiliki hisa za kampuni husika.

Issued shares ni hisa ambazo kampuni imeruhusu ziuzwe kwa wanahisa. Kampuni inaweza kuruhusu sehemu ya hisa zake ziuzwe kama njia ya kuongeza mtaji kwenye kampuni husika. Lakini kwa kuongeza wanahisa wengine maana yake hata **Gawio la Faida** litakuwa linapungua maana **wanahisa wapya** nao watapata gawio la faida kwenye kampuni husika.

- **Hisa ambazo hazijatolewa kuuzwa (Un-issued shares**)

Hizi ni zile hisa ambazo hazijatolewa na kampuni kwa wanahisa **(un-issued shares).** Au ni zile hisa ambazo hazijapewa ruhusa ya kuuzwa kwa **Umma** kama ni **kampuni** ya **Umma (Public Company)**. Siyo lazima kampuni iuze hisa zake zote.

Kampuni inaweza kuuza sehemu tu ya hisa zake na hisa zingine zikahifadhiwa na kampuni husika kwa ajili ya shughuli za mbeleni.

- **Hisa Zilizonunuliwa (Subscribed Shares)**.

Hizi ni hisa ambazo Zimenunuliwa na wanahisa wa kampuni husika. **Subscribed Shares** ni hisa ambazo wanahisa wametoa fedha na kuzinunua hisa husika kwa ajili ya **kuendesha miradi** mbalimbali ya kampuni husika.

3. HAKI ZA HISA (SHARE RIGHTS).

Hizi ni haki ambazo anakuwa nazo mwanahisa kutokana na aina ya hisa anazomiliki. Kwa mfano, Mwanahisa akiwa na **ordinary/common shares,** anakuwa na haki na nguvu zaidi kwenye kampuni husika. Mfano wa haki hizo ni kama **haki ya kupiga kura** kwenye vikao mbalimbali vya kampuni.

Ila mwanahisa akiwa na **Preference shares** anakuwa **hana nguvu kubwa** kwenye kampuni na hatakuwa na haki ya kupiga kura kwenye baadhi ya **vikao** mbalimbali vya kampuni. **Upigaji wa kura** kwa mwanahisa mwenye **preference shares** una mipaka.

4. CHETI CHA HISA (SHARE CERTIFICATE).

Cheti cha hisa hutolewa kwa mwanahisa mpya baada ya kununua hisa kwenye kampuni husika**. Cheti cha hisa** husimama Kama uthibitisho kwamba mwanahisa fulani anamiliki hisa kadhaa kwenye kampuni fulani.

Vitu vya muhimu kwenye cheti cha hisa ni vifuatavyo,

1. Jina la kampuni ambayo inatoa hisa.

2. Jina la mwanahisa mpya.

3. Tarehe ambayo mwanahisa mpya aliwekeza fedha kwenye kampuni.

4. Makazi ya mwanahisa.

5. Idadi ya hisa zilizonunuliwa na mwanahisa.

6. Thamani ya jumla ya hisa zilizonunuliwa na mwanahisa.

7. Bei ya kila kipande kimoja cha hisa.

8. Daraja la hisa **(ordinary shares or preference shares)**

9. Namba ya cheti cha hisa

10. Saini ya mwanahisa na mwenyekiti wa kampuni.

11. Kugonga muhuri wa kampuni kwenye cheti cha hisa

12. Picha ya ukubwa wa passport size ya mwanahisa mpya kubandikwa juu ya **cheti cha hisa.**

Cheti Cha hisa (Share Certificate) husimama kama uthibitisho kwamba mwanahisa fulani anamiliki hisa zenye thamani fulani kwenye kampuni husika.

5. KUSHIKILIA HISA (LIEN ON SHARES)

Ni kitendo cha kushikilia hisa za mwanahisa ambae ana deni kwenye kampuni. Mwanahisa husika inawezekana alikopa fedha kwenye kampuni, au wakati mwanahisa husika ananunua hisa Kwa mara ya kwanza kwenye kampuni husika, hakumalizia Kile kiwango cha chini Cha kununua hisa, hivyo alilipia nusu yake tu kwanza.

Mfano, kiwango cha chini cha kumiliki hisa za kampuni XY COMPANY LTD ni **laki moja (100,000/= T.shs). Mwanahisa** husika akalipia nusu yake ambayo ni **50,000/= T.shs** na deni likabaki **elfu 50**. Kampuni husika itazishikilia zile hisa za elfu hamsini **(lien on 50,000/= T.shs)** ambazo **Mwanahisa** ametoa mpaka pale atakapomalizia kiwango cha fedha kilichobaki ndipo **Mwanahisa** husika atapewa **cheti Cha hisa.**

6. KUKUMBUSHIA MADENI YA HISA (CALLS ON SHARES).

Ni kitendo Cha kampuni kumkumbusha kwa maandishi **Mwanahisa** kumalizia deni lake la hisa kwenye kampuni ambazo hakumalizia kuzilipia kipindi mwanahisa husika ananunua hisa kwa mara ya kwanza.

Mwanahisa anaponunua hisa kwa mara ya kwanza anaweza kutoa kiasi chote cha fedha cha kuanzia kununua hisa yani kwa mfano **(100,000/= T.SHS)** au anaweza kutoa nusu yake kwanza yani **(50,000/= T.SHS).** Kama mwanahisa husika atalipia nusu yake kwanza Kuna tarehe atapangiwa na kampuni ya kumalizia kiwango kilichobaki. Ule muda ukifika labda baada ya mwezi kampuni itamkumbusha kwa maandishi mwanahisa husika kumalizia deni lake.

Kama mwanahisa husika atashindwa kulipa kwa wakati aliopangiwa na kampuni na akapitisha ile tarehe ya kumalizia kulipa kiwango cha chini cha kumiliki hisa ataanza kutozwa na riba.

Zikipita wiki mbili tangu mwanahisa apitishe tarehe anayotakiwa kulipa deni kampuni ina haki kikatiba kuuza zile hisa husika. Na mwanahisa husika ataondolewa kwenye

kitabu cha wanahisa wa kampuni kwa mujibu wa katiba ya kampuni.

****

7. MWANAHISA KUHAMISHA UMILIKI WA HISA KWA KUUZA (TRANSFER OF SHARES).

Ni kitendo cha kuhamisha umiliki wa hisa kutoka kwa mwanahisa mmoja kwenda kwa mwanahisa mwingine kwa hiari na kwa makubaliano ya pande zote. Mwanahisa anaweza **kuhamisha** baadhi ya **hisa** zake kwa kuuza baadhi ya hisa zake kwa mwanahisa mwingine ndani ya kampuni au kwa mtu wa nje ya kampuni.

Mwanahisa akiuza baadhi ya hisa zake kwa mtu mwingine hisa zake za awali zitapungua. Pia **Gawio** la mwanahisa husika alieuza baadhi ya hisa zake litapungua pia. Kama mwanahisa atahamisha hisa zake zote kwa mwanahisa mwingine au kwa mtu wa nje anaetaka kununua hisa zake.

Mwanahisa husika atakuwa anaondoa haki zake zote za umiliki na kuziamishia kwa yule mtu mpya anaemuuzia hisa husika.

Wakati **mwanahisa** anataka kuhamisha umiliki wa hisa zake, kwanza atatangaza nia ya **kuuza hisa** zake kwa

wanahisa wenzake ndani ya kampuni. Kama hakutakuwa na mwanahisa ndani ya kampuni ambae atahitaji kununua hisa za ziada za mwanahisa anaeziuza, ndipo mwanahisa husika anaweza kuuza hisa zake kwa mtu wa nje ya kampuni.

****

8. KUHAMISHA UMILIKI WA HISA KWA KURITHI (TRANSMISSION OF SHARES).

Ni kitendo cha kuhamisha umiliki wa hisa kutoka kwa mwanahisa kwenye kampuni kwenda kwa mtu mwingine kwa **Amri ya Mahakama.** Kuhamisha hisa kwa kurithi **(Transmission Of Shares),** inatokea pale mwanahisa anapofariki au anapopata matatizo ya akili ambayo yanamfanya mwanahisa husika ashindwe kuendelea na shughuli za kampuni husika.

Kwakuwa mwanahisa husika **ameshafariki** au ana **Matatizo ya Akili** mahakama huwa inaamuru hisa za mtu husika zihamishiwe kwa warithi au kwa **Msimamizi wa Mirathi** ambae ndugu wa marehemu watakuwa wamemchagua kwa kuandika barua rasmi asimamie mali za marehemu.

***

TOFAUTI KATI YA KUHAMISHA HISA KWA KUUZA (TRANSFER OF SHARES) NA KUHAMISHA HISA KWA KURITHI HISA (TRANSMISSION OF SHARES) KWENYE KAMPUNI.

Kuna tofauti kubwa kati ya kuhamisha hisa kwa kuuza **(Transfer of Shares)** na kuhamisha hisa kwa Kurithi **(Transmission of Shares)** kwenye kampuni. Mwanahisa kwenye kampuni anaweza kuhamisha sehemu ya umiliki wake wa hisa kwenda kwa mtu mwingine kwa kuuza sehemu ya hisa zake kwa hiari au mwanahisa anaweza kupatwa na matatizo, kama ya akili au mwanahisa anaweza kufariki hivyo kupelekea hisa za mwanahisa husika zikaamishiwa kwenda kwa mtu mwingine kwa **amri ya mahakama**.

KUHAMISHA HISA VS KURITHI HISA.

UTOFAUTI	TRANSFER OF SHARES KUUZA HISA	TRANSMISSION OF SHARES / KURITHI HISA
Maana	Ni kitendo cha kuhamisha hisa za mwanahisa mmoja kwa kuuza kwenda kwa mtu mwingine kwa hiari.	Ni kitendo cha kuhamisha hisa za Mwanahisa kwenda kwa mtu mwingine kwa Kurithi na kwa Amri ya Mahakama.
Chanzo cha kutokea	Mmiliki wa hisa kuamua kuuza baadhi ya hisa zake au kuuza hisa zake zote.	Mmiliki wa hisa, **kufilisika, kupata matatizo ya akili au mmili**ki wa hisa **kufariki**.
Anaesimamia	Muuza hisa na Mnunua hisa	• Mrithi wa mali za marehemu. • Msimamizi wa mirathi **(Administrator)** aliyeidhinishwa na Mahakama.
Malipo	Malipo yatategemea na thamani ya kila kipande cha hisa kinachouzwa na idadi ya hisa zinazouzwa.	Mtu anaerithi hisa za mwanahisa mwenye matatizo ya akili au mwanahisa aliyefariki hatazilipia chochote ili kuzipata hisa husika.
Stamp duty	Stamp duty italipiwa kutokana na thamani ya hisa zinazouzwa.	• Stamp duty hailipiwi
Ukomo wa umiliki wa hisa	Ukomo wa umiliki wa hisa utaisha pale mmiliki wa hisa husika, atakapouza hisa zake kwa mtu mwingine.	Umiliki wa marehemu utaendelea kuwepo kwenye kampuni, warithi watakuja kuendeleza umiliki wa hisa za marehemu.

*****

9. IDADI YA WAJUMBE KWENYE MKUTANO WA KAMPUNI (QUORUM).

Hiki ni kipengele kingine ambacho kipo kwenye **Articles of Associations** ya kampuni. **Quorum** ni idadi ya chini ya wajumbe ambao wanatakiwa kuwepo ili mkutano wa kampuni husika ufanyike. Kama idadi ya wajumbe itakuwa pungufu ya asilimia zilizopangwa kwenye katiba ya kampuni, huo mkutano hauwezi kufanyika. Kutokana na katiba ya kampuni husika, wajumbe wanatakiwa kukubaliana ni **asilimia (%)** ngapi ya wajumbe wakihudhuria mkutano husika wa kampuni ndio mkutano ufanyike.

Inaweza kuwa ni **asilimia 20%** ya wajumbe wote wawepo kwenye mkutano husika wa kampuni au **asilimia 50%** ya wajumbe ni lazima wawepo.

Wanahisa ndio wataamua kiwango cha chini cha wajumbe wanaotakiwa kuhudhuria kikao cha kampuni ili kiweze kufanyika na maamuzi hayo yataandikwa kwenye Waraka na katiba ya kampuni **(Memorandum & Articles of Associations).**

10. KUFILISI HISA (FORFEIT OF SHARES)

Ni kitendo cha kufilisi hisa za mwanahisa ambae hakumalizia deni lake kwenye kampuni na ameshindwa kulilipa baada ya kuongezewa muda mrefu. Au kufilisi hisa za mwanahisa hutokea kama mwanahisa husika amedhurumu mali za kampuni au amebainika kwa ushahidi kuiba mali za kampuni.

Kama mwanahisa alilipa fedha nusu tu za kumiliki kiwango cha chini cha hisa, atapangiwa tarehe ya kumalizia deni. Ikitokea tarehe ya kumaliza deni imefika na mwanahisa husika hajamaliza deni, ataongezewa **siku 14** kwa maandishi na mkurugenzi wa kampuni za kumlaizia deni lake.

Kama na siku **kumi na nne (14)** zitapita bila mwanahisa husika **kumalizia deni lake**, kampuni ina haki kikatiba kufilisi zile hisa ambazo ilikuwa inazishikilia za mwanahisa husika.

Hisa zilizofilisiwa zinaweza kuuzwa kwa wanahisa wengine kwenye kampuni au zinaweza kuhifadhiwa tu na kampuni kwa matumizi ya mbeleni.

Mwanahisa aliefilisiwa hisa zake anaweza kutozwa na **faini ya riba** ya kushindwa kulipa deni lililobaki kwa

wakati. Na atatakiwa kulipa deni husika kwa mujibu wa katiba ya kampuni husika.

****

11. MIKUTANO YA KAMPUNI

Hiki ni kipengele kingine cha muhimu ambacho kipo kwenye **Articles of Associations** ya Kampuni yoyote ile. Kampuni huwa ina **Mikutano** tofauti tofauti ambayo hujadili ajenda mbalimbali kwa ajili ya maendeleo ya kampuni husika. **Mikutano ya kampuni** hutofautiana kwa **idadi ya wajumbe**, **aina ya wajumbe** wanaotakiwa kuhudhuria mkutano husika, pamoja na **malengo** ya kuitisha mkutano husika.

Kwenye kampuni mikutano imegawanyika katika makundi yafuatayo.

- **Mkutano Mkuu wa Mwaka (Annual General Meeting (A.G.M).**
- **Mkutano wa Bodi ya Wakurugenzi (Board of Directors Meeting).**
- **Mkutano wa Dharura (Extra ordinary Meeting)**

❖ MKUTANO MKUU WA MWAKA (ANNUAL GENERAL MEETING).

Huu ni mkutano mkubwa zaidi kwenye kampuni ambao hufanyika mara moja kwa mwaka wa fedha wa kampuni husika. **Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Kampuni**, unawakutanisha **wanahisa wote** wa kampuni husika, **bodi ya wakurugenzi** pamoja na **wadau wote** ambao wanahusiana na kampuni husika.

Kwenye mkutano mkuu wa mwaka wa kampuni husika, **Ripoti ya Mapato na Matumizi ya Fedha** pamoja na ripoti ya nafasi ya kifedha ya kampuni **(Financial Statements**) kwenye mwaka husika wa fedha husomwa. Pia **Uchaguzi Mkuu wa Viongozi** mbalimbali hufanyika kwenye mkutano wa mkuu wa mwaka wa fedha. Kama kutakuwa na mabadiliko ya viongozi kwa **kuchaguliwa viongozi wapya**, ajenda yake itaelezewa na kujadiliwa kwenye mkutano mkuu.

Muda wa uchaguzi ukifika, viongozi wapya watachaguliwa kwa mfumo wa kupiga kura na kiongozi atakaepata kura nyingi ndiye atashikilia nafasi husika kwenye Kampuni.

Watakaoruhusiwa **kupiga kura** ya maamuzi yoyote yale kwenye mkutano mkuu, ni wanahisa wenye hisa ambazo zinawaruhusu kupiga kura tu.

Kwenye **Mkutano Mkuu wa Mwaka**, wanahisa watapewa ruhusa ya kuuliza maswali mbalimbali kuhusu maendeleo ya miradi mbalimbali ya kampuni husika. Maswali hayo yatajibiwa na **Mwenyekiti wa Kampuni** au msaidizi wake kutokana na aina ya swali litakalo ulizwa. Wanahisa pia wataweza kutoa maoni yao na mapendekezo yao, kuhusu masuala mbalimbali ya uendeshaji wa kampuni husika. Kama maoni hayo yatawapendeza wajumbe wengi kwenye mkutano mkuu. **Kura zitapigwa** za kupitisha au kutopitisha mapendekezo mbalimbali kwenye mkutano mkuu wa kampuni husika.

❖ MKUTANO WA DHARURA (EXTRA ORDINARY MEETING).

Mkutano wa dharura, ni mkutano wowote unaofanyika kabla ya tarehe ya mkutano mkuu kufika au baada ya mkutano mkuu kufanyika. **Mkutano wa dharura** kwenye kampuni, huwa unaitishwa kama kuna jambo la dharura limetokea na maamuzi yake yanahitaji kura za wanahisa wote ili jambo husika lipitishwe au lisipitishwe. Mara nyingi, dharura husika haiwezi kusubiri mpaka mkutano mkuu wa mwaka.

Hivyo mkutano wa dharura utaitishwa ili jambo husika lililojitokeza ghafla liweze kutatuliwa haraka.

Taarifa ya mkutano husika wa dharura inatakiwa kutolewa kwa wanahisa angalau **masaa 72** kabla ya mkutano wa dharura husika. Wanahisa wote baada ya kupewa taarifa ya mkutano wa dharura husika, watahitajika kuhudhuria mkutano huo. Kama mwanahisa atashindwa kuhudhuria mkutano husika wa dharura atatakiwa kumtuma mwakilishi wake **(Proxy)** kama mtu wa kuja kwenye mkutano huo wa dharura kwa niaba yake.

Mwanahisa atakaetuma **mwakilishi (Proxy),** anatakiwa kumwandikia barua rasmi mwenyekiti ya kutohudhuria kikao hicho cha dharura hivyo mwakilishi wake ndio atakuja.

Mkutano wa dharura kwenye kampuni huwa unaitishwa kama kuna **mabadiliko ya ghafla ya viongozi** wanaounda bodi ya wakurugenzi. Labda kwa mfano, ghafla **mjumbe wa bodi ya wakurugenzi amefariki**, au **ameugua** ugonjwa ambao utamfanya ashindwe kuendelea na majukumu yake ya kiofisi. Au mjumbe wa bodi ya wakurugenzi ameamua tu **kujiuzulu** kwa sababu binafsi.

Uchaguzi wa dharura ni lazima ufanyike, maana bodi ya wakurugenzi lazima iwe na idadi fulani ya wajumbe kwa mujibu wa katiba ya kampuni husika. Hivyo kama ikatokea mjumbe mmoja atapungua kwasababu zozote zile, ni lazima **mkutano wa dharura** uitishwe ili uchaguzi mdogo ufanyike kufidia nafasi ambayo ipo wazi.

Au, kama kuna mradi wa ghafla umejitokeza kati kati ya mwaka wa fedha wa kampuni husika, kabla ya mkutano mkuu, na mradi husika una manufaa makubwa kwa wanahisa wote. Ni muhimu **mkutano wa dharura** uitishwe ili wanahisa wote waidhinishe fedha za kampuni zitumike

kuwekeza kwenye mradi husika, kama bajeti ya mwanzo ilishapangwa na ikaonekana haitoshi.

❖ **MKUTANO WA BODI YA WAKURUGENZI**

Huu ni mkutano ambao unawakutanisha wajumbe wa bodi ya wakurugenzi pekee yao. **Mkutano wa bodi ya wakurugezni** unaundwa na, **mwenyekiti wa kampuni**, **kaimu mwenyekiti wa kampuni**, **katibu wa kampuni**, **sekretari wa kampuni** pamoja na **wajumbe wengine** wanaounda **Bodi ya Wakurugenzi** ya **Kampuni** husika.

Mkutano wa bodi ya wakurugenzi huwa unaitishwa kujadili masuala mbalimbali ya uendeshaji wa kampuni husika. **Mkutano wa bodi ya wakurugenzi** hujadili matumizi ya **Bajeti ya Kampuni** ambayo ilipitishwa kwenye mkutano mkuu na wanahisa wote. Mkutano pia utajadili **ripoti ya miradi** ambayo kampuni inafanya, nani anasimamia kila mradi na jinsi **mapato** yanavyo kusanywa na kuhifadhiwa kwenye akaunti ya kampuni husika.

****

SEHEMU YA SITA

❖

6. KODI ZA KAMPUNI & ANNUAL RETURNS

KODI ZA KAMPUNI

Kampuni huwa inapata mapato kwa njia mbalimbali. Kwenye mapato hayo ya kampuni kuna wadau mbalimbali ambao wananufaika na mapato ya kampuni husika. Wadau hao ni kama, **Wafanyakazi** kwa njia ya **kulipwa mishahara**, **Wanahisa** kwa njia ya **kupata gawio la faida** na **Kampuni** yenyewe huwa inanufaika kama itatengeneza **faida** baada ya kutoa gharama za uzalishaji na uendeshaji wa kampuni.

Kwa mujibu wa Sheria, Kila mtu ambae ananufaika na mapato ya kampuni huwa anakatwa **kodi** yake. Wanufaika wa mapato ya kampuni ambao hukatwa kodi na serikali ni Pamoja na, **wafanyakazi** kwa njia ya kukatwa **kodi ya Mishahara (Income Tax)**, **Wanahisa** kwa njia ya kukatwa **kodi ya Gawio (Dividend Tax)** la hisa na **Kampuni** yenyewe inakatwa **kodi ya faida ya mapato (Corporate Tax)** baada ya kulipa gharama zote kinachobaki huwa ni

faida ya kampuni na huwa inatozwa kodi ya faida ya kampuni.

- **KODI YA MISHAHARA KWA WAFANYAKAZI (INCOME TAX).**

Kila **Mfanyakazi** ambae ameajiriwa kwenye kampuni yoyote anatakiwa kulipa **kodi ya mshahara.** Kodi ya mshahara huwa inatofautiana kati ya mfanyakazi mmoja na mwingine. Kuna kiwango cha mshahara ambacho mfanyakazi akianza kulipwa anatakiwa kukatwa na kodi kutokana na ukubwa wa mshahara husika. Kadri muajiriwa anavyozidi kulipwa mshahara mkubwa ndivyo anavyozidi kulipa kodi kubwa zaidi kwenye mshahara husika.

Kodi ya mishahara kwa wafanyakazi italipwa kila mwezi ambao mfanyakazi husika anapokea mshahara. Ikitokea mshahara wa mfanyakazi ukaongezwa kodi ya mshahara husika nayo itaongezeka. Ikitokea mshahara wa mfanyakazi husika ukapunguzwa na muajiri wake, kodi ya mshahara nayo itapungua.

Mwajiri ndio huwa anakusanya kodi zote za wafanyakazi wake za kila mwezi na kuziwasilisha kwenye mamlaka ya mapato ya nchi husika. Sehemu ya mshahara

inayobaki baada ya makato ya kodi ndio huwa analipwa mfanyakazi husika.

Kwa mfano mfanyakazi analipwa mshahara wa mia nne elfu fedha za kitanzania **(400,000/= T.SHS).** Kodi ya mfanyakazi huyu inaweza kuwa ni **asilimia 18% ya 400,000/= T.SHS**. Ambayo itakuwa ni shillingi **(72,000/= T.SHS).** Hivyo fedha ambayo mfanyakazi husika ataingiziwa baada ya makato ya kodi ni **(328,000/= T.SHS).**

❖ **KODI YA GAWIO KWA WANAHISA (DIVIDEND TAX) (10%).**

Kila mwanahisa ambae anamiliki hisa kwenye kampuni anatakiwa kulipa kodi ya gawio la hisa pale gawio litakapotolewa. Kodi ya gawio la hisa huwa ni **asilimia kumi (10%)** ya gawio zima la mwanahisa husika. Kadri mwanahisa husika anavyozidi kupata gawio kubwa ndivyo anavyozidi kulipa kodi kubwa zaidi kwenye gawio lake.

Kodi ya gawio kwa kila mwanahisa italipwa kila muda ambao gawio kwa wanahisa hutolewa. Kama kampuni husika ina sera ya kutoa gawio kila baada ya **miezi sita (6),** basi kila baada ya miezi sita gawio linapo tangazwa na kutolewa **asilimia kumi (10%)** ya gawio kwa kila mwanahisa litakatwa kama **kodi ya gawio.**

Ikitokea **gawio la faida** likaongezwa kodi ya gawio husika nayo itaongezeka. Ikitokea **Gawio** husika likapunguzwa na kampuni, hata **kodi ya gawio** nayo itapungua.

❖ **KODI YA FAIDA YA KAMPUNI (CORPORATE TAX) (30%).**

Kila kampuni ambayo imetengeneza faida kutokana na shughuli zake za kibiashara inatakiwa kulipa kodi ya faida ya kampuni. Kodi ya faida ya kampuni huwa ni asilimia therathini **(30%)** ya faida halisi kabla ya kodi **(Net Profit Before Tax)** ambayo kampuni husika itakuwa imeipata. Kadri kampuni husika inavyozidi kutengeneza faida kubwa ndivyo inavyozidi kulipa kodi kubwa zaidi kwenye faida yake.

****

ANNUAL RETURNS

Hii ni ripoti ya taarifa za kampuni ambayo kila mwisho wa mwaka kampuni iliyosajiliwa **(Incorporated)** inatakiwa kutuma katika mamlaka ya usajili wa kampuni **(Company House).** Kwa Tanzania taarifa za annual return za kampuni zinatumwa kwenye mamlaka za **BRELA.**

Taarifa za kampuni ambazo kila mwisho wa mwaka zinatakiwa kutumwa ni kama,

- Taarifa za mabadiliko ya wakurugenzi **(Change of Directors),**
- **Mabadiliko ya sekretari** wa kampuni,
- Mabadiliko ya mtaji wa kampuni **(Changes of Authorized Capital),**
- **Mabadiliko ya wanahisa** kama kuna wanahisa wapya watakuwa wameongezwa kwenye kampuni au wamepungua pamoja na
- Taarifa za fedha za kampuni za mwaka **(Annual Audited Financial Statements).**
- **Mabadiliko ya ofisi (Makao makuu) ya kampuni.**

Na mabadiliko yoyote ambayo yatatokea ndani ya mwaka husika wa kampuni yanatakiwa kuripotiwa kwenye **Annual Returns** ya kampuni husika**.**

Kampuni inapofanya mabadiliko yoyote yale inatakiwa kutoa taarifa kwa **Msajili wa Kampuni** mapema. Kampuni husika itajaza fomu husika kutokana na mabadiliko inayotaka kuyafanya kwenye kampuni husika. Kwa Tanzania fomu hizi zinapatikana kwenye tovuti ya **BRELA.**

Mwishoni mwa kila mwaka husika wa fedha, wakati kampuni inawasilisha taarifa za mwisho wa mwaka **(Annual returns)** kampuni husika inatakiwa kuambatanisha na **Mahesabu ya Kifedha** ambayo yamekaguliwa na mwasibu aliesomea taaluma ya uhasibu. **Financial statements** ambazo zitakuwa **Audited.**

Kila kampuni inatakiwa kuhakikisha inatuma taarifa za kampuni yake kwa wakati. Mfano kampuni husika ilisajiliwa tarehe **5.OCT.2019** Kila inapokaribia **5.OCT** ya mwaka unaofuatia kampuni husika inatakiwa kutuma taarifa zote za kampuni kwa msajili wa kampuni. Hata kama kampuni husika haikufanya mabadiliko yoyote kwenye kampuni Kama kuongeza au kupunguza wanahisa. Bado kampuni husika

inatakiwa kutuma taarifa za **Annual Returns** kwa msajili wa kampuni **(BRELA).**

Ikitokea kampuni husika imefanya mabadiliko yoyote kwenye kampuni husika inatakiwa kutoa taarifa mapema kwa msajili wa kampuni ambae kwa Tanzania ni **BRELA**.

Kwa mfano wetu wa awali hapo juu, kampuni imesajiliwa tarehe **5.OCT.2019** na kabla ya **5.OCT** ya mwaka unaofuatia haijafika, kampuni husika ikafanya mabadiliko ya sekretari wa kampuni kwa kumweka sekretari mpya tarehe **20.JAN.2020.** Kampuni husika inatakiwa kupakua fomu ya mabadiliko ya sekretari **BRELA.** Itajaza fomu husika pamoja na kulipia ada ya fomu husika Kisha itatuma mabadiliko hayo kwa msajili wa kampuni.

SEHEMU YA SABA

❖

7. MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA ZA KAMPUNI.

❖ MAPATO YA KAMPUNI

Mapato ya kampuni ni malipo kwa njia ya fedha au kitu chochote cha thamani, ambacho kampuni inalipwa na mtu au taasisi kwa kufanya kazi fulani au kwa kuuza bidhaa na huduma fulani ambayo ni halali kisheria. Mapato ya kampuni yanaweza kuwa ni **fedha** zinazo tokana na **Mauzo** ya kila siku ya bidhaa na huduma za kampuni, **Wadhamini** kuipa fedha kampuni na watu mbalimbali **Kununua Hisa** kwenye kampuni.

Hizi zote ni njia ambazo kampuni huzitumia kupata fedha za kuendesha shughuli mbalimbali za kampuni pamoja na kulipia gharama mbalimbali za kampuni.

NJIA ZA KAMPUNI KUTENGENEZA FEDHA.

- **MAUZO YA BIDHAA NA HUDUMA ZA KAMPUNI.**
- **UDHAMINI (SPONSORSHIP).**
- **KAMPUNI KUUZA HISA.**
- **KAMPUNI KUUZA HATI FUNGANI.**
- **UWEKEZAJI WA KAMPUNI.**

NJIA AMBAZO KAMPUNI INAWEZA KUZITUMIA KUPATA FEDHA ZA MTAJI (CAPITAL) YA KUENDESHA SHUGHULI ZAKE.

Kampuni Binafsi na **Kampuni za Umma** zinaweza kutumia njia tofauti tofauti kupata fedha za kuendesha miradi yake. Kila njia huwa ina faida zake na hasara zake kwa kampuni husika hivyo umakini mkubwa huwa unahitajika wakati wa kuchagua njia ya **kupata mtaji** wa kuendesha shughuli za kampuni.

Njia za kupata mtaji (Capital) ya kuendesha shughuli za kampuni ni,

1. WANAHISA KUWEKA FEDHA KWENYE KAMPUNI KWA KUNUNUA HISA ZAKE (SHAREHOLDERS' EQUITY FINANCING).

Njia ya kwanza ambayo kampuni inaweza kupata mtaji wa kuendesha shughuli zake ni kwa kuuza hisa zake kwa wanahisa wa kampuni husika na kwa watu wa nje ambao wangependa kujiunga na kampuni husika.

Hii ni njia ya kwanza na kubwa zaidi ambayo kila kampuni duniani huitumia kama njia ya kupata fedha za kuendesha miradi yake.

Faida ya kampuni kuuza sehemu ya hisa zake ni kwamba yule mwekezaji anaekuja kununua hisa anakuja kuwa mmoja wa wamiliki wa hiyo kampuni. hivyo mtagawana faida au hasara ambazo zitapatikana baada ya kufanya miradi kwenye kampuni.

Faida nyingine ya kutumia njia ya **Shareholder's Equity Financing** ni kwamba mwekezaji akinunua hisa leo gawio lake litakuja baada ya miezi sita (6) na kuendelea.

Hivyo kampuni inapata muda wa kutosha wa kuendesha miradi yake bila kuwa na presha ya kutoa fedha ndani ya muda mfupi. Pia kampuni inayo ruhusa ya kutotoa gawio au kutolipa gawio kwa kipindi fulani kama inaona miradi bado haijakomaa vizuri.

Mfano kama miradi haijapata mzunguko mkubwa wa kifedha **(Low Cash Flow)** wa kuweza kuwalipa wanahisa kwa wakati huo. **Kampuni** haitatoa **gawio** kwa kipindi hicho. Au kampuni itatoa sehemu ndogo tu ya faida kama gawio labda **Asilimia 10%** au **20%** ya faida. Na asilimia zingine **80%** au **90%** zitarudishwa kwenye kampuni kama **Retained Earnings.**

2. KAMPUNI KUKOPA FEDHA (DEBT FINANCING).

Njia ya pili ambayo kampuni inaweza kupata fedha za kufanya miradi yake ni kwa **kuomba Mkopo** kwenye taasisi ya kifedha kama **Benki.**

Pia kampuni inaweza kutumia **hatifungani (Bonds & bills)** kama njia nyingine **ya kuomba mkopo** kwa watu binafsi **(Wawekezaji)** au kwa taasisi zingine.

Kampuni inapokuwa imekopa fedha labda benki au kwa mtu binafsi inatakiwa kulipa riba ya mkopo kila baada ya muda fulani au kulipa fedha za mkopo taratibu jumlisha na riba ya mkopo kila baada ya muda fulani.

Hasara ya kampuni kukopa ni kwamba ni lazima zile fedha za mkopo kampuni iwe inazilipa kila baada ya muda wa kulipa ukifika **(Maturity Date).** haijalishi kampuni husika imetengeneza **faida au hasara** ni lazima ilipe madeni iliokopa muda wa deni kulipwa ukifika. Tofauti na kwenye hisa ambapo kama kampuni haina fedha haitalipa gawio kwa wakati huo.

Hasara nyingine ya **Mkopo** ni kwamba Kama kampuni ikishindwa kulipa fedha za mkopo kwa wakati inaweza kupigwa **penalty au fine** au **riba ya mkopo** inaweza kuongezeka kadri mkopo husika unavyozidi kuchelewa kulipwa.

Pia **taasisi za kifedha** huwa zina masharti mengi mpaka uwe na **vigezo vya kupewa mkopo**. Kama **Kampuni** au biashara husika ni mpya, huwa ni vigumu sana kukopeshwa fedha kwasababu **Kampuni** husika inakuwa haina mzunguko mkubwa wa fedha **(constant cash flow)** wa

kuwezesha kulipa **Madeni ya Mkopo** na kubaki na fedha za kuendesha shughuli za kila siku za kampuni.

3. KUUZA BIDHAA NA HUDUMA ZA KAMPUNI.

Njia ya tatu ambayo kampuni inaweza kuitumia kupata fedha za kuendesha miradi yake ni kwa kubuni na **Kuzalisha Bidhaa** na **Huduma** mbalimbali kisha kuziuza kwa wateja tofauti. **Mapato** yanayotokana na **mauzo ya bidhaa na huduma** za kampuni yatatumika kulipia gharama mbalimbali za uendeshaji wa kampuni na faida zingine za mapato zinazobaki zinaweza kutumika kuongeza Miradi mipya kwenye kampuni.

Njia ya kutumia **mauzo ya bidhaa na huduma** za kampuni ina faida zake pale ambapo kampuni inatengeneza **mapato makubwa** kuliko matumizi yake. Hapo kampuni inaweza kutengeneza faida kubwa ambayo inaweza kutumika kufanya miradi mingine mikubwa zaidi.

Changamoto ya kutumia njia ya mauzo huja pale ambapo kampuni ina mapato madogo kuliko matumizi yake. Au kampuni inaweza kuwa inatengeneza faida, lakini zile faida zinakuwa ni ndogo sana kutosha kutanua miradi ya kampuni husika.

Mara nyingi **kampuni mpya** ndio huwa zinakutana na changamoto ya kutengeneza **faida ndogo** kutokana na ugeni wa kampuni husika na bidhaa zake sokoni.

Pia kampuni nyingi huwa zinaanza kwenye hasara kutokana na ukweli kwamba kampuni mpya huwa inaanza na gharama nyingi sana wakati inaanzishwa kama,

- Gharama za kusajili kampuni husika na kupata **(Certificate of Incorporation).**
- Gharama za kukata vibali vyote stahiki **(TIN, LESENI YA BIASHARA, STAMP DUTY, WITH-HOLDING TAX).**
- Gharama za kulipia ofisi ya kampuni na fremu ya kuendesha biashara za kampuni.
- Gharama za kununua bidhaa za kuanzia.
- Gharama za kununua samani za ofisi kama **(Meza, Viti, Makabati ya kuweka Ofisini)** na gharama zingine za aina hiyo.

Ili **kampuni** iweze kumudu gharama zote hizi inatakiwa kuhakikisha inazalisha na kuuza bidhaa kwa wingi ili iweze **kurejesha fedha za mtaji** uliowekezwa na kampuni husika na kuanza kutengeneza faida.

4. <u>KAMPUNI KULIPWA KUTANGAZA BIDHAA ZA WATU AU TAASISI ZINGINE (ENDORSMENT).</u>

Kampuni moja inaweza kulipwa na **kampuni nyingine** kutangaza bidhaa zake kwa makubaliano maalumu. Kwa mfano kwenye mpira tunashuhudia club kubwa za mpira wa miguu kama **Manchester united**, ipo katika mfumo wa kampuni na huwa inalipwa fedha kutangaza bidhaa za kampuni zingine kama **Adidas, Nike, Chevelot** n.k. Klabu mbalimbali huwa zinatangaza bidhaa za kampuni zingine kwenye jezi zake na kwenye viwanja vyake vya michezo ambapo watazamaji wengi huingia na kupata nafasi ya kuona mpira na matangazo ya kampuni zingine.

Fedha za Endorsement huwa ni nyingi sana na huwa zinatajirisha kampuni nyingi sana. Lakini ili kampuni husika iweze kutumika kutangaza kampuni zingine inatakiwa kuwa ni kampuni kubwa na maarufu sana ili kampuni zingine zinavyojitangaza zipate kuwa maarufu na kubwa pia.

5. KAMPUNI KUPEWA TUZO NA ZAWADI (COMPANY GIFTS AND AWARDS).

Njia nyingine ambayo kampuni inaweza kutengeneza fedha ni kupitia zawadi na Tuzo mbalimbali ambazo inaweza **kushinda (Win)** au **kuchaguliwa kushiriki (Nominated).** Kampuni mbalimbali duniani zimeweza kujishindia tuzo nyingi kubwa hivyo kuweza kupata fedha nyingi ambazo zilikuja kutumika kama mtaji wa kukuza kampuni zao.

Lakini Ili kampuni iweze **kushinda Tuzo** au **kuchaguliwa kushiriki** kwenye **Tuzo** fulani inatakiwa iwe inazalisha Bidhaa Bora na bidhaa au huduma husika ziwe zinafanya vizuri sana sokoni.

6. KAMPUNI KUWEKEZA AU KUKOPESHA KAMPUNI ZINGINE NA KULIPWA GAWIO NA RIBA YA MKOPO (COMPANY INVESTMENTS).

Kampuni pia inaweza kufanya uwekezaji kwa **kununua** au **kujenga Majengo** na kupangisha kama **Nyumba za makazi (Residential houses & Apartments), Hoteli** na hata kuwekeza kwenye **hostel za wanafunzi**. Pia kampuni inaweza kuwekeza kwa **Kujenga Migahawa** na **kupata fedha** kupitia **uuzaji wa chakula** na utoaji wa

huduma zingine zinazopatikana kwenye **migahawa. Kampuni** pia inaweza **Kununua Hisa** kwenye **kampuni zingine** na kulipwa **gawio** fulani kila baada ya muda fulani. Na mwisho **kampuni** inaweza **kuikopesha serikali fedha** kwa riba kwa njia ya **Hati Fungani ya Muda Mfupi** au **Hatifungani ya Muda Mrefu (Treasury Bills & Bonds).**

Hizo zote ni njia ambazo kampuni inaweza kuzitumia kutengeneza faida fulani ambayo inaweza kuja kuwekezwa kwenye miradi mingine mikubwa zaidi ya kampuni husika. Lakini siku zote **uwekezaji** huwa unachukua **muda mrefu** mpaka uweze kupata faida kutokana na uwekezaji uliofanya.

Mara nyingi Uwekezaji **(Investment)** huchukua kuanzia **Miezi 3, Miezi 6** mpaka Mwaka mzima na zaidi unaweza kuisha ndio kampuni husika iliofanya uwekezaji iweze kupata manufaa ya uwekezaji wake kwa kuanza kulipwa **Riba** au **Gawio** kutokana na ununuaji wa **Hisa** au **Hati Fungani.**

Kampuni yoyote inapotaka kufanya uwekezaji inatakiwa kuwa na uvumilivu sana na **Wanahisa** wake wanatakiwa wawe ni watu wenye malengo ya mbele zaidi. Maana kwenye **Uwekezaji** wowote ule, ile miezi au miaka ya mwanzo huwa ni vigumu sana kutengeneza faida kubwa.

Lakini kama **Wanahisa** watakuwa **wavumilivu** na wakiwa na **mipango thabiti** ya muda mrefu baada ya muda fulani wanahisa husika watakuja kutengeneza fedha nyingi sana.

Ukiangalia kwa umakini hapo utagundua njia rahisi na salama zaidi za kampuni kuweza kupata fedha za kuendesha miradi yake ni kwa **Kuuza Hisa** zake kwa **Wanahisa** na kampuni kupata mtaji wa kuendesha shughuli zake **(Shareholders Financing)** na njia nyingine salama ni kwa **kampuni kuuza bidhaa** au **huduma** zake kwa **wateja** na kupata fedha za faida ya miradi husika.

❖ MATUMIZI YA KAMPUNI.

Matumizi ya kampuni ni gharama zote za kila siku na kila mwezi ambazo kampuni huwa inaingia wakati inaendesha shughuli zake za kila siku za uzalishaji na uuzaji wa bidhaa na huduma zake kwa wateja.

- **Gharama za Kununua bidhaa au kuzalisha bidhaa.**
- **Mishahara kwa wafanyakazi.**
- **Gawio la faida kwa wanahisa.**
- **Kodi kwa serikali.**
- **Gharama za masoko (kutangaza bidhaa za kampuni, kusambaza bidhaa za kampuni).**

Kila mwezi kampuni inatakiwa kuanda **Ripoti Ya Mapato na Matumizi (Financial Statements)** ili kuratibu kwa ufasaha shughuli za kampuni husika. **Ripoti ya mapato na matumizi** ya kampuni husika kwa mwezi itaonyesha **jumla ya mapato** ambayo kampuni husika imeingiza kwa mwezi husika Kisha itatoa na **gharama za Kununua bidhaa** au kuzalisha bidhaa baada ya hapo gharama za kuendesha

shughuli za kampuni zitatolewa pia ili kupata **Faida ya awali (Gross Profit)** kabla ya kutoa gharama za uendeshaji.

Ukitoa gharama za uendeshaji kampuni **(Operating & Administartive expenses)** kwenye faida ya awali **(Gross Profit)** kinachobaki ni faida kabla ya kodi **(Profit before tax).** Kodi ya kampuni huwa ni **asilimia 30% ya Faida ya kampuni**. Na fedha inayobaki baada ya makato ya Kodi ndio huwa Faida halisi **(Net Profit)** ya mwisho wa mwezi husika.

Kwa mfano kampuni husika inajihusisha na uzalishaji na **Uuzaji wa Asali** ya **Nyuki wakubwa** na **wadogo**. Yafuatayo ni makadirio ya mauzo ya asali kwa mwezi **January.01.2020** mpaka mwezi **February.01.2020.**

MFANO WA MAKADIRIO YA MAUZO YA ASALI KWA MWEZI JAN.1.2020 MPAKA FEB .01.2020.

NO:	AINA YA ASALI	IDADI LITRE	BEI	MAUZO KWA MWEZI
1.	NYUKI WAKUBWA	200	12,000/=	2,400,000
2.	NYUKI WADOGO	100	30,000/=	3,000,000
	JUMLA	**300**		**5,400,000**

Kampuni hii ilifanikiwa kuuza jumla ya **litre 200** za asali **Nyuki Wakubwa** kwa bei ya **12,000/= t.shs** na kufanikiwa kupata mapato ya **2,400,000/= t.shs.**

Pia kampuni ilifanikiwa kuuza **litre 100** za asali **Nyuki Wadogo** kwa bei ya **30,000/= t.shs** na kufanikiwa kupata mapato ya **3,000,000/= t.shs.**

MFANO WA MAKADIRIO YA GHARAMA ZA MANUNUZI YA ASALI KWA MWEZI JAN.01.2020 MPAKA FEB.01.2019.

NO:	AINA YA ASALI	IDADI LITRE	BEI	MANUNUZI KWA MWEZI
1.	NYUKI WAKUBWA	200	5,000/=	1,000,000
2.	NYUKI WADOGO	100	18,000/=	1,800,000
	JUMLA	**300**		**2,800,000**

Kampuni hii ilifanikiwa kununua jumla ya **litre 200** za asali **Nyuki Wakubwa** kwa bei ya jumla ya **5,000/= t.shs** na hivyo ilitumia **1,000,000/= t.shs** kununua **madumu ya asali Nyuki wakubwa.**

Pia kampuni ilifanikiwa kununua **litre 100** za asali **Nyuki Wadogo** kwa bei ya jumla ya **18,000/= t.shs** na gharama ya jumla kuwa **1,800,000/= t.shs.**

RIPOTI YA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA KAMPUNI
JAN. 1. 2020 MPAKA FEB. 1. 2020

Mauzo ya Mwezi.		5,400,000/=
Toa: Manunuzi ya Asali		2,800,000/=
Faida ya Awali (Gross profit)		**2,600,000/=**
GHARAMA ZINGINE ZA MWEZI		
MISHAHARA YA WAFANYAKAZI (2)	460,000/=	
GHARAMA ZA MATANGAZO.	50,000/=	
GHARAMA ZA USAFIRI.	50,000/=	
GHARAMA ZA MAWASILIANO.	50,000/=	
GHARAMA ZA UMEME.	20,000/=	
Chupa tupu za asali (300).	90,000/=	
JUMLA YA GHARAMA ZOTE.		(720,000/=)
PROFIT BEFORE TAX		**1,880,000/=**
Corporate Tax (30%)		**(564,000/=)**
NET PROFIT AFTER TAX		**1,316,000/=**
GAWIO – (DIVIDEND) (40%).		(394,800/=)
RETAINED EARNINGS (60%).		**921,200/=**

VIPENGELE VYA MUHIMU KWENYE RIPOTI YA MAPATO NA MATUMIZI YA KAMPUNI (PROFIT AND LOSS ACCOUNT).

- **MAUZO (SALES)**

Mauzo kwenye **kampuni** yanatokana na **kuuza bidhaa** na **huduma** kwa wateja. Ripoti ya mauzo kwenye kampuni inaweza kuandaliwa kila mwisho wa mwezi kwa kampuni kuzidisha idadi ya bidhaa zilizouzwa na bei ya kila bidhaa. Kwenye mfano wa **ripoti ya Mapato na Matumizi** hapo juu mauzo ya mwezi **ni 5,400,000/- T.shs** iliyopatikana kwa kuuza **asali litre 300** ya **nyuki wakubwa** na **nyuki wadogo.**

- **GHARAMA ZA BIDHAA ZILIZOUZWA (COST OF GOODS SOLD)**

Gharama za bidhaa zilizouzwa ni zile gharama zilizotumika kununua bidhaa au gharama zilizotumika kutengeneza bidhaa. Kwenye ripoti ya hapo juu gharama za asali iliyouzwa ni **2,800,000/= t.shs.**

- **FAIDA YA AWALI (GROSS PROFIT)**

Faida ya awali kwenye kampuni inapatikana kwa kuchukua mauzo ya mwezi kwenye kampuni toa kwa gharama za bidhaa zilizonunuliwa kwa mwezi **(Costs of goods sold)**. Kwenye ripoti ya fedha hapo juu **faida ya awali (gross profit)** ni **2,600,000/= t.shs.**

- **GHARAMA ZA UENDESHAJI BIASHARA**

Gharama za kuendesha biashara au kampuni ni zile gharama zote za kila siku ambazo kampuni itaingia ili kuendesha shughuli za kampuni. Gharama hizo ni pamoja na kulipa mishahara **wafanyakazi, gharama za matangazo, gharama za mawasiliano, gharama za usafiri, gharama za umeme wa ofisini** pamoja na gharama zingine zote za kuendesha shughuli za ofisini kila mwezi. Kwenye ripoti ya hapo juu gharama za jumla za mwezi za kuendesha kampuni ni **720,000/= t.shs.**

- **FAIDA KABLA YA KODI (PROFIT BEFORE TAX - P.B.T)**

Hii ni faida ya kampuni ambayo inapatikana kabla ya makato ya kodi. Faida kabla ya kodi inapatikana kwa kuchukua faida ya awali **(gross profit)** kisha unatoa na gharama zote za mwezi za kuendesha biashara **(operating & administrative expenses).** Kwenye ripoti ya hapo juu faida kabla ya kodi ni **1,880,000/= t.shs.**

- **KODI YA KAMPUNI (30%).**

Kodi ya kampuni ni **asilimia 30%** ya faida yake. Kwenye mfano wa hapo juu faida kabla ya kodi ilikuwa ni sh **1,880,000/= asilimia 30%** yake ni **564,000/= t.shs.**

- **FAIDA HALISI BAADA YA KODI (NET PROFIT).**

Hii ni faida halisi ambayo imebaki kwenye kampuni baada ya makato yote ya kodi. Kwenye mfano wa ripoti ya hapo juu, faida baada ya makato ya kodi ni **1,316,000/= t.shs.**

Kampuni ina maamuzi mawili ya kufanya kwenye faida halisi baada ya kodi. Maamuzi ya kwanza kampuni inaweza kugawa sehemu ya faida Kama **gawio** kwa wanahisa wake au kampuni inaweza **kurudisha fedha za faida**

kwenye kampuni ili **kuongeza uzalishaji** zaidi wa bidhaa na huduma za kampuni husika.

- **GAWIO LA FAIDA (DIVIDEND).**

Ni sehemu ya faida ambayo kampuni inaigawa kwa wanahisa wake. **Gawio la faida** linaweza kuwa ni **asilimia 30%, 40% au 50% ya faida** baada ya baada ya makato ya kodi kwenye kampuni husika. Kwenye ripoti yetu ya hapo juu, aslimia ya gawio la kampuni husika ni **40%** ya faida ya kampuni. Hivyo **394,800/= t.shs** iligaiwa kwa wanahisa wa kampuni husika. **Gawio la faida** huwa nalo linakatwa kodi. Kwahiyo kila mwanahisa kwenye kampuni husika ambae atapata gawio la faida atakatwa **asilimia 10%** ya gawio lake Kama **kodi kwa serikali.**

- **FAIDA ILIYORUDI KWENYE KAMPUNI (RETAINED EARNINGS).**

Hii ni sehemu ya faida iliyorudishwa kwenye kampuni baada ya gawio kwa wanahisa. Kwakuwa gawio kwa wanahisa ni **asilimia 40%** ya faida kwenye ripoti yetu, fedha zitakazo rudi kwenye kampuni **(Retained Earnings)** zitakuwa ni **asilimia 60%** ya faida.

"kampuni huwa zinapenda kurudisha sehemu kubwa ya faida (Retained Earnings) kwenye kampuni ili kampuni iweze kupata fedha nyingi zaidi za kufanya miradi mingine mipya au kuikuza miradi ya awali."

RIPOTI YA MAKADIRIO YA UWIANO WA NAFASI YA KIFEDHA YA KAMPUNI (BALANCE SHEET) FEB .01.2020.

MALI ZA KAMPUNI (ASSETS)		
MALI ZA MUDA MFUPI (CURRENT ASSETS)		
FEDHA MKONONI / BENKI		**921,200 TZS**
ASALI ILIYOUZWA KWA MKOPO	0.0 TZS	
ASALI ILIYOPO (INVENTORY)		
NYUKI WAKUBWA	24,000 TZS	
NYUKI WADOGO	60,000 TZS	
GHARAMA ZILIZOLIPIWA (PREPAID EXPENSES)		
KODI YA JENGO	600,000	
LESENI YA ASALI	53,000	
CERTIFICATE TBS	150,000	
CHUPA TUPU ZA ASALI	90,000	
STICKER ZA ASALI	50,000	
KUDESIGN LOGO	60,000	
BARCODE	220,000	
JUMLA		**1,307,000 TZS**
JUMLA YA MALI ZA MUDA MFUPI		**2,228,200 TZS**

MALI ZA MUDA MREFU (NON-CURRENT ASSETS)		
SAMANI ZA OFISI (VITI, MEZA N.K)	1,000,000	
SIMU YA OFISINI	50,000	
COMPUTER YA OFISINI	300,000	
KABATI YA OFISINI.	250,000	
JUMLA YA MALI ZA MUDA MREFU		**1,600,000 TZS**
JUMLA YA MALI ZOTE		**3,828,200 TZS**

MADENI YA KAMPUNI (LIABILITIES)

MADENI YA MUDA MFUPI (CURRENT LIABILITIES)		
CHUPA TUPU ZA MKOPO	-	
STICKER ZA MKOPO	-	
MKOPO WA BENKI MUDA MFUPI	-	
MKOPO DEBENTURE MUDA MFUPI	-	
JUMLA YA MADENI YA MUDA MFUPI		**0.0 TZS**

MADENI YA MUDA MREFU (NON-CURRENT LIABILITIES)		
MKOPO DEBENTURE MUDA MREFU	-	
MKOPO BENKI MUDA MREFU	-	
JUMLA YA MADENI YA MUDA MREFU		**0.0 TZS**
JUMLA YA MADENI YOTE.		**0.0 TZS**

FEDHA ZA WAMILIKI WA KAMPUNI (SHAREHOLDER'S EQUITY)		
ORDINARY SHAREHOLDERS	2,907,000 TZS	
PREFERENCE SHAREHOLDERS	0.0 TZS	
RETAINED EARNINGS	921,200 TZS	
JUMLA YA FEDHA ZA WAMILIKI		**3,828,200 TZS**
JUMLA MADENI NA FEDHA ZA WAMILIKI		**3,828,200 TZS**

MAELEZO YA RIPTI YA NAFASI YA KIFEDHA YA KAMPUNI (COMPANY BALANCE SHEET).

Ripoti ya nafasi ya kifedha ya kampuni **(Balance Sheet),** inaonyesha uwiano Kati ya mali za kampuni **(Assets)** na madeni ya kampuni **(liabilities)** jumlisha na fedha za wamiliki wa kampuni **(shareholder's equity).**

Kanuni ya balance sheet inasema,

MALI ZA KAMPUNI = FEDHA ZA WAMILIKI + MADENI YA KAMPUNI

Mali za kampuni Zinatakiwa zifanane na fedha za wamiliki wa kampuni ukijumlisha na madeni ya kampuni.

Kwahiyo,

3,828,200 = 3,828,200 + 0

MALI ZA KAMPUNI FEDHA ZA WAMILIKI + MADENI YA KAMPUNI

VIPENGELE VYA (BALANCE SHEET)

MALI ZA KAMPUNI (COMPANY ASSETS).

Ni vitu vyote vyenye thamani fulani ambavyo kampuni husika inavimiliki. Mali za kampuni zinaweza kuwa ni **ardhi ya kampuni**, **magari ya kampuni**, na mali zingine za kampuni zinazoshikika **(Tangible Assets)** na mali za kampuni zisizoshikika **(Intangible Assets).** Kitaalamu Mali za kampuni zimegawanyika katika Makundi mawili makuu. Kuna **Mali za Muda mfupi (Current Assets)** na **Mali za muda mrefu (Non Current Assets)**.

❖ Mali za Muda Mfupi kwenye kampuni (Current Assets).

Ni zile mali ambazo zinaweza kubadilishwa kuwa fedha ndani ya muda mfupi, yani chini ya mwaka mmoja. Mfano wa mali za muda mfupi kwenye kampuni ni kama,

fedha ambazo zipo ofisini au kwenye akaunti ya kampuni, bidhaa za kampuni ambazo zipo tayari kuuzwa kwa wateja **(inventory),** bidhaa ambazo zimeuzwa kwa mkopo kwa wateja **(accounts receivable).** Na mali au huduma ambazo tayari zimeshalipiwa kabla hazijatumika **(Prepaid Expenses)** ndani ya mwaka husika.

Gharama ambazo huwa zinalipiwa kabla **(Prepaid Expenses)** ni kama **kulipia kodi ya jengo** miezi sita (6) au mwaka mmoja kabla haujahamia kwenye jengo husika, **Kulipia Bima** ya mwaka kabla haujaanza kuitumia, **kulipia Malighafi** kabla ya kuwa bidhaa na vitu vingine vyote ambavyo kampuni imevilipia lakini bado haijaanza kuvitumia au muda wa kuvitumia hauzidi mwaka mmoja. Huwa vinahesabika kama ni **mali za muda mfupi** kwenye kampuni.

- **Mali za muda mrefu kwenye kampuni (Non-Current Assets).**

Ni zile mali za kampuni ambazo haziwezi kubadilishwa kuwa fedha ndani ya muda mfupi. Au ni zile mali za kampuni ambazo muda wake wa kutumika ni **zaidi**

ya mwaka mmoja. Mfano wa mali za muda mrefu kwenye kampuni ni kama, **Majengo** ambayo kampuni imenunua, **viwanja** vya kampuni, **Magari ya kampuni, Samani za ofisini za kampuni** kama **Viti, Meza, Makabati** ya kampuni. Pamoja na vitu vyote ambavyo siyo rahisi kuvibadilisha kuwa fedha ndani ya muda mfupi yani chini ya mwaka mmoja huwa zinahesabika kama mali za muda mrefu.

❖ **MADENI YA KAMPUNI (LIABILITIES).**

Ni yale madeni yote ambayo kampuni itakuwa imekopa ili kuendesha shughuli mbalimbali za kampuni husika. Madeni ya kampuni yapo ya aina mbili. Madeni ya muda mfupi **(current liabilities)** na madeni ya muda mrefu **(non-current liabilities).** Kwenye mfano wetu wa hapo juu kampuni haikuwa na madeni yoyote ya muda mfupi na muda mrefu.

******

HITIMISHO

Kila anaemiliki kampuni ni muhimu awe anaanda ripoti za fedha **(Finacial statements)** angalau kila mwisho wa mwezi. Kampuni zinatakiwa kuajiri wahasibu Kwakuwa wamesomea masuala ya mahesabu ya fedha za kampuni. Na kila mwishoni mwa mwaka wa fedha wa kampuni husika.

Kila kampuni inatakiwa kuwasilisha ripoti yake ya fedha **(AUDITED FINANCIAL STATEMENTS**) kwa msajili wa kampuni Kama **Annual Returns.**

MWISHO.

MAREJEO

1. "Presentation of Financial Statements" Standard IAS 1, International Accounting Standards Board. Accessed 24 June 2007.

2. Alexander, D., Britton, A., Jorissen, A., "International Financial Reporting and Analysis", Second Edition, 2005, ISBN 978-1-84480-201-2.

3. Dent, J., Distribution Channels: Understanding and Managing Channels to Market, Kogan Page, 2011, Chapter 1.

4. Armstrong, G., Adam, S., Denize, S. and Kotler, P., Principles of Marketing, Sydney, Australia, Pearson, 2014, pp 297-394.

5. Company's Act (2002).

6. Memorandum & Articles of Associations.

VIFUPISHO VYA MANENO VILIVYOTUMIKA

01. Business Registration and Licence Authority **(B.R.E.L.A).**

02. Tanzania Revenue Authority **(T.R.A).**

03. Tax Identification Number **(TIN).**

04. Mauzo, Manunuzi na Uhifadhi wa bidhaa **(M.M.U).**

05. Copyright Society of Tanzania **(COSOTA).**

06. Tanzanian Shilling **(T.SH)**

07. Tanzania Food and Drugs Authority **(T.F.D.A).**

MAWASILIANO NA OFISI YA GFOX INVESTMENT.

Website: **www.gfox investment.co.tz**

Email: travesgodfrey@yahoo.com

Simu: 0656 - 058184

Instagram: official_mrgodfrey

P.o.box: 404 Dar es salaam, Tanzania.